

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA NANE

---

Kikao cha Tisa – Tarehe 25 Juni, 2012

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

### D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

### MHE. PINDI H. CHANA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

## **MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu Utekelezaji na Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji Pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

## **MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI WA OFISI YA WAZIRI MKUU)**

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Waziri Mkuu Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2012/2012/2013.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 67

### **Mgogoro wa Ardhi Shamba la Malonje**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuza:-

Mwekezaji aliyebinafsishiwa shamba la Malonje (*Malonje Ranch*) alichukua maeneo ya vijiji vyenye mipaka iliyowekwa kisheria, jambo ambalo linazua mgogoro kati yake na vijiji vinavyozunguka shamba hilo la mwekezaji huyo hivi sasa analitumia shamba hilo kwa kilimo badala ya kufuga:-

(a) Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kurejesha maeneo ya vijiji yaliyochukuliwa na mwekezaji huyo ili kuondoa mgogoro uliopo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kumnyang'anya shamba hilo kwa kukiuka masharti ya mkataba kwa kutumia shamba hilo kwa kilimo badala ya kufuga kama ilivyokusudiwa na Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali katika zoezi la urekebishaji Mashirika ya Umma, Mkoa wa Rukwa ulipewa jukumu la kusimamia ubinafsishaji wa shamba la ufugaji wa ng'ombe wa maziwa liliokuwa linamilikiwa na Shirika la Umma la Uendelezaji Ng'ombe wa maziwa.

Ubinafsishaji huu ulifanyika mwaka 2007 kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ambapo mwekezaji (*Efatha Ministry*) alinunua na kulipa shilingi milioni 600 shamba hilo kabla ya kubinafsishwa lilikuwa na ukubwa wa hekta 15,000. Kati ya hizo mwekezaji aliuziwa hekta 10,000 na hekta 5,000 zimegawiwa kwa wananchi wa vijiji vinavyopakana na shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha 23 cha Kamati ushauri ya Mkoa kilichofanyika tarehe 14 Machi, 2012 ilidaiwa kuwa pamoja na mambo mengine kuna mgogoro wa mipaka kati ya shamba la Malonje na baadhi ya vijiji jirani kikiwemo kijiji cha Sikaungu. Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa imeunda Kamati ya Wataalam kufuatilia suala hili na taarifa yao itawasilishwa kwa mkuu wa mkoa kwa hatua zaidi. Hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati suala hili likishughulikiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa inafuatilia uendelezaji wa shamba hilo kulingana na mkataba na kilichobainika ni kutokuwepo kwa mpango mahsus wa uendelezaji na uwekezaji, hivyo kupitia barua Kumb.Na. BA.30/308/1/116 ya tarehe 30 Mei, 2011 mwekezaji alielekezwa kuhakikisha anaandaa mpango wa miaka mitano na matumizi ya shamba hilo.

Tayari rasimu ya awali ya mpango imewasilishwa na inaendelea kuboreshwa. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kufuatilia suala hili ili kuhakikisha mkataba uliowekwa unafuatiwa na kutekelezwa.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na majibu ambayo yanashubiri utekelezaji kwa maana swali langu halijapata majibu. Je, ni lini sasa Serikali itamaliza tatizo hili ili wananchi wawze kutulia na kuendelea na shughuli zao kama kawaida? (*Makofi*)

Swali la pili, shamba la Malonje, liko katika vyanzo maarufu inayotiririka katika Bonde la ziwa Rukwa na maarufu kwa uzalishaji wa kilimo cha Mpunga, mito yenye ni Nzovwe, Momba, Msanda, Mbulu, Mumba, Kisa Songambele Lundi Serikali inanusuluje mito hiyo isikauke kutokana na mwekezaji kulima kwenye vyanzo vyake? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Malocha hiki anachosema hapa asije akafikiri kwamba sisi hatusemi hivyo kwa sababu nimemsikia akisema kwamba anaona kwamba swali hili halijajibowi. Nataka nikuthibitishie kwamba mambo haya anayozungumza Mheshimiwa Malocha ni kweli pale kuna tatizo pale hivi vijiji anavyozungumza hapa viko vijiji tisa ambavyo viko involve katika hili shamba linalosemwa hapa, tumezungumza na RAS Bwana Salum Chima, anakubali kwamba tatizo hili lipo na ndiyo maana walipokutana kwenye *regional consultative committee* ya Mkoa wa Rukwa walikubali kwamba waunde Kamati.

Sasa mimi naisubiri Kamati, Mheshimiwa Waziri Mkuu anasubiri ile Kamati iseme nini ilichoona kule na ndani yake imetakiwa itoe mapendekozo ya nini wanafikiri lifanyike katika tatizo hili ambalo nakiri anachozungumza.

Malocha hapa kwamba ni kweli. Sasa namwomba aone kwamba ni hivyo hivyo vinginevyo nitakuwa nalidanganya Bunge nimwambie tatizo

limekwisha basi nendeni kutoka sasa ninyi chukueni shamba haitawezekana.

Amezungumza habari hii anayozungumza ya kwamba shamba hili linafanya kazi, shamba hili tatizo lililoko hapa ni kwamba shamba hili ni la mifugo na kazi inayotakiwa kufanya kule ni ya mifugo, lakini kinachofanyika kule sasa siyo mifugo kule ni mahindi yanalinwa kule na ndiyo anachosema Malocha, kwa sababu anafikiri kwamba mimi sijaliangalia.

Tunachotaka kupata mkataba, tumesoma mkataba unasema habari ya mifugo na tunamuandikia mwekezaji bwana wewe ulipoleta hapa *business profile* yako ulisema kwamba mimi nitaendeleza mifugo mbona unalima mahindi *simple and clear*, kwa hiyo ile Kamati nayotumewaambia wakaangalie hili jambo.

Sasa ameleta la tatu hapa anasema chanzo cha maji kwamba maji wanamwagilia kule hakuna maji. Mkuu wa Mkoa yuko hapa Mheshimiwa Stella Manyanya, wala hayuko mbali, Malocha na mimi na Stella Manyanya twende tukae nje bwana eeh, kumbe hivi nyle shamba lile shamba mnachukua kutoka kule mmekwenda kuweka kule mnaweka na mifugo huko na ng'ombe wanakaa humo, niachieni hilo tutalishughulikia tutalitatua sisi na Malocha.

Mheshimiwa Spika, na nikumbushe tu Malocha, wakati hili shamba linachukuliwa alikuwa diwani katika Halmashauri ya Sumbawanga kwa hiyo atakuwa ni

mtu muhimu sana wa kutusaidia kuhusu kumbukumbu nini kifanyike katika shamba hili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa hili ni shamba la huko mahali sasa mimi sijui haya mashamba kama wakina Philipa, kumbe hakuwa Philipa aah! Kumbe ni Philipa kumbe mkumbe kama ni shamba lile halafu muanze kuuliza swali lingine sikubali, nimekupa nafasi Mheshimiwa.

Aaah! Mheshimiwa Cecilia Pareso, haya.

**MHE. CECILIA DADIEL PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, kwa kuwa mgogoro kama huu wa Kwela unafanana kabisa na mgogoro uliopo wilaya ya Karatu, ikiwahuisha wananchi na wamiliki wa mashamba ya mikataba hasa katika kata ya Daa na Olidiani. Je, Waziri yuko tayari kuja Karatu na kusikiliza matatizo na kutatua kero hizi zinazowakabili wananchi? Ahsante.

**SPIKA:** Mimi sijaelewa, umesemaji hebu uliza tena.

**MHE. CECILIA DANIEL PARESSO:** Nauliza kwamba kwa kuwa tatizo kama hili linafanana kabisa na tatizo lilioko Karatu, ikiwahuisha wananchi na wamiliki wa mashamba ya mikataba katika kata za Daa na Olodiani wilayani Karatu. Je, Waziri yuko tayari kuja Karatu na kusikiliza kero za wananchi hawa.

**SPIKA:** Lile shamba alipewa mtu afanye mifugo, badala ya kufanya mifugo yeye analima? Halifanani kabisa. Mheshimiwa Kilufi.

**MHE. MODESTUS D. KILIFI:** Mheshimiwa Spika, kwa vile suala la *Ranch* za Taifa kupewa wawekezaji ni sehemu kubwa katika nchi hii ikiwemo Mbarali na kwa vile mashamba hayo hayaendelezwi kama ambavyo ilikuwa imekusudiwa na sijajua Serikali inapata mapato kiasi gani, kiasi kwamba tumeshindwa kuwapa wafugaji ambao wangeweza kulipa mapato hayo Serikalini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hiki anachosema ni kweli, hii anayosema Kilifi anayosema yako maeneo kabisa unakuta mwekezaji amepewa maeneo na kama hili tulilosema la Malocha, unakuta anakwenda anafanya kazi nyingine na bahati nzuri leo tunavyozungumza hapa na wakuu wetu wa mikoa wako hapa wameketi pale wamesikia.

Maelekezo ya Serikali ni kwamba kama mtu amekwenda anafanya kazi nyingine ya ile inayotamkwa kwenye mkataba maana yake amekiuka mkataba na ndani ya Mkataba mle ndani inaonyeshwa pia na namna mkataba utakavyovunjika.

Kwa hiyo, hii anayosema Mheshimiwa Kilifi, kama ana eneo ambalo anajua kwamba hili lina tatizo ni suala la kwenda na kukaa na kuangalia kwamba nini kinachosemwa na kwenda kwenye *ground* wala hatuna haja ya kwenda pale, sisi tutakachofanya tutatuma watu wetu pale waende wakaangalie.

Lakini nataka niseme nichukue nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu sisi hapa tuna

hakikisha kwamba tunasukuma mbele jambo linaloitwa *Public Private Partnership* hatuwezi leo tukakataa hapa tukasema kwamba uwekezaji na sekta binafsi haina nafasi katika nchi hii. Lakini mwekezaji alikuja hapa kwa maelekezo haya ninayotoa hapa, atatakiwa aende akaheshimu mkataba ule, vinginevyo Serikali itatazama tena upya kuhusu mkata huo. (*Makofi*)

Na. 68

### **Kero ya Malimbikizo ya Stahili za Watumishi wa Umma**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Malimbikizo ya stahili za wananchi wa Umma kama vile walimu, wauguzi, askari polisi na kadhalika, imekuwa ni kero kubwa sana.

- (a) Je, ni lini watumishi hao watalipwa malimbikizo ya stahili zao?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kutatua tatizo hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, naomba kutoa maelekezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, malimbikizo na stahili za watumishi hutokana na kupandishwa vyeo uhamisho, ajira mpya, ajira mbadala, likizo na kushinda kesi za makosa ya kinidhamu. Kutokana na taratibu za kiutumishi, mshahara au stahili nyingine hutolewa kwa mtumishi baada ya kukidhi vigezo vinavyohitajika, ikiwemo kukubali cheo au kuwasilisha madai yake rasmi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu maswali Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, yenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 1 Julai, 2011, hadi tarehe 30 Mei, 2012 Serikali ilikwishalipa madai ya malimbikizo ya mishahara yenye thamani ya shilingi bilioni 66,279,154,210.44 kwa watumishi 46 wakiwemo walimu 23,804 ambao walilipwa shilingi bilioni 21,345,370,847.72, watumishi wa afya 7268 walilipwa kiasi cha shilingi bilioni 10,371,885,969, polisi, Magereza na Uhamiaji 1,087 waliolipwa jumla ya shilingi bilioni 1,422,296,266.50 na watumishi na watumishi wengine wapato 14,847 wamelipwa shilingi bilioni 33,139,601,108.22.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua tatizo la kuendelea kwa malalamiko yanayohusiana na madai ya malimbikizo ya mishahara na ambayo yamesababisha hasara pamoja na kupunguza ari ya watumishi wa Umma kufanya kazi. Wizara yangu kwa mwaka wa fedha, 2011/2012 ilianza utekelezaji wa matumizi ya mfumo shirikishi wa taarifa za kiutumishi na

mishahara yaani *Human Capital Management Information System* ambapo kuanzia mwezi Mei, 2011 hadi mwezi Oktoba, 2011 jumla ya maafisa utumishi 413 kati ya 516 sawa na asilimia 78 kutoka katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Idara za Serikali zinazojitegemea, Mamlaka za Serikali za Mitaa, wakala wa Serikali na taasisi za Umma, wamekwishapatiwa mafunzo juu ya kutumia mfumo huu. Aidha, taratibu za kukamilisha mafunzo hayo kwa kundi la maafisa utumishi 113 sawa na asilimia 22 iliyobaki zinaendelea ambapo mafunzo hayo yanatarajiwa kukamilika tarehe 25 Novemba, 2012.

Kwa waajiri ambao maafisa wao tayari wamekwishapata mafunzo haya wanaendelea kutumia mfumo huu kufanya marekebisho katika mishahara ya watumishi wao pamoja na kurekebisha taarifa zingine za kiutumishi na watumishi wa ndani ya ofisi zao.

Kwa kuzingatia uhalali, vielelezo vilivyopo na ofisi yangu imebaki na jukumu la kuidhinisha madai ya usahihi wa taarifa za wahusika moja kwa moja kwa kutumia mtandao. Jambo ambalo linataraja kupunguza kiasi kikubwa tatizo la malimbikizo ya mishahara ya watumishi hapa nchini.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri na mrefu ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mengi ya nyongeza....

**SPIKA:** Hakuna cha mengi, mawili tu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Kwanza, ningependa kujua kuna mkakati gani ambao umewekwa na Serikali ili kuweza kumaliza matatizo na stahiki za mishahara pamoja na kutatua migogoro ambayo imekuwa haiishi na Serikali kuwalipa riba kwa sababu wamekaa na pesa zao kwa muda mrefu?

Serikali ni lini watakuwa tayari kulipa posho kwa mazingira magumu kwa watumishi vijiji ambao wanakuwa wanalipwa na watu ambao wanaishi katika mazingira mazuri mijini pamoja na kuweka mazingira bora ya mahusiano kati ya watumishi na viongozi wao katika maeneo husika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Murtaza Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mikakati ya Serikali ni kama mmoja ambao ni huo wa kuanzisha mfumo wa kompyuta wa kuhakikisha kwamba malimbikizo hayatatokea tena baada ya muda kwa sababu sasa hivi mtumishi akipandishwa cheo Afisa Utumishi aliyefundishwa katika mamlaka husika anahakikisha kwamba ana *feed* taarifa mara moja na zikitufikia Utumishi tunahakiki, baada ya kuhakiki tunazipeleka Hazina kwa ajili ya malipo. Kwa hiyo, baada ya muda mfupi kwa mfumo huu nina uhakika kwamba malimbikizo ya mishahara yatakuwa yamepungua. Mfumo huu unasaidia sana kupunguza urasimu, kupunguza matumizi pia umekuwa ni wa

haraka sana ndiyo maana unaona kwamba watumishi wanaojiriwa upya kuanzia mwaka huu wanapata mishahara mapema iwezekanavyo.

Pia Serikali kwa sasa imeanzisha Bodi ya Mishara ambayo itaanza rasmi tarehe 1 Julai, 2012 katika *financial year* ijayo. Bodi ya Mishahara itaangalia mishahara ya Watumishi wote kwa ujumla wao. Inaitwa Bodi ya Mishahara pamoja na Motisha. Kwa hiyo, Bodi itahakikisha kwamba inaangalia mishahara ya watumishi kwa ujumla wao na siyo mmojammoja kila kada na motisha kwa watumishi wote.

Kuhusu posho ya mazingira magumu, hilo linafanyiwa utafiti na Bodi ya Mishahara itapokea taarifa za nyuma kama zile za Tume ya Mheshimiwa Ntukamazina ili kuhakikisha kwamba wale wanoishi katika mazingira magumu waweze kulipwa posho maalum. Hilo linafanyiwa kazi na hiyohiyo Bodi ya Mishahara watalipwa posho ya mazingira magumu wale ambao wapo kwenye mazingira magumu. Suala la mazingira magumu ni suala pana sana kidogo ni lazima lifanyiwe utafiti siyo tu Wilaya za pembezoni bali ni sehemu nyingi Tanzania zina mazingira magumu, hata Dar es Salaam utakuta baadhi ya sehemu zina mazingira magumu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mehshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, wapo Walimu wenzangu ambao wanapoteza haki ya madai yao kwa vielelezo kupotelea kwenye mafaili ofisini. Je, Serikali itawasaidiaje hawa Walimu ambao wanastahili kabisa

kupata madai yao kwa vile kumbukumbu zimepotelea mikononi mwa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu, naomba yawe mafupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upotevu wa kumbukumbu ni suala gumu kidogo, kwa sababu Serikali yetu inalipa mishahara au inalipa fedha kulingana na *financial regulations* na *financial regulations* lazima uwe na vielelezo vinavyohusika. Sasa kama vielelezo hivi vimepotea itakuwa ni vigumu sana kwa Serikali kulipa fedha hizo kwa sababu itakuwa haina ushahidi.

Lakini kwa mfumo wa sasa hivi ambao tumeufunga Utumishi, kumbukumbu hazitapotea kwa sababu kumbukumbu zote za watumishi zipo kwenye kompyuta, Utumishi pamoja na sehemu za ajira. Ni vema hizo kumbukumbu zikatafutwa ili watumishi hao walipwe lakini bila kumbukumbu nisikudanganye Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaweza tukalipa madai hayo. (*Makofii*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kumekuwa na malalamiko ya watumishi mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama vile Polisi, Walimu pamoja na wengineo kwamba baadhi ya

viongozi wao wamekuwa wanawatisha wanapojitokeza kuweza kueleza juu ya madai mbalimbali ambayo wamekuwa hawalipwi kama vile fedha za likizo.

Ninaomba kujua Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuweza kushirikiana na sisi Waheshimiwa Wabunge ili wafanyakazi ambao wako huru sana kuweza kujieleza kwetu watupatie taarifa hizo na kisha tuweze kuwaletea ninyi na hatimaye kuweza kuwalipa badala ya kutegemea viongozi wao ambao wamekuwa wanawatisha hasa kwa upande wa Polisi kwa mfano Wilaya ya Kasulu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MANEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Machali kama ifuatavyo.

Kwa kweli suala la mwajiri kumtisha mwajiriwa siyo suala jema na kama kuna mtumishi *specific* ambaye ametishwa na ana madai yake ni vema akafuata ngazi zinazohusika ili kupata haki yake. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Polisi na Magereza wengi wamelipwa haki zao na zilikuwa ni za muda mrefu sana lakini mwaka huu tumejitahidi tumehakikisha kwamba wamelipwa haki zao. Kama ana *specific case* ni vema akaniletea ili tuweze kuwaambia Wizara husika au Idara husika tuweze kuyafanyia kazi.

### **Utumiaji wa Lugha ya Alama Nchini**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Watu wenyе ulemavu wa kusikia wana haki ya kusikiliza habari mbalimbali:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kuelekeza na kuhakikisha kuwa watu wenyе ulemavu wa kusikia wanapata huduma hiyo na kuwa na taasisi maalum inayotoa mafunzo ya lugha ya alama?

(b) Je, kwa nini vyombo vy'a Habari na *TV* hazitoi lugha ya alama?

(c) Je, ni lini tutakuwa na lugha ya alama katika mikutano mbalimbali ya viongozi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakiri kwamba upo umuhimu wa kuwepo wakalimani wa lugha ya ishara kwa ajili ya jamii yenye ulemavu wa kusikia. Serikali inazo Taasisi maalum zinazotoa mafunzo ya

lugha ya alama. Baadhi ya vituo hivyo ni Shule za Msingi Buguruni, Sinza Maalum na kadhalika. Vilevile, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı ina Idara ya Elimu Maalum ambayo inashughulikia masuala haya.

Ili kuwezesha vyombo vya habari kutoa lugha ya alama, kwa sasa Serikali inakamilisha marekekebisyoh ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya elektroniki na Posta, 2010 (*Electronic and Postal Communication Act (EPOCA)*) ambazo zitavitaka vyombo vya habari vyote kuwa na wakalimani wa lugha ya ishara.

Mheshimiwa Spika, lugha ya alama inahitaji utaalamu wa elimu ya kipekee kuweza kumudu kutafsiri matangazo kwa ishara na mafunzo yake huchukua muda mrefu kuweza kuhitimu na hivyo idadi ya watu wanaoweza kutafsiri lugha ya ishara ni wanchache sana hapa nchini na pengine duniani kote. Hata hivyo, baadhi ya vyombo vya habari vimekuwa vikitoa habari kwa lugha ya alama kwa baadhi ya vipindi vyake.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada za kuongeza wakalimani wa lugha ya ishara ili wataalamu hao waweze kutumika katika mikutano mbalimbali ya viongozi, suala ambalo litawapa fursa wananchi wote kupata habari.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, pamojana majibu mazuri na mikakati ya Serikali kuhusiana na matumizi ya lugha ya alama, ninapenda kujua kama katika zoezi la kukusanya maoni ya Katiba ambapo kundi hili la walemvu watahusika sana. Je,

Wizara na Serikali imejipanga kuwashirikisha yaani kutumia lugha hizi za alama na makundi yote ya walemavu? (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, kama ifuatavyo:-

Kwa kutambua haki ya wananchi wote kutoa maoni, Serikali ina mpango mkakati kuona kwamba walemavu wanapewa nafasi pekee katika kukusanya maoni kuhusu marekebisho ya Katiba.

**SPIKA:** Ahsante! Mheshimiwa Faida Bakar! Umeacha? Kama umetosheka siyo lazima maana yake na mimi nakosa muda hapa.

Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali! Sikuona kabla Mheshimiwa Mnyika, endelea Mheshimiwa Ngwali!

Na. 70

### **Mashindano ya Olympic Yatakayofanyika London Uingereza**

**MHE. AHMED JUMA NGWALI** aliuliza:-

Je, Serikali kupitia Kamati ya *Olympic Tanzania (TOC)* inakusudia kupeleka washiriki wangapi kuiwakilisha Tanzania katika mashindano ya *Olympic*

ya Dunia yanayotajiwa kufanyika London, nchini Uingereza hivi karibuni?

### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania itawakilishwa na jumla ya wachezaji sita katika mashindano ya *Olympic* yanayotarajiwa kufanyika huko London Uingereza kuanzia mwezi Julai hadi Agost 2012. Kati ya wachezaji hao, wanne watashiriki katika mchezo wa riadha, mmoja katika mchezo wa ngumi na mmoja katika mchezo wa kuogelea. Aidha, timu hiyo itakuwa na Makocha wanenye, wawili wa mchezo wa ngumi, mmoja wa kuogelea na mmoja wa mchezo wa riadha.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, mwezi ujao Tanzania itakuwa mionganini mwa nchi zitakazoshiriki michuano ya michezo ya *Olympic* itakayofanyika Jiji la London nchini Uingereza kuanzia Julai 27 hadi Agosti 12 na kwa kuwa *TOC* imetenga Bajeti ya shilingi milioni 150 tu kwa wanamichezo wetu mwaka huu. Kwa kuwa, Tanzania haijawahi kupata hata medali moja ya dhahabu katika

mashindano hayo makubwa ya *Olympic*, hata medali ya dhahabu kurusha tufe hawajawahi kupata. Je, Serikali kupitia *TOC* inawaahidi nini Watanzania katika mashindano ya *Olympic* ya mwaka huu?

Pili, kwa kuwa *TOC* inafanya kazi katika sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utaratibu usiojulikana kikatiba na kwa kuwa, *TOC* inapata misaada kwa ajili ya wanamichezo kutoka *Olympic Solidarity* si chini ya dola za Kimarekani 100,000 kwa mwaka.

Je, ni utaratibu gani unaotumika na wa wazi katika kuwasaidia wanamichezo hasa wa Zanzibar ambao wanaonekana kutengwa na *TOC*?

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu!

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba maandalizi ya timu hii yamefanywa na Kamati ya *Olympic* kwa kuzingatia vigezo, tuna imani kwamba wachezaji ambao wapo katika Kambi wanaweza wakafanya vizuri katika mashindano hayo yatakayofanyika London Uingereza.

La pili, nataka niseme kwamba Kamati ya *TOC* fedha zake zinakaguliwa na zipo wazi na sisi kama Wizara tuna uwezo wa kuangalia matumizi ya fedha

hizi lakini pia tu niseme kwamba si kwamba hii Kamati ya *Olympic* inaitenga Zanzibar na kwamba Rais wa *TOC* anatoka Zanzibar, Katibu Mkuu anatoka Bara na Katibu Msaidizi anatoka Zanzibar. Kwa hiyo, si kwamba *TOC* inaipendelea Tanzania Bara na kwamba viongozi pia wanatoka katika pande zote za Muungano. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kwa nini tusisitishe kushiriki michuano ya kimataifa kwa sababu michezo ni eneo zuri sana la kuitangaza nchi. Kwa hiyo, tusipofanya vizuri inakuwa ni *opposite* yaani *negative side*. Kwa hiyo, kwa nini tusisitishe kushiriki kwenye michuano ya kimataifa mpaka tutakapokuwa tayari?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbilinyi kama ifuatavyo:-

Mimi nataka niseme kwamba si vema sana kwa Serikali kusitisha timu kushiriki katika michezo ya kaimataifa kwani pia tunapata fursa ya kuitangaza Tanzania lakini kufanya vizuri au kufanya vibaya nacho si kigezo kwamba timu isishiriki bali unapata ushindani na kuelewa matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, nashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hata yeye mwenyewe aendelee kuwahamasisha vijana hata pale wanapofeli katika michezo basi ili wafanye vizuri zaidi. (*Makofi*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba ni sababu gani iliyopelekea kupeleka wanamichezo sita tu wakati Tanzania ina jumla ya watu karibu milioni 45?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu! Twende wote!

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndassa kama ifuatavyo:-

Kamati ya *TOC* inatazama vigezo vilivyowekwa vya kimataifa vya *Olympic* na wachezaji waliokidhi vigezo vya *Olympic* ni haohao sita kwa hiyo tunaona kwamba hao ndiyo wanaofaa pamoja na kwamba michezo ni mingi lakini kwa Tanzania hao ndiyo waliokidhi vigezo vya *Olympic*.

**SPIKA:** Unaona sasa, hili swali limejibiwa vizuri kuanzia Naibu Waziri mwenyewe, waliouliza maswali ya nyongeza, katika muda wa dakika tano tumepata wachangiaji watatu. Ninawapongeza wote waliouliza maswali ya nyongeza katika swali hili. Kwa hiyo, tumetumia muda mfupi. (*Makof*)

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis tunaendelea na Mheshimiwa Susan Kiwanga atauliza swali hilo.

## **Upungufu Mkubwa wa Walimu wa shule za Msingi na Sekondari Nchini**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Kumekuwa na upungufu mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari na wakati huohuo idadi ya watoto wanaoingia shuleni inaongezeka kila mwaka.

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuanzisha vyuo vya Ualimu kwenye Halmashauri nchini ili kukabiliana na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Susan Libweni Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inalitambua tatizo la upungufu wa Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari na inaendelea kulitatua kwa kuajjiri Walimu wote wanaohitimu na kufaulu mafunzo ya Ualimu kutoka Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu viliviyopo nchini.

Mheshimiwa Spika, takwimu za mwaka 2011/2012 zinaonyesha kuwa shule zetu za msingi zina wanafunzi 8,363,386 na Walimu 175,449 ikilinganishwa na majhitaji

ya Walimu 209,085. Hivyo, katika Shule za Msingi kuna upungufu wa Walimu 33,636. Aidha, takwimu za mwaka 2011/2012 pia zinaonyesha kuwa Shule za Sekondari zina wanafunzi 1,789,547 yaani Kidato cha 1 hadi Kidato cha 6 na Walimu 52,146 ikilinganishwa na mahitaji ya Walimu 66,049. Hivyo katika Shule za Sekondari upo upungufu wa Walimu 13,903.

Mheshimiwa Spika, Walimu waliohitimu mwezi Mei, 2012 nchini ni 106 kati ya hivyo 34 ni wa Vyuo vya Serikali na 72 ni vyuo visivyo vya Serikali. Vyuo vya Serikali ni vya Kitaifa na vinachukua wanafunzi kutoka Halmashauri zote nchini. Aidha, vyuo Vikuu na vyuo vikuu vishiriki vnavyotoa programu za ualimuni 29. Hivyo, idadi ya Walimu itaendelea kuongezeka na hatimaye kukidhi mahitaji ya Walimu nchini.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba kwa kuwa kuna tofauti kubwa ya mishahara kati ya Walimu wa ngazi ya cheti na kada nyingine kama kilimo, Madaktari na wengine na kupelekea Walimu kutoridhika na kubaki katika nafasi zao za ualimuna kupelekea upungufu mkubwa Walimu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya Walimu hasa ukizingatia kada ileile ya ngazi ya cheti mishahara ya Walimu iko chini sana na kada nyingine Tanzania?

Pili, hivi karibuni imeripotiwa kwamba kuna Walimu 500 hawajalipwa mishahara yao na mimi nimethibitisha na wapo mashulenii wanaendelea na kazi.

Je, Waziri haoni kwamba Walimu hawa wanakata tamaa pamoja na kuwa unajiridhisha kwamba idadi ya Walimu itazidi kuongezeka? Walimu hawa wataondoka katika fani ya ualimu na kwenda katika fani nyingine ili kuendelea kupata upungufu wa Walimu katika shule zetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu! Ingawa aliondoka kwenye swali la msingi akaenda kwingine!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suzan Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe tu maskitiko makubwa kwa hili swali la nyongeza la kwanza juu ya wasioitakia Tanzania mema, wanaoendelea kutuma *message* kwa walimu wetu wote nchini wakiendelea kupotosha viwango vyatya malipo ya mishahara katika nchi yetu. Serikali kwa ujumla imesikitishwa sana na taarifa ya watu hao wasioitakia amani nchi yetu na kuendelea kuwavuruga Walimu wetu makazini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli yawezekana hayo yanaonekana kuwa ndiyo malalamiko ya Walimu mpaka wanataka hata kutangaza mgomo.

Mheshimiwa Spika, naomba tu unipe dakika moja ili nitaje viwango halisi vyatya mishahara ambavyo vinalipwa na Serikali kuliko hizi *messages* zinazopotosha

Watanzania kwa ujumla. Kwa Walimu wetu nchini kiwango cha mshahara cha Cheti ni shilingi 244,400/= lakini wamepotosha kwamba Wanasheria wanapata shilingi 700,000 wakati Wanasheria katika kiwango cha Cheti wanapata mshahara wa shilingi 262,500/=. Kwa hiyo, huo ni uongo mkubwa. (*Makof*)

Ngazi ya cheti kwa upande wa Muuguzi anapata shilingi 290,000 wakati Mwalimu anapata 244,400/= lakini kwenye *Message* walikuwa wameandika Muuguzi anapata 800,000. Wakati Mwalimu anapopata 244,400/= mtumishi wa Kilimo na Mifugo anapata 221,000 lakini kwenye *message* wameandika 700,000/=. Mhasibu, Mchumi na Mtawala wanapata 221,600 na Mwalimu anapata 244,400/=. Kuna *Messages* zilikuwa zinaendelea kupotosha Walimu kwenye nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi ni ndefu na kama kuna Mbunge yeote anataka kupata ukweli juu ya jambo hili basi ningeomba amwone, na hizi taarifa tutazisambaza kwa Walimu wetu wote nchini ili wasiweze kupotoshwa na maneno yanayotolewa na watu kama hao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Walimu hao 500 ambao hawajalipwa mishahara mpaka sasa, namwomba Mheshimiwa Suzan Kiwanga awe mkweli kama anazo taarifa tupo naye hapa, kila siku tunaonana naye na hata nikitoka hapa anipe majina ya Walimu 500 ambao hawajalipwa mishahara ili tuweze kuwashughulikia haraka iwezekanavyo. (*Makof*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ningependa kuongezea majibu katika lile swali la Mheshimiwa Suzan Kiwanga, kama ifuatavyo.

Watumishi 500 anaosema hiyo namba siyo kweli. Ni Walimu 205 ambao hawajapata mishahara yao na sababu za msingi ni kwamba, *data* zao zilikuja baada ya tarehe 15 Aprili, 2012. *Data processing* inaanza tarehe 1 mpaka tarehe 15 kila mwezi, iwapo taarifa zitakuja tarehe 16 ina maana mtumishi huyu atapata mshahara wake mwezi unaofuata. Kwa hiyo, naomba mnielewe hivyo.

Sababu ya pili ni kwamba, baadhi ya Maafisa Utumishi hawakukamilisha vielelezo kamili vya watumishi hao. Unapoleta *data* zile inatakiwa uambatanishe vielelezo kamili. Viambatanisho vingine havikuambatanishwa. Kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga Walimu 30 taarifa zao hazikuletwa na viambatanisho. Hiyo ndiyo iliyosababisha wakose mishahara. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 72

### **Upungufu wa Walimu wa Hisabati na Sayansi – Bahi**

**MHE. OMARY A. BADWEL** aliuliza:-

Wilaya ya Bahi yenye shule 20 za Sekondari za Kata na Wanafunzi 3,527 ina Walimu 188 tu na

upungufu wa Walimu 184 na mionganini mwa Walimu hao ni 16 tu ndio wanafundisha masomo ya Hisabati na Sayansi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuisaidia Wilaya hii ili iondokane na tatizo hilo la upungufu wa Walimu hususan wa masomo ya Hisabati na Sayansi?

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari A. Badwel, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna upungufu wa Walimu katika baadhi ya shule za Sekondari hapa nchini ikiwemo Wilaya ya Bahi. Hata hivyo, kulingana na takwimu zilizopo kwa mwaka 2011/2012 Wilaya ya Bahi ina walimu 23 wa Sayansi na 17 wa Hisabati. Aidha, Wizara yangu huwapanga Walimu katika Halmashauri kulingana na mahitaji ya kila mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya Walimu wa masomo ya Sayansi Jamii. Kwa mfano katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Walimu wapya waliopangwa vituoni ni 13,639. Kati ya hao Walimu 1,966 tu ndiyo waliosomea masomo ya Hisabati na Sayansi. Hii ni sawa na asilimia 14.4 ya Walimu wote waliopangwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, idadi ndogo ya Walimu wa masomo ya Hisabati na Sayansi inatokana na kuwepo kwa wahitimu wachache wa masomo hayo ikilinganishwa na mahitaji halisi. Aidha, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa Walimu wa masomo ya Hisabati na Sayansi, Wizara yangu kupitia mipango ya MMEM na MMES inatekeleza mikakati mbalimbali ili kupunguza tatizo hili ikiwemo:-

- (a) Kutoa mikopo kwa asilimia 100 kwa Walimu waliochukua Programu za Sayansi na Hisabati ngazi ya Shahada katika Vyuo Vikuu vya Serikali na visivyo vya Serikali;
- (b) Kuanzisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa ambacho kinafundisha programu za Sayansi;
- (c) Kutoa mafunzo ya awali (*bridging course*) kwa wanafunzi wa Kidato cha Sita waliochukua masomo ya Sayansi wenye ufaulu mdogo. Mradi huu unatarajiwu kuanza mwaka 2012/2013 kwa ufadhilli wa Benki ya Dunia. Walimu 1,500 watanufaika na mradi huu na watakuwa ni wa Sayansi tu; na
- (d) Kutoa mafunzo kazini kwa Walimu wanaofundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na *English* kwa shule za msingi na sekondari ili kuinua kiwango cha ufaulu na ufundishaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali itajitahidi

kuongeza idadi ya Walimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati katika Halmashauri zote ikiwemo ya Bahi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Badwel swali la nyongeza, au umeridhika! Kama umeridhika siyo lazima.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, nimeridhika.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa imeonekana ni asilimia 14 tu ya Walimu ambao wanafundisha masomo haya ya Sayansi na Hisabati, na kwa kuwa somo la Hisabati ndiyo somo mama la masomo yote, na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza mikakati mbalimbali, atakubaliana nami kwamba tatizo lipo kwenye mitaala yenye ya kufundishia somo la Hisabati katika shule za msingi na sekondari na tatizo hili limegundulika tarehe 8 na 9 Juni, 2012 Wanahisabati walipofanya mkutano kule Mkoani Morogoro?

Kama hivyo ndivyo je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na lini itahakikisha mitaala ya Hisabati katika shule za msingi na Sekondari inakuwa wazi ili walimu wanaofundisha somo hili na wanafunzi wenye wapate miongozo iliyo sahihi katika kuwekeza kwenye Hisabati? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema kwenye

jibu langu la msingi kwamba kwa mwaka 2011/2012 asilimia 14 ya Walimu tuliowasambaza walikuwa ni wa masomo ya Sayansi kiasi kwamba, ni asilimia ndogo sana. Lakini amejikita katika changamoto kubwa ya vijana wetu kutozingatia somo la Hisabati.

Hii semina anayosema ya *CWT* mimi ndio niliifungua pale Morogoro na Walimu walihutubia vizuri sana na nilipokea maagizo yao na nilikiagiza Chama cha Walimu kwamba, wiki moja hii mtakayokaa Morogoro changamoto zote zinazohusiana na masuala ya Hesabu na nyie ndiyo wataalam maana kulikuwa na Maprofesa na Madaktari pale, watuletee Wizara ya Elimu tuweze kuangalia vizuri na *ku-review curriculum* ya Mtaala wa Hesabu tuone kama hili linaweza likaleta tija kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ujumla tu ni kwamba vijana wetu wa kileo hawapendi sana masomo ya Sayansi huko mashulenii. Hii hali inachangia kabisa, hata ufaulu wa Darasa wa Saba kuingia *Form One* ni mdogo katika masomo ya Sayansi na ufaulu wa kidato cha Nne (IV) kwenda kidato cha Sita (VI) ni mdogo sana kwa *Combinations* za Sayansi. Kwa hiyo nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa kwenye majukwaa huko tuendelee kuwasitiza vijana waweze kupenda masomo ya Sayansi.

Lakini changamoto za Hesabu tunazipokea, na *CWT* wameandaa mkakati wa kutuletea kabrasha tuweze kuona nini walichokijadili ili tuweze kusaidiana. Asante sana.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, eneo kubwa katika Wilaya ya Longido lina mazingira magumu. Kwa hiyo Walimu wanaopangwa katika shule hizo hawataki kwenda. Je, Serikali inaweza kutupa kipaumbele ili wale wanafunzi wanaoomba Ualimu kutoka maeneo hayo wapelekwe kwa sababu wao wanaweza wakahimili mazingira magumu kwa sababu wametokea huko? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, suala hili alilolieza Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, si la jimboni kwake tu. Nimetembelea hata mkoa wa Rukwa, kule Nkasi na Mpanda nimekuta Walimu wengi tuliokuwa tumewapanga mwaka juzi na mwaka jana hawakuripoti. Wiki mbili au tatu zilizopita nilikuwa Kasulu, Kibondo na Kigoma nikakuta nusu ya Walimu waliopangwa kule hawakuripoti.

Tumekaa pale Wizarani tumeanza kuona kwamba labda tubadilishe tu mfumo wa kusambaza Walimu. Labda Halmashauri ziombe Walimu au wale Wanafunzi waweze kufanya *application* kwenye Halmashauri zao tofauti na tunavyowasambaza sasa ambapo mtoto wa Mtwara unampeleka Chunya, wa Chunya unampeleka Dar es Salaam, basi wanashindwa kuripoti. Hata hivyo, hili bado tunaendelea kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, tunapoendelea kuliangalia hilo nimwambie Mheshimiwa Michael Laizer kwamba, kwa kuzingatia maeneo yenu hayo nasema Wabunge wote wenye matatizo ya maeneo magumu ambayo Walimu hawaripoti tuwasiliane nao. Hata ukinipatia taarifa kwamba Walimu hawa wameomba kuja Longido wakati wa kuchagua Walimu kwa ajili ya kuwapeleka kwenye Halmashauri tutazingatia hayo.

Na. 73

### **Biashara ya Vyuma Chakavu**

**MHE. PHILIPA G. MTURANO** aliuliza:-

Biashara ya vyuma chakavu inakuwa kwa kasi sana hapa nchini na imekuwa ni chanzo cha uharibifu wa Miundombinu.

(a) Je, Serikali inakabiliana vipi na tatizo hili hasa uhujumu wa Miundombinu hususan katika Mkoa wa Dar es Salaam?

(b) Je, wanunuzi wa malighafi hii wanaipata wapi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba biashara ya vyuma chakavu imekuwa kwa kasi na imekuwa ni tatizo na chanzo cha uharibifu wa miundombinu hususan katika mkoa wetu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara ilikwisha andaa na kupeleka Waraka wa Baraza la Mawaziri na kupendekeza kutungwa kwa sheria itakayoweka bayana taratibu za mfumo wa usimamizi na udhibiti wa biashara ya chuma chakavu katika hatua mbalimbali za uzalishaji, ukusanyaji, usambazaji, uuzaji na uyeyushaji wake kwa kuzingatia uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa manufaa ya Taifa. Aidha, Muswada huo umeweuka bayana adhabu itakayotolewa kwa mtu atakayebainika kuharibu mazingira na miundombinu.

(b) Mheshimiwa Spika, wanunuzi wengi wa malighafi hii wanaipata kwa utaratibu wa kununua kutoka kwa wakusanyaji na wazalishaji wa malighafi inayotokana na vyanzo mbalimbali. Kwa mfano shughuli za binadamu kama vile vyombo ambavyo matumizi yake hayahitajiki tena kutumika majumbani, viwandani, migodini na watumiaji mbalimbali wa chuma. (*Makofi*)

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

(i) Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake, lakini Wabunge ambao ni

wawakilishi wa wananchi pamoja na wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam, tunapata adha kubwa ambayo inatokana na mashimo makubwa yaliyosababishwa na wizi wa mifuniko ya majitaka.

Maeneo ya Upanga na pale Posta ni hatari sana wakati wa usiku unaweza ukatumbukia wakati unatembea au ukiwa na gari unaweza ukapinduka.

Sasa ni lini basi hii sheria itaanza kufanya kazi kwa sababu imeandaliwa muda mrefu?

(ii) Wanunuzi hawa dola inawafahamu, sasa ni kwanini basi doria haifanyiki katika maeneo ambayo uyeyushaji wa vyuma hivi unafanyika ili kuwabaini watu hawa na wachukuliwe hatua? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, sasa hivi Waraka wa Muswada huu uliishapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri na baraza hilo limeishaujadili na kutoa uamuzi kwamba, sheria hii ya kudhibiti na kusimamia biashara hii ya chuma chakavu itungwe sasa.

Hatua iliyofikiwa sasa hivi ni kwamba, baada ya Baraza la Mawaziri kuleta Muswada ule katika Wizara ili kuweza kufanya marekebisho ya mwisho, Wizara imeisharekebisha na ni wiki iliyopita tu marekebisho haya yamepelekwa kwenye *Cabinet Secretariat* kwa hatua zaidi.

Kwa hiyo, tusubiri waraka huo utakapokuwa umeenda kwa *Attorney General* na hatimaye utakuja hapa Bungeni na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, suala hili la mashimo na usumbufu wake katika sehemu za Posta, Upanga na maeneo mengi ya Dar es Salaam. Ni kweli na ambacho ninaweza kusema sasa hivi ni kwamba, suala hili linahitaji kushirikiana sana na wananchi.

Ningeomba wananchi wote mtoe ushirikiano wenu ili hii biashara na hawa wafanyabiashara waharibifu ambao wanachukua vyuma hivi vizito na nina imani kwamba, chuma kizito hakiwezi kubebwa na mtu mmoja, kinabebwa na watu wengi, sasa endapo mtawaona watu hawa ambao siyo waaminifu wanafanya uharibifu huu naomba sana tushirikiane na vyombo vyaa usalama ili tuweze kukabiliana na suala hili ambalo liko mbele yetu.

Sisi tutajitahidi sheria itakapokuwa tayari tutajaribu kupambana na watu hawa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana! Mheshimiwa Mnyika unatoka huko huko Dar es Saam kwenye mashimo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Ni miezi sita imepita toka Serikali itoe kauli kwa Umma kwamba Muswada wa sheria unaandaliwa na katika kipindi hiki cha miezi sita siyo tu miundombinu ya barabara, bali pia miundombinu ya maji na umeme na mingineyo inaharibiwa.

Lakini vilevile kumekuwa na mfululizo wa taarifa nyingi sana za biashara hizi zikihusishwa na ukwepajji kodi na majina ya makampuni yametajwa hususan na gazeti la Raia Mwema kwa mara kadhaa. Sasa kwa kuwa, sheria nyingine zipo ambazo zinaweza kusimamia jambo hili.

Wakati sheria hiyo ikisubiriwa je, Serikali imechukua hatua gani kutokana na taarifa zililizoandikwa na gazeti la Raia Mwema ambazo zimetaja mpaka majina ya makampuni na watu wanaohusika? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**  
Mheshimiwa Spika, ni kweli sheria hii ambayo tunaipendekeza itachukua muda mrefu na sasa hivi iko kwenye mchakato ambao tunategemea labda baadaye katika vipindi vya Mabunge yajayo huku ndiyo iweze kutungwa.

Lakini mbadala wa sheria ambazo zipo sasa kusema ziweze kusaidia katika kudhibiti hali hii, nafikiri ni pendekezo zuri. Tutaangalia kama tunaweza tukaridhia ili tuweze kuangalia tutumie sheria hizi za zamani.

Lakini rai yangu ni kama nilivyosema kwamba, kikubwa zaidi ni ushirikiano wa wananchi ili tuweze kudhibiti hali hii. Wote vyombo vya usalama, wananchi na hata Waheshimiwa Wabunge suala hili ni wazi linasumbua sana. Tushirikiane kwa pamoja tujaribu kutatua hili wakati tunasubiri sheria mama ambayo inapendekezwa kutungwa.

## **Kuchimba Mabwawa kwa Ajili ya Maji kwa Mifugo**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Kata ya Bukandwe na Nhomolwa ni maarufu kwa ufügaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo lakini maeneo hayo yanakabiliwa na uhaba mkubwa sana wa maji hasa nyakati za kiangazi:-

Je, Serikali ipo tayari kutoa fedha maalum kwa ajili ya kuchimba mabwawa katika Vijiji vya Maguta, Nhungwiza, Nyanhigwa na Kabanga kwa ajili ya maji ya kunywesha mifugo hiyo?

## **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Maselle, Mbunge wa Mbongwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata za Bukandwe na Muhomolwa zina jumla ya ng'ombe 9,495, mbuzi 597 na kondoo 318. Kwa kuzingatia taratibu za kuwawezesha wananchi kuibua miradi ya maendeleo kulingana na vipaumbele wanavyojojiwekea, baada ya kutathmini fursa walizonazo na vikwazo vinavyowakabili au kwa Kiingereza, *Opportunities and Obstacles to Development - O&OD*, Serikali kuanzia mwaka 2005/2006 imewajengea Wafugaji wa Jimbo la Mbogwe malambo 13 kuitia Mipango ya Maendeleo

ya Kilimo Wilayani (*DADPs*), kwa gharama ya shilingi milioni 130 na Bwawa la Ilolangulu kupitia Mradi wa *Rural Water and Sanitation Project* kwa shilingi milioni 84. Aidha, Mradi wa *DASIP* umetekeleza kwa kujenga malambo katikavijiji saba kwa gharama ya shilingi milioni 164. Malambo yaliyojengwa kupitia *DADPs* yapo katika Vijiji vya Ngemo, Kasaka (malambo mawili), Nambubi, Nanda, Lugenga, Bukandwe, Bulugala, Mlange, Isungabula, Nyambale, Bulilila na Buzigula.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe na hatimaye baadaye Halmashauri Mpya ya Wilaya ya Mbogwe, kuzingatia Sera na Mkakati wa *O&OD* na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuhamasisha na kuibua Miradi ya Maji kwa ajili ya mifugo katika Vijiji vya Maguta, Nhungwiza, Nyangwiga na Kabanga, itakayowekwa kwenye Mipango ya Maendeleo ya Wilaya.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Je, Serikali imejipanga vipi kujenga majosho maeneo ambayo yametajwa ya Vijiji vyote vya Mbongwe na Nyang'wale ili kuongeza majosho kwa ajili ya kuosha mifugo?

(ii) Je, Serikali ina mpango gani sasa kufufua Kiwanda cha Ngozi kilichopo Mwanza na kufufua Kiwanda cha Nyama kilichopo Shinyanga ili kunyanyua mapato ya wafugaji hao? Ahsante sana.

## **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Spika, kwanza, utaratibu wa kujenga majosho kama nilivyosema, utaratibu wetu wa *D by D* unazingatia mipango iibuliwe kutoka kule kule vijijini, Halmashauri iratibu na kisha iweke katika Mipango yake. Kwa hiyo, kama tulivyojipanga Kitaifa na katika Wizara, Sera hiyo ndiyo itakayofuatwa, majosho yatakayoibuliwa yatawekwa katika Mpango na yatajengwa katika maeneo ambayo wananchi wameibua.

Swali la pili, Kiwanda cha Ngozi cha Mwanza kipo kwenye mikakati ya *PPP* na hivyo jitihada zinafanyika za kuhakikisha kwamba, kitafanya kazi kama ilivyokusudiwa. Kwa upande wa Kiwanda cha Nyama cha *Triple S* kilichopo Shinyanga, naomba nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, jitihada zitafanyika na kiwanda hicho kilibinafsishwa, lakini kwa muda mrefu hawakuweza kupata fedha za kukijenga japo Kampuni iliyopewa *tender* inaelekea kwamba kwa sasa walisema wanapata mkopo kutoka *TIB* ili waanze kujenga Kiwanda hicho cha Shinyanga cha *Triple S* kwa viwango na kwa awamu kadiri watakavyoendelea kuwa wanapata fedha.

Na. 75

### **Utafiti wa Gesi – Pangani**

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA (K.n.y. MHE. SALEH A. PAMBA)** aliuliza:-

Miaka ya 1990 Kampuni ya AMOCO ilifanya utafiti wa mafuta ya gesi katika eneo la Makarawe Wilayani Pangani:-

Je, ni nini matokeo ya utafiti huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, makofi haya yanatokana na uzushi uliozushwa kwamba nimekatwa mikono. Ninataka niwahakikishie Watanzania wote na hususan Wananchi wa Jimbo la Kibakwe kwamba, siyo kweli ni uzushi mtupu na ni uongo uliokuwa na nia ya kunichafua tu, sihusiani na lolote lile katika suala lililozushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya AMOCO haikuwahi kufanya utafiti wa mafuta katika Mkoa wa Tanga isipokuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*), kwa kushirikiana na Kampuni ya *International Energy Development Corporation (IEDC)* ya Kuwait. *TPDC* na *IEDC* walifanya utafiti eneo hilo ambapo kisima cha utafutaji wa mafuta kilichimbwa katika eneo la Makarawe, Wilaya ya Pangani, Mkoani Tanga mwaka 1984.

Mheshimiwa Spika, kisima hicho kilichimbwa hadi mita 3,821 chini ya ardhi. Aidha, kisima hicho hakikugundulika kuwa na mafuta wala gesi na hivyo kilizibwa na kuachwa (*plugged and abandoned*). Pamoja na matokeo hayo ya Kisima cha Makarawe, TPDC inaendelea na shughuli za utafutaji zaidi wa mafuta na gesi katika maeneo ya Mikoa ya Tanga na Pwani ikishirikiana na Makampuni ya Afren ya Uingereza na Dodsal ya Dubai sawia.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri; je, Serikali inatuambia nini Watu wa Tanga juu ya kuongeza kasi ya utafiti wa mafuta katika Pwani ya Bahari katika Mkoa wa Tanga; na je, mpaka sasa kuna Kampuni ngapi zilizopewa leseni za kufanya utafiti huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa baada ya utafiti huo kuonekana hauna mafanikio, sisi pale Wizarani tunaendelea kupokea watu mbalimbali wenyе nia ya kufanya tafiti na kwa kadiri ambavyo tutawapata basi tutawaelekeza wafanye utafiti katika maeneo hayo. Pia niseme kuwa, wapo katika maeneo mengine ya nchi wakiomba kufanya tafiti, kwa hiyo, siyo rahisi kuwalazimisha watu kwenda kwenye maeneo fulani, lakini watakaokuja tunaweza tukawaelekeza katika maeneo hayo ili kuona kama jitihada zao zinaweza zikawa na matokeo tofauti na yale ya awali.

Na. 76

## Kuandaa Sheria na Sera ya Gesi Nchini

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Kasi ya kusambaza umeme vijijini bado inaendelea kwa kiwango cha kusuasua kutokana na bajeti ndogo ya fedha za kusambaza umeme vijijini:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi na mrefu wa kuongeza vyanzo vypya vyta fedha kwa ajili ya mradi huo wa kusambaza umeme vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Sera, Sheria na Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi. Wizara inashirikiana na Mshauri Mwelekezi, Taasisi ya *Research on Poverty Alleviation (REPOA)*, kwa ajili ya kupitia Rasimu ya Sera ya Gesi Asili. Mshauri Mwelekezi huyo ameanza kazi tangu mwezi Mei, 2012 na anatarajia kukamilisha kazi hiyo mwezi Septemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Rasimu ya Sheria ya Gesi iliandaliwa hata kabla ya kuwepo kwa Sera ya

Gesi, Wizara inakusudia kuiangalia upya ili kujiridhisha kuwa haikinzani na Sera Mpya ya Gesi Asili. Hivyo, inategemewa kuwa Muswada wa Sheria ya Gesi Asili utakuwa tayari umewasilishwa Bungeni mwezi mmoja baada ya Sera ya Gesi Asili kukamilika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maandalizi ya Sera na Sheria ya Gesi, Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Madini na *TPDC* kwa kushirikiana na Mshauri Mwelekezi kutoka Trinidad and Tobago, wapo katika hatua za mwisho za kukamilisha Rasimu ya Mpango huo. Unatarajiwa kukamilika sambamba na Sheria ya Gesi Asili, yaani mwezi mmoja baada ya Sera ya Gesi Asili kukamilika katika kipindi cha miezi sita toka sasa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na kuipongeza Serikali kwa hatua inayoendelea ya kuhakikisha nchi yetu ya Tanzania inapata Sera na Sheria ya Gesi, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha rasilimali hii ya gesi inawanufaisha Watanzania hasa Wanawake na Vijana hata walioko Mikoa ya pembezoni kule Kaisho, Mbambabay, Vikumburu mpaka Busekera Musoma Vijijini?

(ii) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha sasa inawaandaa Wanawake wa Tanzania na Vijana wa Tanzania ili waweze kushiriki katika eneo hili muhimu

sana la uchimbaji wa gesi ili wasiendelee kubaki kuwa watazamaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niseme kwamba, sisi kama Taifa, tunayo furaha kubwa na matumaini juu ya ugunduzi mkubwa wa gesi unaoendelea katika maeneo ya kina kirefu cha bahari na maeneo ya nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, hadi hivi sasa tunavyozungumza, tuna gunduzi zilizopatikana ndani ya nchi karibu 90,000 kwa maana ya *trillion cubic feet* kati ya 35 na 47. Kiasi hicho ni kikubwa sana ni vizuri Taifa likajiandaa katika kupokea gesi, kwa sababu gesi kwa hakika ndiyo itakayoweza kulibadilisha Taifa letu kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, ugunduzi huu ni baraka ya Mwenyezi Mungu na tuna kila sababu ya kujivunia kama Watanzania. Kubwa hapa ni kujijandaa. Sasa niseme tu kwamba, kwa maana ya mkakati wa kuwanufaisha Watanzania kupitia Sera hii ambayo tunaiandaa sasa, ambayo inaandaliwa na Watanzania wenzetu na baadaye kuwashirikisha wadau wote kwa ujumla, imani yangu ni kwamba, tunajitahidi sana kutaka kuweka mazingira ambayo yataweka wazi namna ya kuwanufaisha Watanzania wote katika kupitia ugunduzi wa gesi na matumizi ya gesi katika nchi.

Suala la pili kwamba Wanawake watashiriki namna gani? Tukizungumzia Watanzania wote hapa ni

pamoja na Wanawake, kwa hiyo, niseme tu kwamba gesi itabadilisha maisha ya Watanzania. Gesi itasababisha mbolea na itakuza KILIMO KWANZA, imani yangu kubwa hapa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla ni kwamba, kwa kweli tumshukuru Mungu kwa kutupatia gesi ambayo tunaamini kabisa inaweza kutusogeza kwa matatizo tuliyonayo. Pia tutazalisha umeme mwingi wa kutosha, ambao utatusaidia sana katika kutatua tatizo la umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Jamani m jitendee haki wenyewe mkiwa mnaangalia saa, mkiangalia saa mtajitendea haki wenyewe. Kwa hiyo, maswali yamekwisha na muda pia umepita.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, niwatambulishé baadhi ya wageni tulionao katika Ukumbi wetu leo.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu; kwanza kabisa ni Mama Tunu Pinda, ambaye ni Mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Msaidizi wake. Mnajua leo ni Hotuba ya Waziri Mkuu. (*Makofî*)

Wapo wageni wengine wanne wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni Mchungaji Godfrey Emanuel, Mchungaji Debora Godfrey Malasi, Bwana George Mgina; Bwana George tunamkumbuka ni mtoto wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuna Bwana Gilbert Sampa; ahsanteni sana. (*Makofî*)

Tunao Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote hapa nchini. Naokoa muda sitaki kumtaja mtu mmoja mmoja, kila Mbunge hapa anamjua Mkuu wake wa Mikoa, mkikutana huko nje ulizaneni habari za Mikoa yenu ikoje. Karibuni sana Wakuu wa Mikoa wote na wengine tunawapongeza sana kwa uteuzi wa juzi. Tunaamini kabisa mtaendesha gurudumu la maendeleo katika maeneo mliyonayo kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge walioko hapa. (*Makofi*)

Tunao Madiwani wanne kutoka Rukwa pia ni wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Madiwani wa kutoka Rukwa wapo wapi? Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji wa Mahakama ya Rufani Mstaafu, Mheshimiwa Damian Lubuva, ameambatana na Mjumbe wa Tume hiyo ya Uchaguzi, Mheshimiwa Mchanga Mjaka. Ahsante sana, tunawakaribisheni sana Mheshimiwa Jaji na timu yako.

Pia kuna Viongozi Wakuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, wakiongozwa na Ndugu Peniel Lyimo, ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mku. Ahsante sana.

Tunaye Ndugu Hussein Katanga, Katibu Mkuu wa TAMISEMI; alipo asimame.

Wapo Makatibu Tawala wa Mikoa yote hapa nchini, nao pia naomba wasimame walipo huko wote

kama wapo humu ndani. Ahsanteni sana, tunawakaribisha mkiungana na Wakuu wenu wa Mikoa katika kuendesha gurudumu la nchi yetu.

Tuna Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, wakitajwa waliopo naomba wasimame sijui wapi walipo. Wapo wengi sana, karibuni sana.

Vile vile wapo Wakuu wa Idara na Maofisa wengine kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, wakiongozwa na Bwana Peniel Lyimo. Nashukuru sana.

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, hawa ni Madiwani 50 kutoka Manispaa ya Dodoma wakiongozwa na Mstahiki Meya Simon Miliko. Wako wapi Waheshimiwa Madiwani? Ahsante sana, karibuni sana. Ninyi ni wenyehi wetu, kwa hiyo, mjisikie mko nyumbani kama kawaida.

Tunao Madiwani wengine 36 na Maafisa watatu kutoka Halmashauri ya Kwimba, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Stephania Masangu Wanga. Karibuni sana, poleni na safari.

Tunao Maafisa saba kutoka *OXFAM*, wao wako hapa. Ahsante sana. Mnafanya wapi kazi; karibuni sana.

Tuna wanafunzi wetu 20 kutoka *UDOM*, naomba wasimame walipo. Ahsante, karibuni sana tunawaombeni m jitahidi kusoma kwa sababu Taifa linawasubiri nyinyi zaidi kwa kusoma vizuri. (*Makofi*)

Mwisho wa matangazo ya wageni, sasa shughuli za kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Selemiani Zedi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 25 Juni, 2012, saa 7.00 mchana, kutakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Godfrey Zambi, yeye ni Mwenyekiti wa muda wa watu wanaolima kahawa. Anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa maeneo yanayolima kahawa kwamba, wakutane katika Ukumbi wa Msekwa B, leo saa 7. 00 mchana, mara baada ya kusitisha shughuli hizi.

Nina tangazo lingine ambalo sijawahi kulipata lakini leo lipo; Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Jimbo la Chwaka, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wanaoishi kwenye maghorofa ya *Site One, Two* na *Site Three*, wakutane leo saa saba mchana, kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa; ni muhimu kwa wahusika wote. Sasa hayo mambo siyafahamu, lakini ni wale wanaoishi *Site One, Two And Three*. Sijui kumetokea nini huko kwenye *Site* yenu, kwa hiyo, msikose kuhudhuria hicho kikao.

Waheshimiwa Wabunge, leo katika *Order Paper* yetu, ukianzia pale mwanzo wale wote waliowasilisha nyaraka zao hapa wanapaswa kusoma. Kwa hiyo, ukihesabu Hotuba zinazopaswa kusomwa hapa ni sita. Sasa kwa sababu hiyo, tumekubaliana na wahusika kwamba Kauli ya Waziri Kuhusu Maendeleo ya Mifugo

na Uvubi ambayo ilibidi itolewe sasa hivi naomba itolewe kesho. Zipo Hotuba nyingi mno, zipo sita. Naomba hiyo itolewe baada ya kipindi cha maswali. Kwa hiyo, tunaendelea. Katibu hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa zilizowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Fedha na Uchumi, zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utakelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2011/2012 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2012/2013. Vilevile naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini yake na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, tangu tulipohitimisha Mkutano wa Bajeti wa Bunge hili mwaka jana, Nchi yetu imekumbwa na majanga na matukio mbalimbali yaliyosababisha vifo na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa wote waliofiwa na ndugu, jamaa na marafiki. Mungu azilaze Roho za Marehemu mahali Pema Peponi. Kwa ndugu zetu walioumia na bado wanajiuguza, tumwombe

Mwenyezi Mungu awasaidie kupona haraka na kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nijiunge na wenzangu waliotangulia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya, Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Mei 2012. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Nawapongeza pia Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge waliochaguliwa kuchukua nafasi zilizoachwa wazi. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na Bunge lako Tukufu kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Natarajia kwamba, wote walioteuliwa na kuchaguliwa, watatumia nafasi hizo kwa manufaa ya Bunge na kwa maendeleo ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa takriban siku tano, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili Taarifa Kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2011, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013. Napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu); na Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa (Mb.), Waziri wa Fedha, kwa Hotuba nzuri na ufanuzi wa Hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Vilevile, napenda kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa

kujadili kwa kina Hotuba hizo na hatimaye kupitisha Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipekee, nitumie nafasi hii, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, inayoongozwa na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum. Nawashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, inayoongozwa na Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi. Kamati hizo zimetoa mchango mkubwa wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mfuko wa Bunge. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge lako Tukufu kwa ushauri waliota wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maoni na Ushauri wao utazingatiwa wakati wa utekelezaji wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge ni mwendelezo wa utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010. Vilevile, imezingatia Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mipango na Miradi ya Maendeleo, matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji. Tutatumia rasilimali

chache tulizonazo kwa kazi ambazo zitajielekeza kwenye shughuli za uzalishaji mali na kuongeza tija ili kuchochaea ukuaji wa haraka wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa kwa mwaka 2011 lilikua kwa asilimia 6.4 ikilinganishwa na asilimia 7 mwaka 2010. Ukuaji huo wa asilimia 6.4 ni mkubwa ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambacho kilikuwa wastani wa asilimia 5.1. Kushuka kwa kiwango cha ukuaji uchumi wetu kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukame ambao uliathiri zaidi Sekta ya Kilimo na uzalishaji wa Nishati ya Umeme Nchini. Tatizo la umeme, upungufu wa chakula katika baadhi ya maeneo Nchini pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia vilichangia pia kuongezeka kwa mfumko wa bei. Hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kudhibiti mfumko wa bei ni pamoja na kurejesha upatikanaji wa umeme kwenye hali ya kawaida na kuimarisha ugavi wa chakula Nchini. Hatua hizo zimeanza kupunguza kiwango cha mfumko wa bei. Ni vyema tukumbuke kwamba, hatua za kukabili tatizo la kiuchumi kama vile mfumko wa bei zinapochukuliwa leo, matokeo yake hayawezi kuonekana siku hiyo hiyo. Wataalam wanaeleza kwamba, mara nyingi inachukua miezi 6 hadi 18 kuona dhahiri matokeo ya hatua zilizochukuliwa. Hivyo, siku za usoni tutashuhudia mfumko wa bei ukipungua zaidi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Fedha zina mchango mkubwa katika kuchochaea kasi ya maendeleo na ukuaji wa Uchumi. Kwa kutambua mchango huo,

Serikali inatekeleza Programu ya Maboresho ya Sekta ya Fedha, ambayo imekuwa na mafanikio ya kuridhisha. Mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya Taasisi za Fedha ambazo hadi sasa zimefikia 49 zikiwa na Matawi 519 Nchini kote. Aidha, baadhi ya Taasisi hizo zimeonesha mafanikio makubwa katika eneo la huduma za Kibenki kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imetua msukumo wa uanzishaji wa huduma za Kifedha kupitia Vyama vyta Kuweka na Kukopa (*SACCOs*), ambavyo hadi sasa vimefikia 5,346. Vyama hivyo vimetua mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 627.2. Pamoja na mafanikio hayo, changamoto kubwa inayoikabili Sekta ya Fedha ni viwango vikubwa vyta riba kwenye Mikopo vinavyoendelea kutozwa na Benki za Biashara ikilinganishwa na riba ndogo inayolipwa kwa amana. Changamoto nyingine ni kukosekana kwa Taasisi nyingi za fedha zinazotoa Mikopo ya muda mrefu yenye masharti nafuu kwa Miradi ya Maendeleo hasa kwenye Sekta ya Kilimo. Serikali inatambua Changamoto hizo na tayari Mikakati inaandaliwa kukabiliana nazo hususan kuanzisha Dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali Tanzania pamoja na kukamilisha mchakato wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuanzisha Mfumo wa kuwatambua wakopaji (*Credit Reference Bureau*).

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba zangu za Bajeti za miaka miwili iliyopita, nililijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi

ambayo itafanyika tarehe 26 Agosti, 2012. Nilianza kutoa Taarifa ya Sensa mapema kwa kuwa Sensa ni mchakato unaohitaji maandalizi ya muda mrefu kabla na baada ya zoezi lenyewe la kuhesabu Watu. Kwa kutambua umuhimu wa Sensa katika kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Nchi, zoezi hili limepewa kipaumbele cha pekee katika Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2012/2013. Katika Awamu ya Kwanza ya maandalizi ya Sensa, kazi zilizofanyika ni pamoja na kutenga maeneo ya kuhesabia Watu, kutayarisha Madodoso na Miongozo mbalimbali, kufanya Sensa ya Majaribio, kununua vitendea kazi, kuchapisha Nyaraka za Sensa na kuunda Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kazi za Sensa zinazoendelea ni uhamasishaji na kutoa Elimu kwa Umma ili kila Mwananchi ashiriki kikamilifu katika zoezi hilo. Shughuli nyingine ni utoaji wa mafunzo kwa watakaokuwa Makarani wa Kuhesabu Watu na Wasimamizi, usambazaji wa vifaa na maandalizi ya kuingiza takwimu kwenye Kompyuta. Katika utekelezaji wa zoezi hili, Serikali itawatumia Watumishi mbalimbali wa Serikali wakiwemo Walimu. Kutokana na sababu hiyo, Serikali imelazimika kubadili Mihula ya Shule ili Walimu waweze kusaidia katika zoezi hili la Sensa.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Viongozi wote tusaidiane kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa zoezi la Sensa katika maeneo yetu. Nawaomba Wananchi wote washiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi kwa kutoa ushirikiano na taarifa sahihi kwa Makarani wa Sensa na Wasimamizi ambao

wata tembelea Kaya zetu tarehe 26 Agosti, 2012. Ni wahakikishie Wananchi wote kuwa, taarifa zote zinazokusanywa wakati wa Sensa ni Siri na zitatumika kwa shughuli za Kitakwimu tu. Takwimu hizo hazina uhusiano na Dini, Kodi, Siasa au mambo mengine kama hayo ambayo hayakukusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mwamko mkubwa wa Wananchi kushiriki kwenye masuala ya Kisiasa, hali inayoashiria kukua kwa Demokrasia Nchini. Vyama vipya vya Siasa vimeendelea kusajiliwa na vili vyopo kujiimarisha zaidi. Katika mwaka 2011/2012, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imepokea maombi ya kusajili Vyama vipya Viwili vya Siasa. Chama cha Kijamii (CCK) kimepata Usajili wa Kudumu na kufanya idadi ya Vyama vyenye Usajili wa Kudumu kufikia 19. Chama cha *Alliance for Democratic Change (ADC)* kimepata Usajili wa muda na Chama cha *Movement for Democratic and Economic Change* kinaendelea kufanyiwa uhakiki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kushughulikia maombi ya Usajili wa Vyama, kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010. Aidha, itafuatilia uhai wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa Sheria na kuanzisha Ofisi mbili za Kanda. Kanda hizo ni ile ya Kusini inayojumuisha Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma na Kanda ya Magharibi inayojumuisha Mikoa ya Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi. Nitumie nafasi hii kuwasihhi Watanzania kutumia fursa ya kupanuka kwa Demokrasia kuendelea kushiriki

kwenye Siasa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Nchi. Viongozi wa Vyama vya Siasa waoneshe mfano wa kuendesha Siasa za kistaarabu zenyelengo la kuunganisha Watanzania na siyo kuwachonganisha. Hakuna Nchi au Kiongozi aliyewahi kupata sifa nzuri kwa kuwa chanzo cha mifarakano. Tudumishe utulivu na amani pamoja na ustaarabu wetu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa katika Mkutano wa Tano wa Bunge, mwezi Novemba 2011, Bunge lako Tukufu lilitipisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 8 ya Mwaka 2011 (Sura ya 83). Aidha, Bunge lilitanya marekebisho ya Sheria hiyo katika Mkutano wa Sita, mwezi Februari 2012. Hatua hiyo, ilimwezesha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuteua Wajumbe wa Tume itakayoratibu na kukusanya Maoni ya Wananchi kuhusu Mabadiliko ya Katiba. Tume hiyo yenye Wajumbe 32 inajumuisha Wawakilishi wa Makundi mbalimbali katika jamii kutoka pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Tume imeanza kazi rasmi tarehe 1 Mei, 2012, kama ilivyopangwa. Serikali imefanya maandalizi muhimu kuiwezesha Tume kufanya kazi yake ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuipatia Vifaa vya Kisasa vya kukusanya na Kutunza Kumbukumbu na kufungua Tovuti rasmi. Aidha, Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali imepewa jukumu la kuchapisha kwa wingi Katiba na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ili Wananchi waweze kuelewa na kutoa

michango yao kwa uhakika zaidi kwenye mchakato wa kutoa maoni.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na Mheshimiwa Augustino Ramadhani, Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania, kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti. Vilevile, napenda kuwapongeza Wajumbe wote, wakiwemo Katibu na Naibu Katibu kwa kuteuliwa kuunda Tume hiyo. Napenda kuwasihhi Wananchi wajitokeze kwa wingi na kutoa maoni yao kwa utulivu katika Mikutano itakayoitishwa na Tume na kuwapa Wajumbe ushirikiano wa kutosha ili hatimaye tupate Katiba ilioandikwa na Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Aprili, 2012, Muungano wetu ultimiza Miaka 48 ya Watanzania kuishi pamoja, kwa amani na utulivu. Katika mwaka 2011/2012, Vikao 14 vya Kisekta vya Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) villifanyika kutafuta ufumbuzi wa changamoto za Muungano. Kikao cha Kamati ya Pamoja cha SMT na SMZ, chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kilifanyika ambapo Hoja 13 zilijadiliwa na Hoja Mbili zilipatiwa ufumbuzi. Hoja zilizopatiwa ufumbuzi ni kuhusu ongezeko kubwa la Ankara za umeme kutoka *TANESCO* kwenda *ZECO* na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Aidha, imekubalika kuwa marekebisho ya Sheria

yafanyike mapema ili kupata ufumbuzi katika hoja zinazohusu Usajili wa Vyombo vya Moto, Kodi ya Mapato na Kodi ya Zuio (*Withholding Tax*).

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine ambazo zipo katika hatua mbalimbali za kutafutiwa ufumbuzi zitaendelea kujadiliwa katika Vikao vya Kamati ya pamoja vya Kisekta na Kamati ya Pamoja. Serikali pia itaendelea kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kwa kuhakikisha kwamba Sekta, Wizara na Asasi Zisizo za Muungano zinakutana na kujadili changamoto zilizopo. Ni ukweli usiopingika kwamba, Muungano wowote Duniani unakutana na changamoto mbalimbali. Jambo muhimu ni pande zote zinazounda Muungano kuzitatua changamoto hizo. Hivyo, ni vyema tukaendelea kukaa pamoja na kujadiliana ili Muungano wetu huu ambao msingi wake ni mahusiano ya kihistoria ya pande zote mbili uendelee kudumu kwa faida ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, Bunge. Katika mwaka 2011/2012, Bunge limetekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya msingi ya kutunga Sheria na kuisimamia Serikali. Kamati za Kudumu za Bunge pia zimetekeleza majukumu yake ipasavyo na Bunge zima limefanya Mikutano minne kwa mujibu wa Sheria. Katika Mikutano mitatu iliyofanyika, Miswada ya Sheria nane ilipitishwa na Maswali ya kawaida 373 na ya Nyongeza 894 ya Waheshimiwa Wabunge yalijibiwa na Serikali. Aidha, Maswali ya Msingi 78 ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa na kujibiwa. Hoja mbalimbali za Kamati za Kudumu za Bunge ziliwasilishwa na kujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Ofisi ya Bunge itakarabati Ukumbi wa Bunge na kuboresha miundombinu mingine ya Ofisi zake ikiwa ni pamoja na kuweka Vifaa vya Mawasiliano na kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo. Aidha, huduma za Utafiti na Sheria zitaimarishwa sambamba na shughuli za Kamati za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Sekta Binafsi, Uwekezaji na Uwezeshaji; Maendeleo ya Sekta Binafsi; Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi ili iweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali na kufanya biashara na hatimaye kuwa Injini ya Ukuaji wa Uchumi. Katika kufanikisha lengo hilo, Serikali inasimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini wenyе lengo la kurekebisha mifumo iliyopo ili kupunguza ghamama za kufanya biashara na kuwekeza Nchini. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na uanzishaji wa Kituo Kimoja cha Utoaji wa Huduma kwenye Bandari ya Dar es Salaam, ambapo muda wa mizigo kukaa Bandarini umepungua kutoka wastani wa siku 25 mwaka 2009 hadi kufikia wastani wa siku 9 mwezi Mei 2012.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kupunguza vizuizi vya kudumu katika Barabara Kuu, kuunda Kamati za pamoja kwenye Vituo vya Mipakani mwa Nchi (*Joint Border Post Committees*), kuendelea na taratibu za kuanzishwa kwa Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja Mipakani (*One Stop Border Posts*) na kuweka mkazo kwenye matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki

kwenye maeneo ya ulipaji kodi, mabenki, usajili wa makampuni na utunzaji wa kumbukumbu kwenye masjala mbalimbali. Sambamba na hatua hizo, majadiliano na Sekta Binafsi yamefanyika kwa lengo la kupata ufumbuzi wa changamoto za Kisera, Kisheria na Mifumo ya Kitaasisi zinazoikabili Sekta hiyo. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itafanya tafiti zinazohusiana na maendeleo ya Sekta Binafsi, pamoja na kuendeleza mashauriano na Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo na Taasisi Zisizo za Serikali kwa lengo la kuiwezesha Sekta Binafsi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji; katika mwaka 2011/2012, Serikali imefanya juhudini kubwa za kuhamasisha na kuvutia Wawekezaji wa Ndani na Nje. Kutohana na juhudini hizo, Kituo cha Uwekezaji Nchini kilisajili jumla ya Miradi 681 yenye thamani ya shilingi trillioni 11.6 na fursa za ajira 89,803. Kati ya Miradi iliyosajiliwa, Miradi 356 sawa na asilimia 52.3 ni ya Wawekezaji wa Ndani, Miradi 166, sawa na asilimia 24.4 ni ya Ubiammo kati ya Wawekezaji wa Ndani na Nje na Miradi 159, sawa na asilimia 23.3 ni ya Wawekezaji wa Nje. Mitaji ya moja kwa moja ya Wawekezaji wa Nje (*FDI*), iliyointingizwa Nchini imeongezeka kutoka shilingi billioni 681.2 mwaka 2010 hadi trillioni 1.3 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza kasi ya Uwekezaji Nchini kuitia Sera ya Ubiammo kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Serikali imefanya maandalizi ya msingi ya kuanzisha Kitengo cha Uratibu wa masuala ya Ubiammo kwenye Kituo cha Uwekezaji na Kitengo cha Fedha (*PPP – Finance Unit*) kwenye Wizara ya Fedha. Jumla ya Miradi 125 iliyoinishwa na Wizara

mbalimbali itafanyiwa uchambuzi zaidi na Vitengo hivi ili kubaini kama inakidhi vigezo vyta kutekelezwa chini ya utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Miradi hiyo ni pamoja na ile ya kuzalisha umeme, ujenzi wa barabara, reli, bandari na ujenzi wa majengo kwa ajili ya ofisi na biashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweuka umuhimu wa kipekee kuhamasisha ushiriki wa Wawekezaji wa Kitanzania kuanzisha Miradi ya Uwekezaji katika Mikoa na Wilaya kwa kuandaa Makongamano na Mikutano ya Kuhamasisha Uwekezaji na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa Wawekezaji Wadogo. Hadi sasa, Mikutano ya kuhamasisha Uwekezaji imefanyika katika Mikoa ya Ukanda wa Ziwa Tanganyika ya Rukwa, Katavi na Kigoma pamoja na Mikoa ya Mara, Singida, Arusha na Mbeya. Aidha, Wilaya za Mbinga, Njombe, Mufindi, Mbozi na Kahama nazo zimefanya Mikutano hiyo. Mikutano ya Kikanda ya Uwekezaji itaendelea kufanyika katika mwaka 2012/2013. Nahimiza, Viongozi wa Mikoa na Wilaya kuandaa Mikutano hiyo na kuondoa vikwazo vinavyokwamisha uwekezaji katika maeneo yao. Ofisi ya Waziri Mkuu itasambaza Mwongozo kwa Mikoa ili ishirikiane ipasavyo na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa Mikutano ya Uwekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kushiriki katika Mikutano mbalimbali inayohusu masuala ya uchumi, biashara na uwekezaji. Mwezi Mei 2012, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa *World Economic Forum* – Addis Ababa na baadaye katika Mkutano wa Nchi Nane Zilizoendelea katika Viwanda (G8) huko

Washington, Marekani. Katika mikutano hiyo, Serikali ilielezea Mipango yetu ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo Nchini, hususan Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT*). Mipango hiyo ilipokelewa na kukubalika ambapo Tanzania imeingizwa katika Mpango wa G8 wa Kuendeleza Kilimo Barani Afrika. Nchi nyingine Barani Afrika zilizokubalika kushiriki katika Mpango huo ujulikanao kama G8 *The New Alliance for Food Security and Nutrition* ni Ethiopia na Ghana. Chini ya Mpango huu, Tanzania itanufaika na misaada ya shilingi trilioni 1.41 kwa ajili ya kuwekeza katika Sekta ya Kilimo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Uongozi wake mahiri na juhudni zake za kuhakikisha kwamba Nchi yetu inakuwa moja ya Nchi Tatu Barani Afrika zitakazonufaika na Mpango huo. Hii inathibitisha kuwa ziara za Mheshimiwa Rais Nje ya Nchi mara nyingi zina manufaa makubwa kwa uchumi na maendeleo ya Nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kuainisha Miradi itakayoteklezwa na Wawekezaji wa Ndani na Nje katika Ukanda wa *SAGCOT* yameanza. Kutokana na ukubwa wa Ukanda huo wa Kilimo, Miradi itakayoainishwa itatekelezwa kwa Mfumo wa Kongano (*Clusters*), ambapo Wakulima Wadogo watashirikiana na Wawekezaji Wakubwa kuendeleza Kilimo.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kuona matunda mazuri yaliyotokana na ushirikiano kati ya Wawekezaji Wakubwa na Wakulima Wadogo katika kuongeza uzalishaji na tija. Hali hii imejionesha dhahiri kwenye Kilimo cha Mpunga huko Kilombero ambapo Kampuni ya *Kilombero Plantations Limited* iliyowekeza kwenye Shamba la Mngeta Wilayani Kilombero, imewasaidia Wakulima Wadogo kupata Teknolojia rahisi ya kupanda na kupalilia mpunga. Wakulima hao wamewezechwa kuanzisha vikundi vyta uzalishaji na kukopeshwa mbegu bora. Kutokana na ushirikiano huo, uzalishaji wa mpunga kwa Wakulima Wadogo umeongezeka kutoka wastani wa tani mbili hadi tani saba kwa hekta moja. Utaratibu wa namna hiyo pia unatumwa na Mwekezaji wa Kampuni ya Sukari Kilombero na umewanufaisha Wakulima Wadogo wa Miwa Wilayani Kilombero kuitia vikundi vyao vyta uzalishaji. Ushirikiano wa aina hiyo unatoa fursa za Masoko na Usindikaji wa Mazao yanayozalishwa na Wakulima Wadogo wanaozunguka mashamba ya Wawekezaji Wakubwa. Hii ni dalili njema kabisa na mfano wa kuigwa na Wawekezaji Wakubwa na Wakulima Wadogo Nchini.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Watanzania wenzangu kuona uwekezaji mkubwa katika Kilimo kama fursa muhimu ya kuongeza uzalishaji na tija. Jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba, maslahi ya Wakulima Wadogo yanalindwa kwa kuwekeana mikataba mizuri na kufuatilia utekelezaji wake. Ni imani yangu kwamba, tukiitumia vizuri ardhi yenye rutuba tuliyonayo tutaweza kuongeza ukuaji kwenye Sekta ya

Kilimo ambayo ni tegemeo kwa Watanzania wengi na hatimaye kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004 kupitia Programu na Mifuko mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Aprili 2012, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (*Mwananchi Empowerment Fund*), umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 7.3 kwa Wajasiriamali 7,187 katika Mikoa ya Dodoma, Lindi, Manyara, Mtwara, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Singida na Tanga. Sehemu kubwa ya mikopo iliyotolewa ilitumika kugharamia shughuli za kilimo ikijumuisha ununuzi wa pembejeo na zana za kisasa za kilimo na umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), katika mwaka 2011/2012, Miradi 878 yenye thamani ya shilingi bilioni 18.6 iliyobiuliwa na Wananchi kwenye Halmashauri zote Tanzania Bara na Zanzibar ilitekelezwa. Vilevile, hadi kufikia Desemba 2011, Mfuko huo umetoa shilingi bilioni 1.14 kwa walengwa 14,000 kupitia utaratibu wa uhawilishaji fedha katika kaya maskini. Aidha, mafunzo ya ujasiriamali yametolewa kwa vikundi 500 Nchini katika Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar. Vile vile, Wajumbe 8,780 wa Kamati za Usimamizi wa Mradi na 13,500 wa Kamati za Serikali za Vijiji na Mitaa walipata mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2012/2013, Serikali itaanza utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya

TASAF Benki ya Dunia imepitisha shilingi bilioni 345.4 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huo utakaotekelizwa kwa kipindi cha miaka mitatu. Serikali pia itasimamia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili Wajasiriamali wengi zaidi wanufaik. Aidha, Serikali itawahamasisha Wananchi kuweka akiba, kuwekeza na kutambua na kutumia fursa za kiuchumi zilizopo ili kuongeza kipato na ajira.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa mkakati wa kuhimiza Kilimo cha Kisasa kinachotumia Kanuni Bora za Kilimo, Zana za Kisasa na msukumo kwenye Kilimo cha Umwagiliaji ndiyo njia ya uhakika ya kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo. Aidha, ushirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi ni nguzo muhimu ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo. Jitihada za Serikali katika mwaka 2011/2012 zilielekezwa katika vipaumbele hivyo pamoja na kuongeza upatikanaji na matumizi ya Pembejeo na Zana Bora za Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Serikali iliimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo hasa mbolea, mbegu bora na madawa ya mimea. Jumla ya Vocha milioni 5.3 za Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo zilisambazwa kwa Kaya milioni mbili Nchini. Lengo la Serikali ni kuongeza upatikanaji wa pembejeo ili kuwanufaisha Wakulima wengi waweze kuongeza tija, uzalishaji na kipato. Kama nilivyoahidi kwenye Hotuba yangu ya mwaka 2011/2012, tayari Serikali imefanya Ukaguzi Maalum kuhusu utoaji wa Ruzuku za Pembejeo kwenye Kilimo kwa utaratibu wa Vocha. Kutokana na matokeo ya awali ya ukaguzi huo, TAKUKURU imefungua Kesi 19 kwa wale

waliobainika kufanya ubadhirifu na udanganyifu katika utoaji wa Vocha za Pembejeo za Kilimo. Pamoja na hatua hiyo, Serikali itaboresha mfumo wa sasa wa utoaji wa Vocha za Pembejeo kwa kubuni mfumo mwingine ambao utaondoa upungufu uliojitokeza katika mfumo unaotumika hivi sasa. Lengo ni kuhakikisha kwamba, Vocha zinawafikia walengwa kwa wakati na zinatumika kwa madhumuni yaliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, Serikali kupitia SUMA JKT ililingiza Nchini matrekta makubwa 1,860 na zana zake; matrekta madogo ya mkono 400 na pampu za umwagiliaji 1,100 kupitia mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya India. Ili kuwawezesha Wakulima wengi zaidi kumudu bei ya matrekta hayo, Serikali imeamua kupunguza bei ya matrekta hayo kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, bei ya trekta moja la *Horse Power 50* imepunguzwa kutoka shilingi milioni 25.6 hadi milioni 16.5 na trekta la *Horse Power 70* imepunguzwa kutoka shilingi milioni 45.8 hadi milioni 38.8. Natoa wito kwa Halmashauri, Vyama vya Ushirika, Vikundi vya Wakulima na Wananchi kutumia fursa hii kununua matrekta hayo. Aidha, jana baada ya kushauriana na Halmashauri husika, tullaifikiana kuwa Halmashauri ziangalie uwezekano wa kuwapunguzia zaidi Wakulima kiwango cha asilimia 30 wanachotakiwa kuchangia katika ununuzi wa matrekta ya SUMA JKT ili waweze kupata matrekta hayo kwa bei nafuu zaidi. Lengo ni kuhakikisha kuwa, matrekta hayo yanawafikia Wakulima wengi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imekarabati miundombinu ya skimu 32 za umwagiliaji zenyе ukubwa wa hekta 17,824. Aidha, kazi ya ujenzi wa mabwawa 8 ya maji inaendelea na upembuzi yakinifu wa Miradi 25 ya Umwagiliaji yenye eneo la hekta 17,113 umefanyika. Kutokana na juhudи hiso, eneo la umwagiliaji Nchini limeongezeka kutoka hekta 331,490 mwaka 2010/2011 hadi hekta 345,690 mwaka 2011/2012. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itashirikiana na Wadau wa Maendeleo kuwawezesha Wakulima 33,108 katika Skimu 20 za Umwagiliaji zenyе hekta 15,431 kulima Zao la Mpunga kibiashara kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Mheshimiwa Spika, llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010 ilielekeza Serikali iandae Programu Kabambe ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo ambayo itajumuisha uendelezaji wa malisho, kuchimba na kujenga malambo, mabwawa na majosho na huduma za ugani ili hatimaye Wafugaji waondokane na ufgaji wa kuhamahama. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta ya Mifugo imeandaa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo. Kukamilika kwa Programu hii kutaiwezesha Sekta ya Mifugo kutoa mchango zaidi kwenye Pato la Taifa na kuwanufaisha Wafugaji. Mafanikio ya Programu hii yatategemea sana Wadau wa Sekta ya Mifugo kuzingatia Sheria Na. 13 ya Mwaka 2011 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu inayohusu maeneo ya malisho na rasilimali ya vyakula vya mifugo. Nawahakikishia Wananchi kwamba, Serikali itasimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria hii na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo ili kuleta

mabadiliko kutoka kwenye uchungaji kwenda kwenye ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imetoa Ruzuku ya shilingi bilioni 1.6 zilizotumika kununua na kusambaza lita 62,500 za dawa za kuogesha mifugo na dozi milioni 3.5 za chanjo ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe katika Halmashauri zote Nchini. Serikali pia imeendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali kujenga na kukarabati majosho 108 na malambo 98. Aidha, Kituo cha Taifa cha Uhamilishaji kilichopo Usa River, Arusha na Vituo Vitano vya Kanda vya Afya ya Mifugo vimeimarishwa. Serikali itaendelea kutoa Ruzuku ya Dawa za Mifugo na kuhamasisha Wafugaji na Wafanyabiashara kuwekeza zaidi kwenye Ufugaji wa Kisasa na unenepeshaji Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi, katika mwaka 2011/2012, Serikali ilianza kutekeleza Mkakati wa Uendelezaji Ukuzaji Viumbe kwenye Maji kwa kuimarishe Ufugaji Samaki na ukuzaji wa Viumbe vingine. Utekelezaji wa Mkakati huo, umeongeza idadi ya mabwawa ya kufugia samaki kutoka 19,039 mwaka 2010/2011 hadi 19,443 mwaka 2011/2012, na Vituo vya Kuzalisha Vifaranga vimeongezeka kutoka 8 hadi 10 ambapo jumla ya vifaranga milioni 1.9 vya samaki vimezalishwa na kusambazwa kwa Wadau. Aidha, elimu ya usimamizi na matumizi endelevu ya Rasilimali za Uvuvi imetolewa katika maeneo ya Wavuvi. Vikundi 188 vilihamasishwa kufanya shughuli mbadala kwa kupatiwa elimu ya ujasiriamali ambapo Miradi Midogo 459 ya kiuchumi imeanzishwa. Katika mwaka

2012/2013, Serikali itafanya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 1997 na kuandaa mkakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ufugaji Nyuki ina mchango mkubwa katika kuondoa umaskini na kuhifadhi mazingira. Kwa kuzingatia fursa kubwa tuliyonayo ya Rasilimali za Ufugaji Nyuki, Serikali imeziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa zote Nchini kuanzisha Mashamba Darasa ya kutoa Elimu ya Ufugaji Nyuki. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya Wafugaji Nyuki 4,573 kutoka Wilaya 33 walipewa mafunzo ya Ufugaji Bora wa Nyuki. Aidha, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wamepewa mafunzo kuhusu Ufugaji Bora wa Nyuki ili waweze kuwa chachu ya uhamasishaji katika Mikoa na Wilaya kuhusu manufaa ya ufugaji nyuki. Kutokana na jitihada hizo, katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa asali ulifikia tani 9,500 zenye thamani ya shilingi bilioni 27 na nta iliyozalishwa ilikuwa tani 600 zenye thamani ya shilingi bilioni tatu. Aidha, tarehe 9 Juni, 2012 nilipata fursa ya kufungua Kiwanda kipyaa na cha Kisasa cha kuchakata asali kilichoengwa na Kampuni ya *Honey King Limited* katika Kijiji cha Visiga Mkoani Pwani na hivyo kufanya jumla ya Viwanda vya kuchakata na kufungasha asali Nchini kufikia vinane. Napenda kuwapongeza Wawekezaji hao kwa kujenga Kiwanda chenye uwezo wa Kuchakata tani 10,000 za asali kwa mwaka. Nawaomba Wafugaji Nyuki kuitumia vizuri fursa hii kwa kuzalisha Mazao ya Nyuki kwa wingi na yenye ubora ili kunufaika na soko la kuaminika la Kiwanda hicho na vingine vilivyopo hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kutoa elimu ya Ufugaji Nyuki kwa Wadau mbalimbali. Aidha, ili kutangaza ubora wa asali na nta ya Nchi yetu, yatafanyika Maonesho Maalum ya Mazao ya Ufugaji Nyuki mwezi Oktoba 2012. Maonesho hayo yataandaliwa kwa ushirikiano baina ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Viwanda na Biashara, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania na Wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza utekelezaji wa Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani Mazao na Huduma za Kifedha Vijiji (*Marketing Infrastructure Value Addition and Rural Finance Program - MIVARF*) mwezi Julai, 2011. Kazi zilizotekeliza ni pamoja na kuandaa mfumo wa utekelezaji ikiwemo uundaji wa Kamati za Usimamizi, ununuzi wa vitendea kazi, kuajiri wafanyakazi na kuitambulisha Programu katika Mikoa yote. Aidha, uchambuzi wa Maandiko ya Miradi iliyopokelewa kutoka Halmashauri mbalimbali umefanyika na Halmashauri zitakazoanza kushiriki katika utekekezaji wa Programu zimechaguliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, kilometa 250 za barabara za vijiji zitakarabatiwa, maghala mawili yatajengwa na manne yatakarabatiwa. Vilevile, vituo vinne vya mafunzo ya uongezaji thamani mazao vitakarabatiwa; Wakulima watapatiwa mafunzo kuhusu hifadhi ya mazao, mbinu za kuyafikia masoko na Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuviendeleza Vikundi 864 vya Kifedha vikiwemo

VICOBA, kuzijengea uwezo SACCOS 108 pamoja na Asasi nyingine ndogo za Kifedha ili ziweze kutoa Huduma za Kifedha Vijiji kwa ufanisi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango na umuhimu wa Sekta ya Viwanda katika kuleta maendeleo endelevu, kuongeza ajira, kuongeza thamani ya mazao, kukuza masoko, kuongeza Mapato ya Serikali na fedha za kigeni. Kwa kuzingatia umuhimu huo, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na uhamasishaji wa Uwekezaji wa Viwanda Vipya katika Maeneo Maalum ya Uzalishaji (*EPZ*) na Maeneo Maalum ya Uchumi (*SEZ*). Idadi ya Makampuni yaliyosajiliwa katika maeneo hayo imeongezeka kutoka 44 mwaka 2010/2011 hadi 54 mwaka 2011/2012. Uwekezaji wa Mitaji umeongezeka kutoka shilingi trilioni 1.02 hadi trilioni 1.1. Pia, mauzo ya nje yameongezeka kutoka shilingi bilioni 560.5 hadi bilioni 706.5 na Ajira zimeongezeka kutoka 13,500 hadi 15,100.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali itaimarisha Sekta ya Viwanda kwa kuhimiza uwekezaji katika Viwanda vya kuongeza thamani ya mazao na bidhaa za kilimo na kuwaunganisha Wakulima na wenyewe Viwanda ili kuwawezesha kupata soko la uhakika. Aidha, itaendelea kuweka umuhimu katika utekelezaji wa Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali zenyelengo la kuboresha Sekta ya Madini ili Taifa linufaike zaidi na rasilimali hiyo. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha Shirika la Madini la Taifa

(*STAMICO*) ili liweze kuchukua Hisa kwa niaba ya Serikali katika Migodi Mipyä inayotarajiwa kuanzishwa. Kupitia utaratibu huo, *STAMICO* inamiliiki asilimia 45 ya hisa katika Mgodi wa Backreef na asilimia 55 zinamiliikiwa na Mwekezaji. Hatua nyingine ni kuwawezesha Wachimbaji Wadogo kuanzisha Vituo vya kuwasaidia kukopeshwa na kununua Vifaa vya Kisasa vya kuchimbia Madini katika maeneo ya Rwamgasa - Geita, Londoni - Manyoni na Pongwe - Bagamoyo. Aidha, kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini Nchini, shughuli za Ukaguzi katika Migodi mikubwa zimeimarishwa na sasa Migodi mingi imeanza kulipa Kodi ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imechukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba Makampuni yote Makubwa ya Madini yanalipa mrabaha wa asilimia nne kwa kuzingatia matakwa ya Sheria Mpya ya Madini Na. 14 ya Mwaka 2010. Makampuni ya Madini ambayo hayajazingatia matakwa haya ya Kisheria yametakiwa kulipa malimbikizo yote tangu Sheria hiyo ilipopitishwa mwaka 2010. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, hakuna Kampuni ya Madini ambayo itakwepa kulipa mrabaha kwa kiwango kipyä na kodi zote kama inavyotakiwa.

Tutakuwa makini kuhakikisha kwamba, Sheria na Taratibu za Biashara ya Madini na Hifadhi ya Mazingira zinafuatwa na kila Mmiliki wa Mgodi. Napenda kutoa wito kwa Wachimbaji Wadogo, jamii inayozunguka Migodi Mikubwa na Wamiliki wa Migodi Mikubwa, kushirikiana kwa karibu na kila mmoja atimize wajibu

wake ili kuleta mahusiano mazuri na kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudini zinazoendelea za kutangaza Vivutio mbalimbali vya Utalii, idadi ya Watalii imeongezeka kutoka 782,699 mwaka 2010 hadi 867,994 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 11. Mapato yatokanayo na Utalii yameliingizia Taifa shilingi trilioni 2.14 mwaka 2011 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.96 mwaka 2010. Serikali pia, imeandaa Programu ya Kutunza na Kuweka Kumbukumbu za Urithi wa Malikale ili kupanua wigo wa Vivutio vya Utalii.

Hatua hii itaiwezesha Tanzania kutangaza zaidi maeneo ya urithi wa Utamaduni wetu pamoja na Maeneo 22 ya Wapigania Uhuru kwa ajili ya Ukombozi wa Bara la Afrika. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaongeza kasi zaidi ya kutangaza Vivutio vya Utalii wetu nje ya Nchi, kwa kutumia Balozi zetu na Tovuti; kuwavutia Wawekezaji wa Nje na Ndani katika Sekta ya Utalii na kuhamasisha Utalii wa Ndani.

Mheshimiwa Spika, Vijana ndiyo sehemu kubwa ya nguvu kazi katika Nchi yetu. Inakadirisha kuwa asilimia 35 ya Watanzania wote ni Vijana wenyewe umri kati ya miaka 15 hadi 35. Aidha, Vijana ni asilimia 68 ya Watanzania wote wenyewe nguvu na uwezo wa kufanya kazi. Jitihada kubwa za Serikali zinaendelea kuwekwa katika kutoa msukumo kwenye uwekezaji katika sekta zenye fursa kubwa ya kutoa ajira nyingi kama vile kilimo, mifugo, uvuvi, ufugaji nyuki, ujenzi, mawasiliano, uchukuzi, utalii na viwanda. Aidha, ili kuwawezesha

Vijana kupata mitaji, Serikali imeongeza mtaji kwa Benki ya Rasilimali, Benki ya Wanawake, Benki ya Posta na Mifuko mbalimbali ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Vilevile, Mafunzo ya Ujasiriamali na Elimu ya Ufundu Stadi kwa Vijana waishio Mijini na Vijiji yataimarishwa kwa lengo la kuwaongeza sifa katika Soko la Ajira hasa Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa uhakika wa tatizo la ajira hususan kwa Vijana utatokana na jitihada za makusudi za kuongeza uwekezaji katika sekta zote. Napenda kutoa rai kwa Viongozi na Watendaji wote kwenye ngazi ya Taifa, Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuhakikisha kwamba wanaongeza jitihada za kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji na kuongeza kasi ya ukuaji wa Sekta Binafsi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali muhimu katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Hata hivyo, ili kunufaika na Rasilimali hiyo, ni muhimu ardhi ipimwe na kuwa na Mpango endelevu wa matumizi bora ya ardhi. Kwa kuzingatia umuhimu huo, hadi kufikia Aprili 2012, mipaka ya Vijiji 11,261 ilipimwa, Vyeti vya Ardhi ya Vijiji 3,283 villitolewa, upimaji wa Viwanja 26,788 na Mashamba 706 ulifanyika na Hati za Hakimiliki za Kimila 46,063 zilitolewa na kufanya jumla ya Hati za Hakimiliki za Kimila zilizokwishatolewa Nchini kote kufikia 157,968.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha Wananchi kunufaika na Rasilimali Ardhi wanayomiliki, Serikali itakamilisha Mradi wa Kuweka Kituo cha Kupokea Picha za Satellite (*Direct Satellite Imagery Receiving*

*Station).* Kituo hicho kitawawezesha Wananchi kupimiwa ardhi yao na kupatiwa hati kwa vile upimaji na utayarishaji wa ramani kwa ardhi yote Nchini utakuwa umerahisishwa kwa kiasi kikubwa. Huu utakuwa ukombozi wa kiuchumi kwa Watanzania wengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kujenga Mtandao Mpya wa Alama za Msingi za Upimaji Ardhi Nchini (*National Geodetic Control Network*). Alama hizo zinatarajiwa kuanza kutumika mwezi Julai, 2012. Mtandao wa Alama hizo, utarahisisha upimaji wa ardhi kwa matumizi mbalimbali na kupunguza gharama za upimaji Nchini.

Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2011, Serikali iliwasilisha Bungeni Mpango wa Dharura wa Kuondoa Mgao wa Umeme uliokuwepo Nchini. Mgao huo ulisababishwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa uzalishaji hasa kwenye vyanzo vya umeme vya maji. Kutokana na utekelezaji wa Mpango wa Dharura wa Umeme, hadi kufikia mwezi Aprili 2012, jumla ya Megawati 342 zimezalishwa na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Uzalishaji huo umeimarisha hali ya upatikanaji umeme na hivyo makali ya mgao kupungua. Hata hivyo, uzalishaji wa Umeme wa Dharura ni wa gharama kubwa kutokana na mitambo mingi kuendeshwa kwa kutumia mafuta ya dizeli.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuendelea na hali hii ya uzalishaji umeme kwa gharama kubwa huku tukiwa na Rasilimali zinazoweza kubadili kabisa hali hiyo. Kwa hiyo, Serikali imeanza kutekeleza Mradi Mkubwa wa

Ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza kiasi cha Gesi itakayotumika kuendesha Mitambo ya Uzalishaji Umeme. Tayari fedha za kutekeleza Mradi huu zimepatikana na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka 2012/2013.

Serikali pia katika mwaka 2011/2012 imetoa shilingi bilioni 39 ikiwa ni sehemu ya mchango wake katika ujenzi wa Mradi huo. Fedha nyingine kiasi cha shilingi bilioni 110 zimewekwa katika Bajeti ya 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambayo Serikali imechukua kutatua tatizo la Umeme Nchini ni kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika uzalishaji na usafirishaji wa umeme. Kwa kuanzia, Serikali inashirikiana na Serikali ya Marekani kubaini vikwazo vinavyozuia Sekta Binafsi kuwekeza kwenye Miradi mikubwa ya Umeme. Kazi hiyo itafuatiwa na utekelezaji wa Mpango Maalum wa Pamoja wa Miaka Mitano utakaoanza kutekelezwa mwaka 2012/2013. Lengo ni kuzalisha umeme wa MW 2,700 ifikapo mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Umeme Vijijini unatekeleza Programu Kabambe ya Kusambaza Umeme Vijijini katika Mikoa 16. Mikoa hiyo ni Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya, Rukwa na Tabora. Chini ya Programu hiyo, Miradi Midogo 41 inatekelezwa ambapo wateja 22,000 watalipiwa gharama za kuunganisha umeme kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini. Programu hiyo itawawezesha Wananchi wengi zaidi

vijijini kupata nishati ya umeme ili kuharakisha maendeleo katika maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada za Serikali za kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Nishati, kasi ya utafutaji na ugunduzi wa hazina mpya ya Gesi Asili Nchini imeongezeka. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hivi karibuni Makampuni yanayofanya utafiti wa Gesi Asili Nchini yamegundua kiasi kikubwa cha Gesi Asili yenye futi za ujazo trillioni tatu. Gesi hiyo imegundulika kwenye kina cha maji marefu baharini takriban kilometa 80 kutoka Nchi kavu Mashariki mwa Mkoa wa Lindi. Ugunduzi huo unafanya kiasi cha Gesi kilichogundulika hadi sasa kwenye kina cha maji marefu baharini kufikia futi za ujazo trillioni 20.97. (*Makof*)

Kwa kuzingatia fursa zinazotokana na kasi kubwa ya ukuaji wa Sekta ya Gesi Nchini, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika kikamilifu na ugunduzi wa rasilimali hiyo. Serikali inaandaa Sera na Sheria Mahususi ya Gesi Asili pamoja na Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi kwa lengo la kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sekta hiyo. Aidha, Serikali itawawezesha Vijana wetu kupata Mafunzo Maalum (*Specialized Training*), yanayohusiana na masuala ya Gesi Asili kwa lengo la kupata Wataalam Wazalendo waliobobea kwenye sekta hii kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); Nchi zote Duniani zimeazimia

kubadili Teknolojia ya Utangazaji kutoka Analojia kwenda Dijitali ambayo imeonekana kuwa na tija na yenye kutumiwa na vifaa vingi zaidi vya mawasiliano. Kwa kuzingatia Azimio hilo, Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki nazo zimekubaliana kutekeleza mabadiliko hayo na kuanza Kurusha matangazo katika mfumo wa dijitali pekee ifikapo tarehe 31 Desemba 2012. Ili Watanzania wawe tayari kuyapokea mabadiliko hayo, Serikali imeandaa mpango wa kuelimisha Umma unaojulikana kwa jina la "*Digital Tanzania*" ambao ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Agosti 2011. Wananchi wote watambue kwamba mabadiliko ya teknolojia za utangazaji kutoka analogia kwenda dijitali ni matokeo ya ukuaji wa kasi wa Teknolojia ya Mawasiliano ambao hatuwezi kuuepuka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Awamu ya Pili ya Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa wenye urefu wa kilomita 3,000 umekamilika na kuanza kutumika. Kukamilika kwa Awamu hii kunafanya Nchi yetu kuwa na Mkongo uliojengwa wenye jumla ya kilometa 7,300 na kumeiwezesha Mikoa yote ya Tanzania Bara kuunganishwa kwenye Mkongo huo. Aidha, Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa umeunganishwa na Kisiwa cha Pemba kupitia Tanga. Katika mwaka 2012/2013, Kisiwa cha Unguja kitaunganishwa na Mkongo huo kupitia Dar es Salaam, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Mkongo wa Majini.

Mheshimiwa Spikakatika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea kujenga, kukarabati na kuzifanyia matengenezo Barabara Kuu za Mikoa na Wilaya ili ziweze kupitika wakati wote. Hadi mwezi Mei 2012, Serikali imejenga jumla ya kilometra 305.6 za Barabara Kuu na kilometra 29.5 za Barabara za Mikoa kwa kiwango cha lami.

Pia, imefanya ukarabati mkubwa wa kilometra 78.4 za Barabara Kuu kwa kiwango cha lami na kilometra 463.2 kwa kiwango cha changarawe katika Barabara za Mikoa. Aidha, jumla ya kilometra 7,209 za Barabara za Mamlaka ya Serikali za Mitaa zimefanyiwa matengenezo ya kawaida. Vilevile, ujenzi wa Daraja la Nangoo lililopo Mtwara na Daraja la Malagarasi Mkoani Kigoma umeanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali imepanga kujenga kilometra 414 na kukarabati kilometra 135 kwa kiwango cha lami na kujenga madaraja 11 katika Barabara Kuu. Vilevile, itajenga kilometra 573 kwa kiwango cha changarawe na kilometra 32 kiwango cha lami katika Barabara za Mikoa pamoja na Madaraja 27.

Katika kipindi hicho, Mfuko wa Barabara unatarajiwa kuingiza zaidi ya shilingi bilioni 400 ambazo zitatumika kwa ajili ya matengenezo, ujenzi na usimamizi wa Miradi mbalimbali ya Barabara, zinazosimamiwa na *TANROADS* na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma katika Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na kukarabati Bandari za Kigoma na Mwanza. Aidha, imekamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari Mpya ya Mbegani (Bagamoyo) na Mwambani Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali iliweka Menejimenti Mpya ya Shirika la Reli (*TRL*) inayoongozwa na Wazalendo. Serikali pia ilitoa fedha za kukarabati miundombinu chakavu ya Reli ya Kati ikiwa ni pamoja na ukarabati wa injini za treni na mabehewa ya abiria. Aidha, kazi ya usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa (*Standard Gauge*) na kuiunganisha na Nchi za Rwanda na Burundi imeanza mwezi Februari 2012 na inatarajiwa kukamilika Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania, Zambia na Jamhuri ya Watu wa China, mwezi Machi 2012, zimesaini Mikataba yenye Thamani ya shilingi bilioni 66.67 kwa ajili ya kuboresha miundombinu na huduma za *TAZARA*. Mikataba hiyo itatekelezwa kuanzia mwaka 2012/2013. Jitihada hizo zitawezesha huduma za Reli kuimarika na hivyo kutoa mchango mkubwa katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Huduma Za Jamii; katika mwaka 2011/2012, Serikali imeanza kufanya Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995 kwa lengo la kuiboresha ili kuendana na Mazingira ya sasa. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwaka

2012/2013. Aidha, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ambapo jumla ya madarasa 485 na nyumba za Walimu 344 zilijengwa na madawati 61,363 yalinunuliwa.

Katika kipindi hicho, jumla ya Walimu 11,243 walijiriwa na 2,259 walipewa mafunzo kazini ili kuongeza ubora wa ufundishaji wa Masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza. Lengo ni kuwajengea Walimu uwezo wa kufundisha na hatimaye kuongeza kiwango cha ufaulu wa Wanafunzi katika masomo hayo.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sekondari, katika Mwaka 2011/2012, utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Elimu ya Sekondari (MMES II) umekuwa na mafanikio ya kuridhisha. Jumla ya madarasa 1,316, maabara 127 na nyumba za Walimu 270 zilijengwa na madawati 123,855 yalinunuliwa. Katika kipindi hicho, jumla ya Walimu wa Sekondari 13,900 wameajiriwa na Vitabu Milioni 1.5 vilinunuliwa na kusambazwa katika Shule mbalimbali za Sekondari. Wanafunzi waliojiunga na Kidato cha Kwanza wallongezeka kutoka 456,350 Mwaka 2011 hadi 517,993 Mwaka 2012. Hili ni ongezeko la Wanafunzi 61,643.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya Shule za Sekondari ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Jitihada zitaongezwa katika kuhamasisha ujenzi wa madarasa zaidi kwa ajili ya Wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha Tano na Sita kukidhi mahitaji makubwa yaliyojitokeza baada ya kupanuliwa kwa Elimu ya Sekondari Nchini.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Ufundı Stadi yana mchango mkubwa katika kuwapatia ujuzi na kuwajengea uwezo Wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Msingi na Sekondari. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imekamilisha ujenzi wa Vyuo vya Mafunzo ya Ufundı Stadi katika Mikoa ya Lindi, Pwani, Manyara, Arusha na Dar es Salaam.

Kukamilika kwa Vyuo hivyo kumeongeza idadi ya Wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Ufundı kutoka 72,938 mwaka 2010 hadi 102,217 mwaka 2011. Katika Mwaka 2012/2013, Serikali itapanua zaidi Mafunzo ya Ufundı Stadi Nchini.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu, katika mwaka 2011/2012, Serikali ilitekeleza Mpango wake wa kuimarisha miundombinu ya Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Juu Nchini. Kutokana na hatua hiyo, Udhili wa Wanachuo katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki uliongezeka kutoka Wanachuo 40,993 mwaka 2005/2006 hadi 139,638 mwaka 2010/2011. Idadi ya Wanachuo waliopewa mikopo ya elimu ya juu ikijumuisha Wanachuo wa Vyuo Vikuu na Vyuo vingine uliongezeka kutoka 42,729 mwaka 2005/2006 hadi 93,784 mwezi Aprili 2012. Aidha, katika kipindi hicho, fedha zilizokopeshwa Wanachuo hao ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 56.1 hadi bilioni 291. Katika

mwaka 2012/2013, Serikali itatoa kipaumbele katika kuongeza ubora wa Elimu ya Juu ili kuendana na mahitaji ya Soko la Ajira Nchini na katika Jumuiya ya Afrika Mshariki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya, katika mwaka 2011/2012, Serikali imetekeleza Mpango wa Kugawa Vyandarua vyenye Dawa ili kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa malaria. Hadi Desemba 2011 jumla ya Vyandarua milioni 17.6 viligawanywa bila malipo kwa kila Kaya yenye watoto wenyе umri chini ya miaka mitano nchi nzima. Sambamba na hatua hiyo, Mpango wa Kunyunyizia Dawa ya Ukoko aina ya /CON kwenye kuta za Nyumba ili kuua mbu ulitekelezwa katika Wilaya 18 za Mikoa ya Kagera, Mwanza na Mara ambayo imeonekana kuwa na Maambukizi makubwa ya Malaria.

Mheshimiwa Spika, aidha, jitihada za kuongeza upatikanaji wa dawa mseto za kutibu malaria kwa bei yenye punguzo zinaendelea. Jitihada za udhibiti wa malaria zimechangia kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 99 kwa kila watoto 1,000 mwaka 1999 hadi vifo 51 kwa kila watoto 1,000 mwaka 2010. Vile vile, vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 147 kwa kila watoto 1,000 mwaka 1999 hadi vifo 81 kwa kila watoto 1,000 mwaka 2010. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuangamiza Viluwiluvi vya Mbu kwa kutumia njia za kibaiolojia kwa ushirikiano na Serikali ya Cuba. Mpango

huo ulianza mwaka 2011 kwa majaribio katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, Serikali itaandaa mkakati maalum wa kugawa vyandarua kupitia shulenii ili kuhakikisha kuwa matumizi ya vyandarua yanakuwa endelevu. Natoa wito kwa wananchi wote kutumia vyandarua vinyavyotolewa na Serikali kwa lengo lililokusudiwa badala ya matumizi mengine. Vile vile, nawahimiza kutokomeza mazalia ya mbu na kuweka mazingira katika hali ya usafi ili tufanikiwe kuondoa ugonjwa wa malaria nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kupunguza idadi kubwa ya wagonjwa wa moyo wanaopoteza maisha kwa kukosa tiba stahiki na gharama kubwa inayotumika kupata tiba hiyo nje ya nchi. Ili kutekeleza dhamira hiyo, katika mwaka 2011/2012, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imekamilisha ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Upasuaji, Tiba na Mafunzo ya Ugonjwa wa Moyo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Pamoja na mafanikio hayo, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili iliendelea kutoa huduma za upasuaji mkubwa wa moyo ambapo hadi mwezi Aprili, 2012, jumla ya wagonjwa 300 walipata huduma hiyo na hivyo kuokoa zaidi ya Shilingi bilioni sita (6) ambazo zingetumika kuwapeleka wagonjwa hao nje ya nchi. Napenda kuwapongeza Madaktari na Wahudumu wote wa Afya kwa huduma nzuri wanayotoa kwa wagonjwa. (*Makofii*)

Nawasihi kuendelea na moyo huo, kwani wamepewa dhamana kubwa ya kuwashudumia wananchi kutokana na ujuzi na weledi walio nao.

Mheshimiwa Spika, huduma kwa Watu wenye Ulemavu, katika mwaka 2011/2012, Serikali imekamilisha zoezi la kuandaa Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu iliyopitishwa na Bunge mwaka 2010. Utekelezaji wa Sheria hiyo umeanza ambapo watu wenye ulemavu wanapatiwa haki na huduma za msingi ikiwemo elimu, afya, ajira na kulindwa kisheria. Kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, Serikali kwa kiasi kikubwa imedhibiti vitendo vyatukatili walivyokuwa wanafanyiwa. Napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa wananchi wote kuwapenda na kuwahudumia walemovu wakiwemo Watu wenye Ulemavu wa Ngozi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lishe, katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2011/2012, nililitaarifu Bunge kuhusu hali isiyoridhisha ya lishe hapa nchini na hatua ambazo Serikali umeanza kuzichukua kukabiliana na hali hiyo. Napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa, Mkakati wa Kitaifa wa Lishe ulizinduliwa rasmi tarehe 20 Septemba, 2011. Mkakati huo umeainisha maeneo ya kipaumbele ambayo yatakelezwa katika kipindi cha miaka mitano ili kupunguza idadi ya watoto wenye uzito pungufu, udumavu, pamoja na idadi ya wanawake wajawazito wenye upungufu wa damu.

Mheshimiwa Spika, ili kuliongezea uzito suala la lishe, Kamati zitakazohakikisha kwamba Mkakati wa lishe unatekelezeka kikamilifu zimeanzishwa katika ngazi ya Taifa na Halmashauri. Napenda kutoa msisitizo wa kipekee kwamba lishe bora ni muhimu kwa maendeleo ya watu na Taifa kwa ujumla. Lishe duni ina madhara makubwa hasa kwa watoto wadogo;

mtoto mdogo anapokosa lishe bora, maendeleo yake katika masomo yana walakini mkubwa na hali hiyo haiwezi kurejeshwa tena. Hivyo, Watendaji katika ngazi zote watoe umuhimu mkubwa kwenye suala la lishe bora kwa kuendelea kutoa elimu ya lishe bora ili wananchi walielewe na wale chakula chenye virutubisho muhimu ambavyo viro kwenye maeneo mengi nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji, Serikali imeboresha huduma ya maji Vijijini kwa kujenga Miradi mipyä, kupanua na kukarabati iliyopo kwa kushirikisha wananchi. Katika mwaka 2011/2012, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*) iliendelea na utekelezaji wa mradi wa maji katika Wilaya za Moshi Vijijini na Hai. Vilevile, kwa kushirikiana na Serikali ya Japan iliendelea kutekeleza mradi wa maji Vijijini katika Mikoa ya Mwanza, Mara na Tabora. Aidha, Serikali imeendelea na juhudi zake za kujenga mabwawa ya maji katika maeneo kame nchini. Mabwawa yanayoendelea kujengwa ni Kawa (Nkasi), Sasajila (Chamwino), Matwiga (Chunya), Nyambori (Rorya), Wegero (Musoma), Habiya (Bariadi), Iguluba (Iringa), Mwanjoro (Meatu) na Seke Ididi (Kishapu). (*Makof*)

Mheshimwa Spika, Serikali pia, imeimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde yote tisa (9) ya maji nchini na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vyia maji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Serikali imejenga visima 946 katika Halmashauri 84.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mijini, Serikali imejenga na kukarabati Mifumo ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa 19. Kutokana na jitihada hizo, kiwango cha upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Miji hiyo kimeongezeka kutoka asilimia 84 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 86 mwaka 2011. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kuboresha upatikanaji wa maji Mijini kwa kuimarisha utendaji wa Mamlaka za Maji za Miji nchini. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, Serikali itakamilisha upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Chini na kuanza ujenzi wa bomba jipya la maji kutoka Ruvu Chini hadi kwenye matenki ya maji yaliyopo maeneo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, itakamilisha Usanifu wa Mradi wa Kuchimba Visima Virefu katika maeneo ya Kimbiji na Mpera na kuanza ujenzi wa Visima hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi na usalama, Majeshi yetu ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yanafanya kazi nzuri kuhakikisha kwamba hali ya usalama wa nchi na mipaka yetu ni shwari. Aidha, Majeshi yetu yameshiriki kikamilifu katika shughuli za kiraia kusaidia wananchi wakati wa majanga hususan mafuriko, ajali na milipuko ya magonjwa. Pamoja na kazi hizo, katika mwaka wa 2011/2012, Jeshi la Kujenga Taifa limekamilisha ukarabati wa Makambi 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa yenye uwezo wa kuchukua vijana 20,000 kwa wakati mmoja. Kwa mwaka 2012/2013, jumla ya vijana 5,000 wataanza tena kujeunga na JKT kwa Mujibu wa Sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kuitikia Wito wa kutekeleza Azma ya Kilimo Kwanza, mwaka 2011/2012,

Jeshi la Kujenga Taifa limezalisha tani 731.5 za mbegu bora zenye thamani ya Shilingi Milioni 544.4. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kuyawezesha Majeshi yetu kwa vifaa na zana za kivita na upatikanaji wa mahitaji muhimu. Serikali pia itaendelea kukarabati Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya kuchukua vijana wengi zaidi na pia kujenga maghala salama ya kuhifadhi silaha, mabomu na milipuko.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa ya kudhibiti matukio ya uhalifu hapa nchini. Mafanikio hayo yamepatikana kutokana na ushirikiano mzuri kati ya Polisi na wananchi kupitia Mkakati wa Ulinzi Shirikishi. Moja ya Mbinu zinazotumika na Jeshi hilo ni kuwashirikisha Wadau, hasa Viongozi wa Kijamii kama vile Wazee wa Kimila, Madhehebu ya Dini, Vyama vyta Hiari katika kuhamasisha wananchi kuzuia na kudhibiti uhalifu nchini.

Mheshimiwa Spika, mbinu nyingine ni kudhibiti tatizo la kuzagaa kwa silaha ndogo nchini kwa Kusajili na kuhamasisha wananchi kujitokeza kuwekewa Alama Maalum kwenye Silaha wanazomiliki. Hadi kufikia mwezi Februari 2012, jumla ya Silaha Ndogo 1,250 zilisajiliwa. Natumia fursa hii kuvipongeza Vyombo vyetu vyta Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri wanayofanya kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, tunayo changamoto ya ajali nyingi za barabarani. Ajali hizo zimeendelea kupoteza maisha ya watu wengi na kusababisha ulemavu wa kudumu kwa wengine. Jeshi

la Polisi kwa kushirikiana na Wadau wengine lijpange kukabiliana na ajali hizo kwa umakini ili kuokoa maisha ya Watanzania yanayopotea kutokana na ajali ambazo zinazuilika. Hii ni pamoja na kuendelea kutoa elimu ya Usalama Barabarani, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara, kuwachukulia hatua za Kisheria Madereva wazembe na kuweka Mfumo madhubuti wa kudhibiti mwendo kasi wa magari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda; Serikali inatekeleza Sera ya Diplomasia ya Uchumi inayoweka umuhimu katika ushirikiano wenye maslahi ya kiuchumi kwa nchi yetu na nchi nyingine pamoja na Mashirika ya Kimataifa. Tayari tumeanza kushuhudia mafanikio ya Sera hii kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Balozi zetu kwa kudumisha mahusiano mema na kuitangaza Tanzania katika medani za Kimataifa. Jitihada hizo zimewezesha kuvutia Wawekezaji wengi, kuongeza idadi ya Watalii, fursa za kibiashara na ajira.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi Wanachama zinatekeleza makuballiano ya kuanzisha Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja Mipakani (*One Stop Boarder Posts*). Hadi sasa ujenzi wa Vituo vinne vya Mpakani vya Horohoro, Holili, Sirari na Mtukula uko katika hatua za kukamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, mwenendo wa biashara baina ya Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki umezidi kuimarika ambapo

mauzo nje yameongezeka kwa asilimia 12.8 kutoka Shilingi bilioni 512.76 mwaka 2010 hadi Shilingi bilioni 578.39 mwaka 2011. Serikali inaendelea na maandalizi ya Sera ya Mtangamano ambayo itakuwa mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Kitaifa za Mtangamano wa Kikanda na Mkakati wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tawala Za Mikoa na Mamlaka Za Serikali Za Mitaa, mwaka 2010/2011; Serikali ilitangaza nia ya kuanzisha maeneo Mapya ya Utawala ya Mikoa minne ya Simiyu, Katavi, Njombe na Geita pamoja na Wilaya Mpya 19 na Tarafa 34 kwa lengo la kusogeza na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Tayari Serikali imeyaanzisha rasmi maeneo hayo na Uteuzi wa Viongozi wa kusimamia Mikoa na Wilaya hizo umefanywa.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Viongozi wa Mikoa na Wilaya kutekeleza majukumu yao ipasavyo, Serikali imetoa Mafunzo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya zote nchini mwezi Mei, 2012. Aidha, Serikali imetekeleza ahadi yake ya kutoa mafunzo kwa Madiwani 4,451 nchini. Ni imani yangu kwamba baada ya mafunzo hayo, utendaji kazi wa Viongozi hao utakuwa ni wa ufanisi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusogeza huduma kwa wananchi kwa kuzipandisha hadhi Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mamlaka za Miji Midogo ya Geita, Bariadi na Tarime zimepandishwa hadhi na kuwa Halmashauri za Miji. Vilevile, Tangazo la kuanzishwa kwa Halmashauri za Manispaa za Lindi na

Ilemela limetolewa kwenye Gazeti la Serikali Na.182 na 256, Tangazo la Kupandishwa Hadhi kwa Halmashauri ya Manispaa ya Arusha kuwa Halmashauri ya Jiji limetolewa katika Gazeti la Serikali Na. 341. Serikali inaendelea na taratibu za kuanzisha Halmashauri za Wilaya 25 Mpya zikiwemo 19 kwenye Wilaya Mpya zilizoanzishwa na sita kutokana na kugawa baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa wakati nahitimisha mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Ofisi yangu mwaka jana, niliahidi kuwa Serikali itaangalia upya viwango vya Posho za Waheshimiwa Madiwani kwa lengo la kuviongeza. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba zoezi hilo limekamilika na kuanzia mwaka 2012/2013 Waheshimiwa Madiwani watalipwa Viwango Vipyta vya Posho vilivyoboreshw. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie masuala Mtambuka. Kuhusu jinsia, Ibara ya 176 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, inahimiza kutambua uwezo na nguvu kubwa ya Wanawake katika kusukuma kasi ya maendeleo na kuleta mageuzi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imeandaa Mkakati na Mwongozo wa Kitaifa wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Nchini. Aidha, imeunda na kuzindua Kamati ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kutoa fursa zaidi za kuwawezesha wanawake katika nyanja mbalimbali pamoja na kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Haki za Wanawake na Watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vita Dhidi ya Rushwa. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea na Mapambano Dhidi ya Vitendo vya Rushwa Nchini. Jumla ya tuhuma zilizopokelewa hadi Mei 2012 ni 4,498. Kati ya hizo, tuhuma 884 uchunguzi wake umekamilika na majalada yamefunguliwa. Aidha, kesi 612 ziliendeshwa Mahakamani. Kati ya hizo, kesi 478 zinaendelea na 134 zilitolewa uamuzi ambapo kesi 46 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuadhibiwa, kesi 32 ziliondolewa Mahakamani kutokana na sababu mbalimbali na kesi 56 watuhumiwa wake waliachiwa huru.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mafunzo kuhusu Vita Dhidi ya Rushwa yametolewa kwa wanajamii 328,947 na Watumishi 439 wa Serikali. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kuchunguza tuhuma 2,729 zilizopo na tuhuma mpya zitakazopokelewa pamoja na kuendelea na uchunguzi maalum wa tuhuma zilizobainishwa kwenye Taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ubadhirifu katika Taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazingira. Serikali imeendelea kutekeleza Sera, Mikakati, Sheria, Kanuni na Miongozo ya Kuhifadhi Mazingira. Miongoni mwa kazi zilizotekelawa ni pamoja na kuandaa Kanuni 14 za Usimamizi wa Mazingira ikiwemo Udhibiti wa Taka, Matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa na tathmini na ukaguzi wa athari za mazingira. Pamoja na miongozo hiyo, Miradi 130 imefanyiwa tathmini na kupatiwa Hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Kampeni ya

Upandaji Miti imeendeshwa na mafunzo kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi yametolewa. Serikali itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza Mikakati ya Kuhifadhi Mazingira kwa kushirikiana na Wadau wengine. Serikali pia itaendelea kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi, kutoa Elimu ya Hifadhi ya Mazingira kwa Umma na kuhamasisha utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti Nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu maafa, katika mwaka 2011/2012, Serikali imeshughulikia matukio ya maafa katika maeneo mbalimbali nchini. Maafa hayo yalisababishwa na mafuriko, magonjwa ya mlipuko, upopo mkali na ukame uliosababisha baadhi ya maeneo kupata upungufu wa chakula. Ukame ulizikumba Wilaya 55 na kuathiri watu 2,186,990 ambao walihitaji msaada wa chakula. Hadi mwezi Mei 2012, Serikali imetoa tani 69,688 zenyе thamani ya Shilingi bilioni 24.4 kwa waathirika ikiwa ni chakula cha msaada. Vilevile, imetoa Shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya kusafirishia chakula hicho hadi kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliendelea kushughulikia Waathirika wa Milipuko ya Mabomu iliyotokea tarehe 16 Februari 2011, katika Kambi ya Jeshi ya Gongo la Mboto, Dar-es-Salaam. Serikali inakamilisha ujenzi wa nyumba 36 za Waathirika wa mabomu zilizobomoka kabisa ambazo zinajengwa na SUMA JKT katika eneo la Msongola, Manispaa ya Ilala. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mafuriko yaliyotokea Jiji ni Dar es Salaam mwezi Desemba 2011, yalikuwa na athari kubwa. Mafuriko hayo, yalisababisha watu 41 kupoteza maisha, mali nyingi za wananchi kupotea na miundombinu ya barabara, madaraja, umeme na maji kuharibika. Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali ilichukua hatua za kuwasaidia waathirika wa mafuriko kwa kuwapatia misaada ya kibinadamu kama vile, makazi ya muda, chakula, mavazi, malazi na huduma za matibabu. Serikali pia imewapatia waathirika waliokuwa wamejenga nyumba zao mabondeni viwanja katika eneo la Ekari 360 liliopo Mabwepande, Wilayani Kinondoni ili waweze kujenga makazi mapya. Hadi mwezi Mei 2012, Kaya 1,010 zilizoainishwa kuwa katika maeneo hatarishi zaidi zimetengewa viwanja. Vilevile, miundombinu muhimu katika eneo hilo ikiwemo maji, barabara na umeme pamoja na huduma za afya, elimu na Kituo cha Polisi imejengwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo la wananchi kujenga katika maeneo hatarishi, Serikali imeziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ziandae Mipango Endelevu ya kuwaondoa watu wanaoishi mabondeni na kuwashamshia katika maeneo salama. Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam tayari zimeandaa Mpango ambao utaanza kutekelezwa katika Bajeti ya mwaka 2012/2013. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, wakati nahitimisha Hotuba ya Makadirio ya Ofisi yangu, niliahidi kuwa Serikali itatoa kifuta machozi kwa wafugaji ambao mifugo yao ilikufa kutokana na ukame

mkali uliotokea mwaka 2008/2009. Athari za Ukame huo, ni pamoja na vifo vingi vya mifugo, wakiwemo ng'ombe, mbuzi na kondoo katika Wilaya za Monduli, Longido na Ngorongoro. Kutokana na hali hiyo, mfumo wa maisha wa wafugaji wengi ulivurugika kwa kuwa uchumi wao unategemea zaidi ufugaji. Baada ya tathmini kufanyika, Serikali iliamua kutoa mifugo ya kianzio (*seed stock*) ili kuziwezesha Kaya zilizopoteza mifugo yote kuendeleza ufugaji. Utekelezaji wa zoezi hilo umeanza na utaendelea katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha. Napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara wa kuwawezesha wafugaji hao na kushiriki yeye binafsi katika uzinduzi wa Mpango huo uliofanyika tarehe 19 Februari 2012, Wilayani Longido.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali itajenga uwezo zaidi wa nchi yetu wa Kuzuia, Kujandaa na Kukabiliana na Maafa na kurejesha hali ya kawaida kwa waathirika. Aidha, Serikali itakamilisha maandalizi ya Sheria Mpya ya Menejimenti ya Maafa, mapitio ya Sera ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004 na Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa UKIMWI. Tanzania ni moja kati ya nchi 32 duniani ambazo zimethibitishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa kuweka jitihada kubwa za kupunguza kiwango cha maambukizi mapya ya UKIMWI kwa Asilimia 25. Mafanikio hayo yanatia moyo kwamba mkazo unaotiliwa na Serikali na Wadau wengine umeanza

kuzaa matunda. Hata hivyo, jitihada zaidi zitahitajika kutoka kila Sekta, Asasi Zisizo za Serikali, wananchi na watu binafsi katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imeweka jitihada kubwa za kuendelea kupunguza maambukizi mapya, vifo vitokanavyo na UKIMWI na unyanyapaa. Hadi Desemba 2011, jumla ya watu 1,125,211 wamepata huduma na Ushauri Nasaha na Upimaji wa VVU kwa hiari. Aidha, watu wanaoishi na VVU wapatao 412,108 wanapata Dawa za ARV's chini ya Mpango wa Taifa wa Matunzo na Matibabu. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaimarisha uratibu wa shughuli za UKIMWI hasa katika Asasi za Kiraia na kuongeza juhudi za uraghibishaji na uhamasishaji kwa umma. Serikali pia itaandaa Mkakati wa Tatoo wa Kitaifa wa Mapambano dhidi ya UKIMWI na kufanya mapitio ya Mkakati wa Kinga Nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na dawa za kulevya. Serikali imejizatiti kukabiliana na tatizo la usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Februari 2012, kilo 349 za dawa za kulevya za Viwandani, kilo 48,227 za bangi na kilo 10,680 za mirungi zilikamatwa. Hali hii si nzuri na ni dalili tosha kuwa nguvu zaidi zinahitajika ili kukabiliana na janga hili kubwa kwa jamii yetu. Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya madhara ya dawa za kulevya, kufanya misako na operesheni katika maeneo mbalimbali na kuendelea kuteketeza mashamba ya bangi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaimarisha na kuboresha huduma za tiba na utengemao kwa waathirika wa dawa za kulevy. Napenda kuwatahadharisha wale wote wanaojihusisha na biashara hiyo haramu kwamba Tanzania siyo Kituo cha kupitisha au sehemu ya kufanya biashara ya dawa za kulevy. Vyombo vya Usalama vimeimarishwa ili kudhibiti biashara hiyo. Nachukua fursa hii kukishukuru na kukipongeza Kikosi Maalum cha Serikali cha Kupambana na Dawa za Kulevy ambacho kimefanya kazi kubwa ya kukamata dawa nyingi zilizoingizwa nchini. Nawasihi waendelee kufanya kazi hiyo kwa moyo zaidi ili kuiepusha nchi yetu na athari kubwa zitokanazo na matumizi ya dawa za kulevy.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma. Katika mwaka 2011/2012, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma imefanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Kuendeleza Mji Mkuu Dodoma ili kuzingatia kasi ya ukuaji wa Mji huo. Aidha, mapitio ya Ikama na Muundo wa Utumishi umefanyika kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kiutendaji wa Mamlaka. Kazi nyingine zilizofanyika ni ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 27 katika maeneo ya Ipagala, *Area E, Chang'ombe Extension*, Mwangaza, Chidachi na inaendelea na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 15 kwa kiwango cha Lami katika maeneo ya Kisasa na Chang'ombe. Aidha, Mamlaka imepata mkopo kutoka Benki ya CRDB wa jumla ya Shilingi bilioni 16 kwa ajili ya uwekaji wa miundombinu ya maji, umeme na barabara zenye jumla ya urefu wa kilomita 20.6 kwa kiwango cha lami katika eneo la uwekezaji la Njedengwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu itafanya kazi ya kusanifu Mpango ya Makazi ya Uendelezaji wa Miji (*Satellite Towns*) katika maeneo ya Ihumwa na Hombolo. Mamlaka pia itaendelea kupima viwanja 7,850 katika maeneo ya lyumbu, Nzuguni na Miganga na kukamilisha upimaji wa viwanja vya zamani 1,938 katika maeneo ya Ipagala, Nkuhungu na Kisasa. Hali kadhalika, Mamlaka itajenga barabara zenyet urefu wa Kilomita 11.3 kwa kiwango cha Lami katika maeneo ya Area 'A' na Kikuyu na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na barabara kwa kiwango cha lami katika eneo la Uwekezaji la Njedengwa. Serikali pia itafanya kazi mapendekezo ya Mshauri Mwelekezi aliyefanya mapitio ya Muundo wa *CDA* hasa kutatua mwingiliano wa utendaji uliopo kati ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi. Mwezi Novemba 2011, nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania imojiunga na Mpango wa Kimataifa wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (*Open Government Partnership - OGP*). Mpango huo unahimiza uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa Uwazi, Utawala Bora, Uadilifu, Mapambano Dhidi ya Rushwa na Ushirikishwaji mpana wa wananchi katika mipango ya maendeleo na usimamizi bora wa rasilimali za Taifa. Chini ya makubaliano ya Mpango huo, kila nchi inaandaa Mpango Kazi wa Utekelezaji ambao ni shirikishi na unaotekelzeza kulingana na mazingira yake. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Serikali imeandaa

Mpango Kazi wa utekelezaji ambapo Sekta za Afya, Elimu na Maji zimepewa kipaumbele. Mpango Kazi huo uliwasilishwa katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Viongozi wanaohusika na Mpango huo uliofanyika tarehe 17–18 Aprili 2012, nchini Brazil. Utekelezaji wa Mpango huo utaanza katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Matumizi ya Serikali. Katika Mkutano wa Saba wa Bunge mwezi Aprili 2012, niliahidi kuwa Serikali itayafanyia kazi maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakijadili Taarifa mbalimbali za Kamati za Kudumu za Bunge. Taarifa hizo ni pamoja na zile za Kamati zinazoshughulikia Hesabu za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ziliainisha Hoja mbalimbali za Ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2009/2010. Aidha, nilieleza kuwa Serikali itawawayibisha wote walotajwa kuhusika na ubadhirifu wa mali ya umma ulioainishwa katika Taarifa hizo pale itakapothibitika kuwa Watumishi hao wametenda makosa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Taarifa na Hoja zote za Ukaguzi za mwaka 2009/2010, zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuzitafutia majibu fasaha katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Aprili 2012. Baada ya zoezi hilo kukamilika, Taarifa hizo zitawasilishwa ngazi ya Mkoa ambapo watapitia majibu ya Hoja hizo na kuziwasilisha katika Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*). Taarifa za Mikoa na Halmashauri zote zitawasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu,

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kabla ya mwezi Novemba 2012 ili hatimaye kuandaa majibu ya pamoja na kuyawasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara, Wakala, Mashirika ya Umma na Idara za Serikali Zinazojitegemea zimeagizwa kupitia Hoja zote zilizotolewa na Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuzifanyia kazi. Wakala wa Serikali na Mashirika ya Umma yametakiwa kupitisha majibu ya Hoja kwenye Bodi za Wakurugenzi kabla ya kuwasilishwa Wizarani. Utaratibu huo utakuwa endelevu na utafanyika kila mwaka. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa usimamizi wa Fedha za Umma unaimarishwa katika ngazi zote. Majibu ya Hoja zote yatawasilishwa Bungeni ili kuongeza uwazi na uwajibikaji wa Fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hiyo, Watumishi wa Umma watakaotuhumiwa kufanya ubadhirifu wa fedha za Umma watachunguzwa na tuhuma zikibainika ni za kweli watavuliwa madaraka waliyo nayo na kufikishwa katika Vyombo vyा Sheria. Napenda kusitiza kwamba, Serikali haitawahamisha Watumishi wa alna hiyo, bali hatua za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa wakiwa kwenye vituo vyao vyा kazi. Natoa wito kwa Watendaji Wakuu wa Serikali, Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma na Madiwani kuhakikisha wanashiriki ipasavyo katika kusimamia fedha za umma kwa mujibu wa Sheria, Taratibu, Miongozo na Kanuni zilizopo. Nawaagiza Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kubandika kwenye mbao za matangazo za Makao Makuu ya

Halmashauri na katika vituo vyote vya utoaji huduma kiasi cha fedha kinachopokelewa kila mwezi na matumizi yake. Hii itawezesha wananchi kufuatilia matumizi ya fedha zilizopelekwa kwa ajili ya utoaji huduma kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kupunguza matumizi yasiyo na tija, hususan ununuzi wa magari makubwa na ya kifahari ambayo gharama za ununuzi na uendeshaji ni kubwa sana. Kuanzia mwaka 2012/2013, hatua zaidi zitachukuliwa kwa kuweka ukomo wa ukubwa wa injini wa magari ambayo yanaweza kununuliwa na Serikali Kuu na Taasisi zake pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Chini ya utaratibu huo, magari yatakayonunuliwa yatakuwa ni yale yasiyozidi ukubwa wa injini wa CC 3,000 kwa Viongozi na Watendaji Wakuu na yasiyozidi CC 2,000 kwa Watumishi wengine ambao wana stahili ya kutumia magari ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ili kupunguza matumizi ya magari kwa Viongozi na Watendaji Wakuu kwa safari za Mikoani, Serikali itaanzisha vituo vya Kanda vya magari ya Serikali au kila Ofisi itatenga magari machache yatakayotumika Mikoani kwa shughuli za kikazi. Mwongozo wa utekelezaji utatolewa. Inategemewa kuwa utaratibu huu utapunguza matumizi ya fedha za Serikali kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nimeelezea kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeliza kwa kipindi kilichopita. Aidha, nimetoa Mwelekeo wa Kazi

zitakazofanyika mwaka 2012/2013. Kwa kuhitimisha, napenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Wote tunatambua kuwa tumeanza kutekeleza Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kwa Tume ya Kuratibu maoni kuanza kazi. Tuendelee kuwaelimisha wananchi kuhusu Mambo ya Msingi wakati wa kuchangia maoni na kwamba kila mmoja anao wajibu na uhuru wa kutoa maoni yake kwenye Tume bila shinikizo lolote.

(b) Tumepitisha Bajeti ya Serikali ambayo changamoto yake kubwa ni rasilimali fedha kidogo tuliyonayo kukidhi mahitaji makubwa ya kutoa huduma bora kwa wananchi tunaowaongoza. Kutokana na hali hiyo, ni muhimu kujipanga vizuri kudhibiti na kusimamia matumizi ya fedha za umma kwa ufanisi na tija zaidi. Serikali itaimarisha Mifumo yake ya usimamizi na ufuatiliaji na kuhakikisha kwamba fedha za umma zinatumika kulingana na Sheria na Kanuni za Matumizi ya Fedha za Serikali.

(c) Katika muda usiozidi miezi miwili ijayo, tarehe 26 Agosti 2012, itakuwa ni Siku ya Sensa ya Watu na Makazi nchini. Napenda kusisitiza kwamba uandikishaji hautakuwa wa siku moja tu, bali siku hiyo ndiyo itakayokuwa msingi wa kuhesabu watu waliolala katika Kaya husika. Kazi hiyo itaendelea kwa siku saba hadi tarehe 2 Septemba 2012. Natoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano kwa Makarani wa Sensa na kujitokeza kuhesabiwa na kuhakikisha kwamba kila mtu anahesabiwa mara moja tu. Aidha, Viongozi katika

Ngazi zote wana wajibu mkubwa wa kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki kwenye Sensa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza Hotuba yangu, nimwombe Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa atoe maelezo ya Mapitio ya Kazi zilizofanyika katika mwaka 2011/2012 na Mwelekeo wa Kazi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2012/2013. Ni matumaini yangu kwamba maelezo hayo yatawezesha Waheshimiwa Wabunge na wananchi kufahamu kwa upana shughuli zinazoteklezwa na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nguvu na kuniwezesha leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyoionesha kwangu kwa kunitfea katika nafasi hii ya kuwa Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Waziri Mkuu ili nishughulikie Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naahidi kufanya kazi kwa uwezo wangu kadri Mungu atakavyonijalia.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba nzuri ya Mwelekeo na Malengo ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, kwa hotuba ya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa

mwaka 2011/2012 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013. Pia nampongeza Mheshimiwa Dokta William Mgimwa, Waziri wa Fedha kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo na nimpongeze vile vile kwa hotuba aliyotoa kuhusu mapendekezo ya Serikali ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2012/2013. Hotuba zote zilizotangulia zimeonesha mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu wa Spika kwa uongozi imara na madhubuti katika Bunge hili. Aidha, namshukuru kwa namna ya pekee Naibu Waziri Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mbunge wa Siha, anayeshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Majaliwa Kasimu Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, anayeshughulikia Elimu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Katibu Mkuu Bwana Hussein A. Kattanga, Naibu Makatibu Wakuu Bwana Jumanne A. Sagini, Bwana Alphayo J. Kidata, Wakurugenzi na Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao kwa kipindi kifupi nilichofanya nao kazi wamenipa ushirikiano wa kutosha. Hivyo, ni imani yangu tutafanikisha kuyatekeleza majukumu ya ofisi kwa manufaa ya Watanzania wote. Niwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wote wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Mabaraza ya Madiwani, wote kwa pamoja nawaahidi ushirikiano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza wafuatao kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri kama ifuatavyo: Mheshimiwa Dokta Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Dokta Fenella Ephraim Mukangara, Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki, Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza na Mheshimiwa Dokta Abdallah Omari Kigoda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwapongeza wafuatao kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri katika Wizara mbalimbali, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mheshimiwa Dokta Seif Suleiman Rashid, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mheshimiwa Dokta Charles John Tizeba, Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki, Mheshimiwa Stephen Julius Maselle, na Mheshimiwa Mhandisi Dokta Binilith Satano Mahenge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Musa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Kadhalika, nampongeza Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge na Waheshimiwa Dokta Dalali Kafumu, Joshua Nasari kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge katika Majimbo yao na Mheshimiwa Cesilia Pareso kuwa Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kutoa pole kwa familia za Wabunge wenzetu waliopoteza maisha baada Bunge la Bajeti la mwaka 2011/2012. Wabunge hao ni Marehemu Jeremiah Sumari aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki na Marehemu Regia Mtema aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Tunaomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na awajalie ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu moyo wa subira.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uongozi wa Mwenyekiti Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi kwa kuichambua bajeti ya ofisi yetu na kutupa maoni na ushauri ambao unaendelea kutujenga katika utendaji wetu wa kazi, nawashukuru sana. Tutayachukua maoni na ushauri walioutoa kwa uzito unaostahili na kuufanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wananchi wa Mtwara Vijiji kwa mshikamano na ushirikiano wanaonipatia katika majukumu yangu ya Ubunge na Uwaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naahidi kuendelea kuwatumikia kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia ili kwa pamoja tufanikishe shughuli za kujiletea maendeleo katika Jimbo letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Mwelekeo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Utawala Bora; Serikali za

Mitaa ndio mhimili mkubwa wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika lengo zima la kuhakikisha yanakuwepo maendeleo endelevu katika nchi yetu. Upelekaji wa madaraka kwa wananchi unapitia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na ndiyo maana Serikali za Mitaa na ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa maendeleo vimetambuliwa katika Katiba na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ufafanuzi wa dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi umeelezwa kwa kina zaidi katika Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1998 (*The Policy Paper on Local Government Reform of 1998*).

Mheshimiwa Spika, katika Sera hii, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapewa uhuru (*autonomy*) wa kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu utoaji wa huduma kwa wananchi walio katika mamlaka hizo kwa kuwashirikisha wananchi katika kujiletea maendeleo na ustawi wao kwa ujumla. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuutumia uhuru huo kwa kuzingatia Katiba na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na endapo zitakwenda kinyume chake, Serikali Kuu inao wajibu wa Kikatiba na Kisheria kuingilia kati (*intervene*) na kuchukua hatua dhidi ya mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa umetekeliza kwa awamu mbili. Awamu ya Kwanza ilianza kutekelezwa mwaka 1998 hadi 2008 na Awamu ya Pili imeanza kutekelezwa mwaka 2009 na utakamilika mwaka 2014. Katika awamu ya pili Mikoa yote imepewa Wataalam Washauri watakaosaidia kujenga uwezo wa ngazi hii ili

kuweza kuzishauri na kuzisimamia kwa karibu Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wataalam hawa watafanya kazi kwa karibu na Makatibu Tawala Wasaidizi katika Sekretarieti za Mikoa katika kuimarisha masuala ya fedha na rasilimali watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ni matarajio yetu kwamba baada ya muda, wataalam wote walio katika Sekretarieti za Mikoa watakuwa wamejengewa uwezo wa kusimamia shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Halmashauri 62 zimepatiwa magari ili kuwedesha vitengo vya Ukaguzi wa Ndani kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Nyenzo hii ya usafiri itawawezesha kukagua shughuli mbalimbali zinazotekelawa katika ngazi za chini za Halmashauri na hivyo kubaini thamani ya fedha katika miradi inayotekelawa. Aidha, Mikoa yote imepatiwa magari ambayo yatatumiwa na Wataalam waliopelekwa katika ngazi hiyo pamoja na wale wa sehemu ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa ili kuwawezesha kuzifuatilia kwa karibu Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizo katika Mikoa yao.

Mheshimiwa Spika, ili Madiwani waweze kutekeleza majukumu yao vema umeandaliwa utaratibu wa kuwakopesha vyombo vya usafiri kupitia Benki. Tayari makubaliano yameshafikiwa kati ya Serikali na *NMB* ili kuwawezesha Madiwani kupata vyombo vya usafiri. Baadhi ya Madiwani wameanza kufaidika na utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, Waweka Hazina katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wamejengewa uwezo

kwa kupatiwa mafunzo ya viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (*International Public Sector Accounting Standards (IPSAS)*). Hivyo, ni mategemeo yetu kwamba mfumo huu utawasaidia katika kutekeleza majukumu waliyokabidhiwa ya kusimamia vizuri fedha za Serikali na kutoa taarifa zilizo sahihi kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza shughuli zinazohusiana na uboreshaji wa uendeshaji wa Mabaraza ya Kata, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilimteua Mtaalam Mshauri ambaye alipewa kazi ya kuitia Sheria na nyaraka mbalimbali zinazohusu uendeshaji wa Mabaraza ya Kata na kupendekeza namna bora ya kuboresha utendaji kazi wa Mabaraza hayo kwa kuzingatia mabadiliko yaliyotokea hadi sasa. Baadhi ya matatizo yaliyoibuliwa na Mtaalam Mshauri katika taarifa yake ni pamoja na malipo na posho kwa Wajumbe wa Baraza la Kata; uwezo na sifa za Wajumbe wa Mabaraza ya Kata; mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Kata; ukosefu wa vitendea kazi; kutekeleza majukumu ya Kimahakama zaidi kuliko ya usuluhishi; Mabaraza hayo kuwepo chini ya Mamlaka tatu tofauti yaani chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ambalo lipo chini ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza katika taarifa hiyo zilijadiliwa na wadau mbalimbali na hatimaye maoni na mapendekezo ambayo yaliwasilishwa Serikalini. Maoni na mapendekezo hayo

yanafanyiwa kazi na Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, ili kuimarisha utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali imekuwa ikichukua hatua kwa watumishi wanaotuhumiwa kwa makosa mbalimbali. Kuanzia mwaka 2009/2010 hadi Machi, 2011/12, Wakurugenzi wa Halmashauri wapatao 24 walichukuliwa hatua za kinidhamu, kati yao nane walivuliwa madaraka, 11 walipewa onyo, watatu wamepumzishwa kazi na wawili wamesimamishwa kazi na kesi ziko Mahakmani. Aidha, Wakuu wa Idara 74 wa Halmashauri mbalimbali wamechukuliwa hatua za kinidhamu kutokana na tuhuma zinazowakabili.

Mheshimiwa Spika, kujenga uwezo wa Sekretarieti za Mikoa, Ofisi yangu imetoa mafunzo kwa viongozi wa Sekretarieti za Mikoa ili kuwakumbusha majukumu yao kwa lengo la kuboresha utendaji wa kazi. Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na Maandalizi ya Mipango na Bajeti kwa Makatibu Tawala Wasaidizi 75 kutoka Mikoa 21. Mafunzo hayo yalilenga kuwapa uelewa zaidi katika kuandaa Mipango, Bajeti na Taarifa za Mikoa yao. Makatibu Tawala wa Mikoa 21 wamepata mafunzo hayo katika Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo ambapo dhumuni kubwa lilikuwa ni kuwajengea uwezo wa kiutendaji ili kuwawezesha kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kujenga uwezo wa Sekretarieti za Mikoa ni pamoja na kuimarisha utendaji wa Maafisa

Tarafa. Mkakati uliopo ni kuhakikisha kuwa Maafisa Tarafa wanapata vitendea kazi hususan vyombo vyaa usafiri na ofisi. Aidha, nafasi wazi za Maafisa Tarafa 145 tayari zimepata kibali cha ajira na mchakato wa kuwaajiri unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu imeendelea kuzifanyia mapitio Sheria mbalimbali ili ziweze kuendana na mabadiliko yanayojitokeza katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sheria ya Tawala za Mikoa namba 19 ya mwaka 1997. Mapitio yatakapokamiliika yatawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Lengo kubwa ni kuimarisha utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, makisio ya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2010/2011, makadirio yalikuwa shilingi bilioni 173.1 na makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 158.3 sawa na asilimia 92. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 makadirio yalikuwa shilingi bilioni 350.5. Hadi kufikia Machi 2012 zimekusanya wa shilingi bilioni 142.8 sawa na asilimia 40.7.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa katika Halmashauri ni kuiwekea makadirio kidogo katika ukusanyaji mapato. Ili kuondoa tatizo hili Ofisi yangu imeanza kuandaa mikakati ya kusaidia kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Vikao vyaa kitaalam vyaa uchambuzi wa mipango na bajeti za kila chanzo na ushahidi wa takwimu za walipa kodi na vitu vinavyolipiwa kodi (*Tax Payers na Tax Objects*)

vimefanyika. Taarifa hizo muhimu zitatumika pamoja na taarifa za utafiti unaotarajiwa kufanywa na Wataalam Washauri katika kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, taarifa ya ukaguzi wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2011 iliwasilishwa Bungeni tarehe 12 Aprili 2012. Kwa mara ya tatu mfululizo, hesabu hizi ziliandaliwa kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya uhasibu kwa Sekta ya Umma (*IPSAS*). Kwa ujumla, matokeo ya ukaguzi wa hesabu hizo yanaonesha kuwa bado kuna kazi ya ziada ya kufanya ili kuwa na utendaji ulioimarika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) inaonesha kuwa kiwango cha utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kinaendelea kuimarika. Hii inatokana na ukweli kwamba, kumekuwa na ongezeko la Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati zinazoridhisha (*safi*) kutoka 66 (48.9%) mwaka 2009/2010 mpaka hati 72 (54%) mwaka 2010/2011. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati zenye shaka zimepungua kutoka 64 (48.1%) mwaka 2009/2010 mpaka hati 56 (42%) Mwaka 2010/2011. Vile vile, kumekuwa na ongezeko la Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati zisizoridhisha (*chafu*) kutoka nne (3%) mwaka 2009/2010 mpaka tano (4%) mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya ukaguzi huo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebainisha sababu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kupata hati zenyе shaka au zisizoridhisha kama ifuatavyo: Kutotolewa kwa mafunzo ya kutosha ya kuandaa taarifa za fedha kwa kutumia viwango vya Kimataifa vya uhasibu kwa Sekta ya Umma (*IPSASs*) na hivyo kuandaliwa kwa taarifa za fedha zisizo sahihi; Kuwepo kwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaokiuka maadili ya kazi zao na kujihusisha na ubadhirifu wa fedha za Halmashauri na hata kula njama na watumishi wa Benki na udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuainisha vyanzo vya mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi. Hii imetusaidia kuanza kuyafanyia kazi ili kuzuia kujirudia kwa hali hii. Eneo tunalolipa kipaumbele ni kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na usimamizi kwenye ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa.

Mheshimiwa Spika, ili kuzipa uwezo Halmashauri kusimamia fedha kwa ufanisi, matumizi ya mfumo wa *Epicor 9.05* katika mfumo wa *Intergrated Financial Management System (IFMS)* utaanza kutumika kwa Halmashauri zote nchini mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, mwezi Mei, 2012 Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imefanya Mkutano wa kazi uliowashirikisha Makatibu Tawala wa Mikoa yote, Wakurugenzi wa Halmashauri zote, Waweka Hazina wa Halmashauri zote pamoja na wataalam wengine

kutoka ngazi ya Mkoa kwa ajili ya kutafuta suluhisho la kudumu la dosari na mapungufu yanayoendelea kujitokeza katika taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Moja ya maazimio muhimu ya Mkutano huo ni kwamba, kuanzia sasa makosa yanayotokana na uzembe na uwezo mdogo wa kusimamia kazi hautavumiliwa.

Mheshimiwa Spika, kila Katibu Tawala wa Mkoa atawajibika kwa kutochukua hatua zinazolenga kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika Halmashauri chini ya Mkoa anaoongoza. Kadhalika Mkurugenzi wa Halmashauri atapimwa kwa kigezo cha uwajibikaji kutokana na tathmini mbalimbali ikiwemo taarifa ya ukaguzi, kuweka kwenye mbaao za matangazo taarifa za miradi inayotekelawa katika Halmashauri pamoja na fedha zote zilizopokelewa kwa ajili ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kunakuwa na uzingatiaji wa viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa Sekta ya Umma (*IPSASs*) na kunakuwa na usahihi wa taarifa za hesabu zinazoandaliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali itaendelea kutoa mafunzo yanayotakiwa kwa wahasibu katika ngazi zote zinazohusika. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa watumishi wote watakaobainika kuhusika na ubadhirifu, wizi na kuzisababishia hasara Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutowajibika ipasavyo, wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hizo napenda kuzipongeza Halmashauri 11 ambazo

zimeendelea kupata hati zinazoridhisha (hati safi) kwa kipindi cha miaka minne (4) mfululizo; Halmashauri hizo ni za Wilaya za Mufindi, Biharamulo, Missenyi, Siha, Nachingwea, Serengeti, Kyela, Maswa, Singida na Manispaa ya Shinyanga. Vile vile, napenda kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Mtwara kutokana na Halmashauri zote za Mkoa huo kupata hati zinazoridhisha.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Barabara za Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2011/2012 kiasi cha shilingi bilioni 94.02 kutoka katika Mfuko wa Barabara zilitengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Halmashauri. Hadi kufikia mwezi Machi, 2012 jumla ya shilingi bilioni 73.7 zilikuwa zimepokelewa na kupelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara, pamoja na miradi mikubwa kuitia fedha za maendeleo ambazo ni asilimia 10 ya bajeti ya Mfuko wa Barabara zinazotolewa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 kiasi cha shilingi bilioni 128.9 kinategemewa kutoka kwenye Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfumo wa Kupeleka Ruzuku ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (*LGDG*). Mfumo wa Kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa Ruzuku ya Maendeleo ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Mfumo huu ndio unaotumika katika kugawa ruzuku ya

maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia uwazi na usawa. Kupitia Mfumo huu, tathmini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kila mwaka na ruzuku ya maendeleo hupelekwa katika Mamlaka hizo kulingana na jinsi zilivyofuzu vigezo vilivyowekwa. Ruzuku ya kujenga uwezo hutolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote kwa ajili ya kuijimarisha kiujuzi na maarifa kwenye maeneo ambayo Mamlaka hizo zitakuwa zimebaini kuwa na upungufu.

Mheshimiwa Spika, Mfumo huu ulifanyiwa tathmini mwezi Septemba 2011. Mojawapo ya mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini hii ni kufanya mapitio ya vigezo vya tathmini, kiwango cha ruzuku na namna ya kupata ruzuku ya maendeleo na ya kujenga uwezo. Kutokana na mapendekezo haya, utaratibu mbadala unaandaliwa ambao utatumika kupima Mamlaka za Serikali za Mitaa. Utaratibu mbadala unaopendekezwa ni wa kuzitumia Sekretarieti za Mikoa katika upimaji wa awali wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zitakuwa zimeshindwa kufuzu, ufuatiliaji utafanywa na timu ya wataalam ili kubaini chanzo cha mapungufu pamoja na mbinu za kuondokana na mapungufu hayo. Hata hivyo, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huzingatiwa wakati wa kufanya maamuzi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakazopata ruzuku ya maendeleo na kujenga uwezo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2012, jumla ya shilingi bilioni 106.6 zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mfumo huo zikiwa ni ruzuku isiyo

na masharti. Aidha, kwa upande wa Sekta ya Kilimo jumla ya shilingi bilioni 59.8 ziliikuwa zimepelekwa kwa ajili ya ruzuku ya maendeleo ya kilimo na shilingi bilioni 43.3 zilipelekwa kwa ajili ya ruzuku ya maendeleo ya maji vijiji. Vile vile shilingi bilioni 80.9 za Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Afya ambazo ni asilimia 100 zimetolewa na kupelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji Tanzania (*TSCP*), Mradi wa uboreshaji wa miundombinu katika Miji Tanzania ni matokeo ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania, Benki ya Dunia na Serikali ya Denmark. Mradi ulizinduliwa rasmi Oktoba, 2010 na umepangwa kutekelezwa hadi mwaka 2014/2015. Madhumuni ya mradi huu ni kuziwezesha Halmashauri nane (8) zinazohusika na utekelezaji wa mradi huu, kuboresha miundombinu na utoaji wa huduma za jamii katika Miji. Mamlaka hizi ni Jiji la Mwanza, Tanga na Mbeya; Manispaa za Arusha, Dodoma, Kigoma Ujiji, Mtwara Mikindani na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma. Hadi Machi, 2012, sh. 21,520,034,150.00 (Kati ya sh. 49,807,534,150.00 zilizotengwa) ziliikuwa zimetolewa kwenye Halmashauri na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali. Kiasi kilichobakia kitaendelea kutolewa kadri utekelezaji unavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, mbali ya fedha za ujenzi wa miundombinu, kiasi cha sh. 4,068,292,750.00 kimeshapelekwa kwenye Mamlaka zinazotekeleza mradi huu kwa ajili ya kujenga uwezo katika maeneo

mbalimbali katika Mamlaka hizo. Maeneo hayo ni kama vile Idara za Mipango Miji ambapo yamefanyika mafunzo ya *Geographical Information Systems (ARC-GIS)* pamoja na ununuzi wa mfumo huo (*ARC-GIS software*). Vile vile, Wizara ya Ardhi imepewa kandarasi ya kurekebisha picha za *Satelite (Rectification and Digitization of satelite image)* na kazi hiyo inaendelea kutekelezwa katika maeneo ya mradi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuimarisha Halmashauri za Manispaa 11 na Miji saba (7), katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa kuimarisha miundombinu pamoja na uwezo wa kutoa huduma za jamii katika Halmashauri za Manispaa 11 na Miji saba (*Urban Local Government Strengthening Programme*). Manispaa zinazohusika ni Morogoro, Moshi, Iringa, Bukoba, Shinyanga, Singida, Musoma, Sumbawanga, Songea, Lindi na Tabora. Miji inayohusika ni Babati, Njombe, Korogwe, Mpanda, Kibaha, Geita na Bariadi. Mradi utatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2012/2013 hadi 2016/2017. Mradi utagharimu kiasi cha dola za Kimarekani milioni 175 ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Kati ya fedha hizo, dola milioni 160 zitagawiwa katika Halmashauri husika kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya aina mbalimbali kulingana na mipango ya Halmashauri hizo. Fedha zinazobaki yaani dola milioni 15 ni kwa ajili ya uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TEHAMA. Ofisi yangu imeendelea kuhakikisha kuwa taarifa sahihi zinapatikana katika ngazi zote za Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa na kuwezesha utoaji wa huduma kupitia Serikali Mtandao. Miundo ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa imetengenezwa kwa kuzingatia mahitaji ya TEHAMA na hivi sasa vimeanzishwa vitengo vya TEHAMA katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mawasiliano tumefunga vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya *video conferencing* katika kila Sekretarieti ya Mkoa. Ofisi inaendelea kujenga uwezo kwa kutoa msaada wa kiufundi ili Mikoa iweze kutoa huduma ya kiufundi ya TEHAMA katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yaani Dawati la Usaidizi la TEHAMA. Aidha, Ofisi imeanzisha *Computer Laboratory* kwa ajili ya kufundisha watumishi wake katika ngazi zote kuhusu mifumo mbalimbali inayotumika katika utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Spika, mifumo ambayo imeshafanyiwa kazi katika ngazi zote za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni ifuatayo:- Tovuti za Sekretarieti za Mikoa, mfumo wa barua pepe, mfumo wa *Integrated Financial Management System*, *Planrep* na Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (*LGHRS*) ambao ultengenezwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa Ufadhilli wa *Intra-Health International*. Zoezi la uingizaji takwimu za rasilimali watu linaendelea katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 89 na Sekretarieti za Mikoa 13 ambako mfumo umewekwa. Vifaa vya TEHAMA na mafunzo kwa watumiaji wa mfumo huu vitaendelea kufungwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizosalia kupitia Programu ya Kuboresha Mfumo wa Serikali za Mitaa, Awamu ya Pili (*LGRP II*).

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa Shule za Msingi na Sekondari nchini. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia utoaji wa elimu ya Msingi na Sekondari kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ofisi ilizagiza Halmashauri kupitia Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kwamba watoto wenyewe umri stahiki wanaandikishwa na kuhuduria Shule za Msingi bila kukosa kama inavyoelekezwa na Sera ya Elimu na Mafunzo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Halmashauri zilitakiwa zisimamie uwepo wa madarasa ya elimu ya awali kwenye Shule za Msingi ili watoto wengi zaidi wapate fursa ya kuhuduria elimu ya awali kabla ya kuanza darasa la kwanza. Ofisi ilishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za *Capitation* katika Halmashauri zake ikiwa ni pamoja na fedha nyingine zinazopelekwa katika Halmashauri husika. Aidha, Halmashauri zimetakiwa kutumia fedha wanazopata kwa uadilifu ili kuепuka madeni hasa ya chakula na vifaa vya kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, iko changamoto ya maeneo ya shule hasa mijini kuvamiwa au kwa kutumia mikataba isiyo halali, wafanyabiashara kujenga vibanda vya biashara kuzunguka eneo la shule. Matumizi ya maeneo ya shule yamefafanuliwa katika Gazeti la Serikali Na. 298 la mwaka 2002 kuwa ni kinyume cha sheria, kanuni na taratibu kufanya biashara katika maeneo ya shule au kutumia majengo ya shule kwa shughuli za biashara. Kupitia Bunge lako Tukufu

nawaagiza Makatibu Tawala wa Mikoa yote kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Serikali tarehe 15 Januari, 2010 kuhusu kudhibiti biashara katika maeneo ya Shule. Aidha, Wakuu wa Mikoa wanatakiwa kufuatilia suala hili kwa karibu kuhakikisha kuwa biashara hizo zinasitishwa katika maeneo ya shule. Hata hivyo, suala la kuwepo kwa vibanda vyta chakula, Ofisi yangu kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kulifanyia kazi ili kupata utaratibu utakaoonekana unafaa katika kutoa huduma ya chakula katika shule kwa ajili ya walimu na wanafunzi bila kuathiri maadili ya msingi ya shule zetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile, viko vibali vyta biashara vinavyotolewa na Halmashauri ambavyo vinasababisha kujengwa kwa majengo ya biashara za nyumba za kulala wageni na baa karibu na viwanja vyta shule. Napenda kutumia fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuziagiza Halmashauri zote hususan za mijini kusitisha vibali vyote vilivyotolewa vyta kufanya biashara za nyumba za kulala wageni na uendeshaji wa baa katika viwanja vinavyopakana na maeneo yaliyojengwa shule. Aidha, liko suala ambalo linajitokeza la maeneo ya shule za Msingi na Sekondari kutokuwa na hati miliki kwa viwanja ambavyo vimejengwa shule hizo. Hali hii inachangia uvamizi wa ujenzi wa makazi na biashara katika viwanja vyta shule. Halmashauri zote nchini zinatakiwa kupima viwanja vyta shule zilizo katika maeneo yao na kuzipatia hati miliki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ili kuratibu na kusimamia upatikanaji wa maslahi ya walimu wa shule za msingi

na sekondari kwa kuyaboresha, jumla ya walimu 23,167 waliwasilisha madai yao Serikalini na kati ya hao 17,682 ni wa shule za msingi ambao walipelekewa sh. 13,040,096,775.00 na walimu 5,485 ni walimu wa shule za sekondari ambao walipelekewa sh. 6,169,789,992.00. Walimu waliopo katika Sekretarieti za Mikoa walipelekewa sh. 22,789,680.00 na kufanya jumla ya fedha zilizopelekwa kufikia jumla ya sh. 19,232,676,447.00. Madai ya malimbikizo ya mishahara ya kiasi cha sh. 25,643,594,545.43.00 yanalipwa kwenye mishahara ya walimu husika kupitia mfumo wa malipo ya mishahara ya watumishi wa umma. Hadi Aprili 2012 jumla ya shilingi 16,567,655,437.34 zilikuwa zimelipwa. Aidha, jumla ya shilingi 2,642,231,329.78 zilikuwa zimebaki na zitaendelea kulipwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa miaka miwili mfululizo iliendelea kuratibu uendeshaji wa mashindano ya michezo ya Shule za Msingi (UMITASHUMTA) na Shule za Sekondari (UMISSETA). Michezo iliyoshindaniwa ni riadha, mpira wa miguu, mpira wa mikono, mpira wa pete, mpira wa wavu, bao, meza, mpira wa kikapu. Aidha, kulikuwepo mashindano ya taaluma na ubunifu kwa shule za msingi. Mashindano ya *UMITASHUMTA* yanahuisha wanafunzi kutoka Tanzania Bara pekee wakati *UMISSETA* iliwahuisha wanafunzi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Katika mwaka wa fedha 2011/12, ruzuku ya uendeshaji shule (*Capitation grant*) iliyotengwa kwa elimu ya msingi ni shilingi bilioni 50.

Hadi kufikia mwezi Mei, 2012 kiasi cha shilingi bilioni 10.1 kimetolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ukarabati wa majengo ya shule, kuendesha mitihani ya ndani na uendeshaji wa shule za msingi. Aidha, shilingi bilioni 30 ambazo ni sehemu ya *Capitation* zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya kiada kwa ajili ya shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za chenji ya Rada. Serikali ilipokea fedha za fidia ya ununuzi wa Rada kiasi cha Paundi milioni 29.5 kutoka Serikali ya Uingereza sawa na shilingi bilioni 72.3 za Kitanzania ambazo zitatumika kuimarisha elimu ya msingi nchini. Kati ya kiasi hicho, ilikubalika shilingi bilioni 54.2 sawa na asilimia 75 zitumike kununua vitabu vya kiada kwa shule za msingi na shilingi bilioni 18.1 sawa na asilimia 25 itumike kutengeneza madawati kwa shule za msingi. Ununuzi wa vitabu vya kiada utazingatia vitabu ambavyo viliainishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis mwaka 2009 hata kabla ya fedha za fidia ya rada hazijajulikana kuletwa nchini ambapo vitabu viwili viwili vya kiada viliteuliwa kwa kila somo. Kila shule ya msingi nchini itapata vitabu hivyo.

Mheshimiwa Spika, mazungumzo yamefanyika ili kila Mchapishaji atakayepewa zabuni awajibike kufikisha vitabu hivyo kwenye shule. Ili kuimarisha uwazi vitabu vitapokelewa shulenii na Kamati ya Shule mbele ya wanafunzi, wazazi na Serikali ya Kijiji au Mtaa. Mahali kamili kwa wachapishaji yatatolewa baada ya kupata uthibitisho toka Mikoa na Halmashauri zote

kwamba vitabu vimepokelewa kwa ubora na idadi iliyokubalika.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 18.1 zitatumika kutengeneza madawati kwa shule za msingi. Kiasi cha madawati yatakayopatikana hakitatosha lakini kitasaidia kupunguza tatizo kubwa la madawati linalozikabili shule zetu za msingi nchini. Awali ilipendekezwa kuwa madawati hayo yanunuliwe na kusambazwa kwenye Halmashauri zilizokuwa na upungufu mkubwa wa madawati yaani upungufu unaofikia madawati 100,000 au zaidi. Hata hivyo, Serikali imetafakari tena na kuona kwamba kigezo cha upungufu mkubwa pekee si kigezo bora cha kutumia katika kugawa madawati. Kutokana na uamuzi huu, kila Halmashauri itapata mgao wa madawati.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Kazi za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili (MMES II) zilizotekeliza katika mwaka 2011/2012 ni kufanya uchambuzi yakinifu wa shule 264 ambazo zitafanyiwa ukarabati mwaka 2012/2013; kuandaa moduli za mafunzo ya Bodi za Shule na Waratibu Elimu Kata ili kusimamia uendeshaji na uratibu wa elimu ya Sekondari. Mafunzo yataanza katika mwaka wa fedha 2012/2013. Maafisa Elimu wa Mikoa 25, Maafisa Elimu Taaluma wa Mikoa 25, Maafisa Elimu wa Sekondari wa Halmashauri 133, Maafisa Elimu Taaluma 133 wa Halmashauri na Wakuu wa Shule 3,435 wa shule za Serikali na zisizo za Serikali walipata mafunzo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya II (MMES II).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 22.9 kwa ajili ya uendeshaji wa shule za sekondari. Hadi kufikia Machi, 2012 jumla ya shilingi bilioni 7.6 zimetolewa na kupelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya *Capitation* ya shule ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vitabu vya kiada na vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2012/2013 ni kufanya ukarabati wa shule 264 zilizoanishwa; Kutoa mafunzo kwa Bodi za Shule, kuendesha michezo ya UMISSETA; Kushiriki katika kufuatilia utoaji wa elimu ya sekondari katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu na Ardhi Oevu. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu (*PFM*) ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kuendeleza usimamizi shirkishi wa misitu katika baadhi ya Halmashauri za Mikoa ya Morogoro, Iringa Njombe, Mbeya, Lindi Tanga, Ruvuma, Rukwa, Lindi, Kigoma, Mtwara, Mara, Shinyanga, Dodoma, Pwani na Kagera chini ya ufadhilli wa *DANIDA* na *Finland*. Kiasi cha fedha kilichotolewa hadi Machi 2012 ni sh. 490,493,000.00. Fedha hizo zimetumika kuratibu utoaji wa elimu kwa jamii kuhusiana na hifadhi ya misitu na mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Programu Shirikishi ya Usimamizi wa Ardhi

Oevu iliidhinishiwa sh. 758,600,000.00. Kati ya fedha hizo sh. 158,600,000.00 ni kwa ajili ya uratibu na shilingi 600,000,000.00 zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotekeleza Programu. Programu hiyo inatekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mikoa ya Arusha, Iringa, Njombe na Mbeya. Kazi zilizotekelezwatika Mamlaka hizo ni pamoja na kufanya mapitio ya mwongozo wa usimamizi wa fedha na utekelezaji wa programu na kuandaa mafunzo kuhusu mwongozo kwa watendaji wa Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*ASDP*). kwa kutumia bakaa ya fedha ya mwaka 2010/2011 na fedha za 2011/2012, Halmashauri zimeendelea na uboreshaji wa miundombinu ya masoko ya mazao kwa kujenga jumla ya masoko 84 kwa wanufaika 197,750, barabara za maeneo ya Vijiji (*feeder roads*) zenye urefu wa kilomita 263 na madaraja madogo 25 kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa mazao na pembejeo yamefanyiwa ukarabati. Aidha, kwa upande wa miundombinu ya mifugo, jumla ya malambo 27 yamejengwa kwa wanufaika 47,837. Vile vile Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuvijengea uwezo vikundi mbalimbali vya wakulima kiuchumi katika maeneo yao na jumla ya wanufaika 17,315 wamepatiwa mafunzo ya uboreshaji wa bidhaa zinazotokana na kilimo ili kuwa na uhakika wa masoko. Pia jumla ya mashamba darasa 4,542 na vikundi 14 vya watumia maji (*Water User Association*) vimepatiwa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji mazao ya kilimo na mifugo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Jumla ya shilingi 677,000,000.00 zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 65 kwa ajili ya kutekeleza mkakati wa kufufua na kuendeleza Sekta ya Viwanda vya Ngozi. Kila Halmashauri imepangiwa kutumia jumla ya sh. 10,415,384.00 zinazotekeliza mkakati huo. Vikao vya uhamasishaji, mafunzo, warsha na ziara za mafunzo vilifanyika kwa wadau wa zao la ngozi ikiwa ni pamoja na Wafugaji, Wachunaji, Wawambaji, Wasindikaji, Wachambuzi wa Madaraja na Wafanyabiashara, Madiwani, Maafisa Ugani, Wakuu wa Idara, Viongozi wa Vijiji na Vitongoji. Uhamasishaji huu umeleta ufahamu juu ya umuhimu wa zao la ngozi na umechangia katika ongezeko la ubora na biashara ya zao la Ngozi. Vile vile, vimeanzishwa vikundi vya ujasiriamali katika usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za zao la ngozi na uundaji wa Vyama vya Wadau wa zao la ngozi unaoendelea kufanyika katika Halmashauri zote zinazotekeliza Mkakati.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2012 jumla ya ngozi za ng'ombe zilizokusanywa zilikuwa ni 475,639, ngozi za kondoo ni 94,166 na ngozi za mbuzi ni 322,249. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya sh. 855,900,000.00 zimetengwa kwa ajili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 65 Tanzania Bara zinazotekeliza Mkakati huu na jumla ya sh. 25,000,000.00 zimetengwa kwa ajili ya uratibu.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Mfuko wa Pamoja wa Afya (*Health Basket Fund*). Serikali kupitia Mfuko wa

pamoja wa Afya katika kipindi cha fedha cha mwaka 2011/2012 imeweleva jumla ya Sh. 80.99 bilioni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma katika zahanati 4,105, vituo vya afya 457 na hospital 112 zinazomilikiwa na Serikali ili kuimarisha huduma za tiba na Afya kwa ujumla. Aidha, kuitia Mfuko huu shughuli zifuatazo zimetekelizwa:

Ununuzi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi, kujenga uwezo kwa watumishi wa sekta ya afya wa ngazi zote, usimamizi, ufuatiliaji na uratibu na kuimarisha muundo wa sekta ya afya. Vile vile Mfuko huu umesaidia kuimarisha utaratibu wa rufaa kutoka vituo vya afya au zahanati kwenda Hospitali za Wilaya na usambazaji dawa, chanjo na vitendanishi. Mfuko huu pia umetumika kuhakikisha watumishi wanakuwepo katika vituo vya kutolea huduma masaa yote na upatikanaji wa maji, umeme na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taasisi na Mashirika. Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kimeendelea na mipango yake ya kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Katika kipindi hicho Chuo killiweza kuanzisha kozi mpya nne, hivyo kufanya jumla ya kozi zinazotolewa mpaka sasa kuwa nane kutoka nne za awali. Kozi mpya zilizoanzishwa zinalenga kuongeza wataalam wa fani ambazo zitasaidia kuimarisha utendaji kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kozi hizo ni: Astashada ya Maendeleo ya Jamii, Astashahada ya Usimamizi wa Rasilimali Watu, Stashahada ya Maendeleo ya Jamii na Stashahada ya Usimamizi wa Rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, udahili wa wanafunzi pia uliongezeka kutoka wanafunzi 1,389 mwaka 2010/2011 hadi kufikia wanafunzi 2,286 katika mwaka wa masomo 2011/2012. Idadi hii ni ongezeko la wanafunzi 897 sawa na asilimia 65 ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka wa masomo 2010/2011. Chuo kiliendesha mafunzo ya muda mfupi kwa Wenyeviti wa Vijiji 32 vya Halmashauri za Mbinga na Maafisa Watendaji wa Vijiji 20 wa Halmashauri za Misenyi, Magu, Karagwe na Ukerewe, Wakuu wa Idara kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nzega (Maafisa sita) na Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo kilipewa kiasi cha shilingi bilioni 1.5 ikiwa ni ruzuku ya miradi ya maendeleo. Kiasi cha shilingi 426 milioni kimetumika kulipia sehemu ya fidia ya eneo lililochukuliwa na Chuo kwa ajili ya upanuzi, shilingi milioni 300 zitatumika kujenga nyumba mbili (2) za watumishi, shilingi 700 zitatumika katika mradi wa ujenzi wa kituo cha afya na sehemu ya kiasi kilichobakia shilingi 75 milioni kimetumika kuweka samani katika nyumba mpya 15 za watumishi (daraja la A na B).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo kimetenga shilingi milioni 650 kwa ajili ya kulipa fidia. Serikali itaendelea kukiimarisha Chuo kwa kuongeza idadi ya wataalam mbalimbali ili kiweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Usafiri wa Haraka (Dar es Salaam *Rapid Transit - DART*). Usafiri wa haraka Dar es Salaam (*DART*) ni Mkakati wa Serikali wa muda mrefu utakaotumia mabasi makubwa kupitia njia maalum katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano. Usanifu wa kina wa mradi awamu ya pili (*Kilwa Road*) na ya tatu (*Nyerere Road*) umekamilika. Ujenzi wa Miundombinu awamu ya kwanza katika barabara ya Morogoro umeanza kutekelezwa. Wakala unakamilisha usanifu wa kina wa mfumo wa *DART* awamu ya pili na ya tatu yenye urefu wa kilomita 42.3.

Mheshimiwa Spika, gherama za ujenzi wa mfumo huu awamu ya kwanza kupitia Benki ya Dunia ni dola za Marekani milioni 225.37 na Serikali ya Tanzania hadi sasa imechangia shilingi bilioni 11.5. Sekta Binafsi inatarajiwa kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani milioni 40.9. Aidha, hivi sasa mradi umefikia hatua muhimu ya utekelezaji baada ya kusainiwa kwa mkataba kati ya Kampuni ya Ujenzi ya *STRABAG* kutoka Ujerumani na Serikali tarehe 22 Desemba 2011. Wakala pia umelipa fidia awamu ya kwanza katika kituo cha mabasi Ubungo kwa kutumia shilingi milioni 500 zilizokuwa zimetengwa mwaka 2011/2012. Matarajio kwa sasa ni kwamba ifikapo mwaka 2014 sehemu kubwa ya mradi itakuwa imekamilika na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (*LAPF*). Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Mfuko uliandikisha wanachama wapya 10,195 kati ya lengo la kuandikisha wanachama 10,216. Hadi Machi 2012, Mfuko ulikusanya michango ya

wanachama shilingi bilioni 66 kati ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 87.5. Katika lengo la uwekezaji, Mfuko uliwekeza shilingi bilioni 111.46 kati ya lengo la kuwekeza shilingi bilioni 163.83. Vilevile, katika kipindi hicho Mfuko ulipata shilingi bilioni 20.37 kutokana na uwekezaji uliokuwepo kati ya matarajio ya kupata shilingi bilioni 43.81 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Mfuko unategemea kuandikisha wanachama wapya 11,591 na kufanya idadi ya Wanachama kuongezeka kutoka 92,269 Juni 2012 hadi 103,860 ifikapo Juni 2013. Mfuko umelenga kukusanya shilingi bilioni 107.66 kutokana na Michango ya wanachama na kuwekeza shilingi bilioni 196.74 kwenye vitega uchumi mbalimbali na kulipatia Shirika mapato ya shilingi bilioni 42.67. Pia Mfuko unategemea kutumia kiasi cha shilingi bilioni 35.27 kwa ajili ya malipo ya mafao. Aidha, Mfuko katika kutekeleza Sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii, umepanga kuendelea na utafiti wa kubainisha utaratibu bora wa kutoa mafao ya elimu na njia muafaka ya kupanua wigo kwa sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo yake, Shirika la Elimu Kibaha kwa mwaka 2011/12 limeweza kutoa Elimu na malezi bora kwa wanafunzi 2,920. Wanafunzi 915 walipata elimu ya msingi (wavulana 447 na wasichana 468), Wanafunzi 1,532 walipata Elimu ya Sekondari Kidato cha Kwanza hadi cha Nne (Wavulana 855 na Wasichana 677) na wanafunzi 373 ambao wote ni Wavulana walipata Elimu ya Sekondari Kidato cha Tano na Sita. Aidha,

vitabu 914 vilinunuliwa, Walimu 126 walilipwa posho ya nauli wakati wa likizo, walimu 26 walikuwa wakiendelea na masomo katika ngazi ya Shahada na Walimu 11 walajiriwa. Shirika lilitoa huduma ya Maktaba kwa wadau 34,112, wanaume 27,706 na wanawake 7,406.

Mheshimiwa Spika, elimu ya nadharia na vitendo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi ilitolewa kwa wanachuo 408 (wavulana 245 na wasichana 163). Mafunzo yaliyotolewa ni Kilimo na Mifugo, Ujenzi na Useremala, Ushonaji na Upishi, Ufundi wa Magari, Uundaji na Ufuaji Vyuma na Umeme wa Majumbani. Mafunzo ya muda mfupi yalitolewa kwa wadau 255. Mafunzo hayo yalikuwa ni udereva, ujasiriamali, kilimo cha bustani, kilimo cha uyoga, kutengeneza tofali na kuchakata ngozi.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kinga na tiba kupitia Hospitali Teule ya Tumbi ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani ilitolewa kwa wagonjwa 247,985. Kati yao waliolazwa ni 50,949 (wanawake 33,798 na wanaume 17,151) na wa nje walikuwa 197,036 (wanawake 105,246 na wanaume 91,790). Pia hospitali ilihudumia majeruhi wa ajali za barabarani 2,724.

Mheshimiwa Spika, Shirika pia liliendelea kupambana na janga la UKIMWI. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, wagonjwa 6,168 (wanaume 2,845 na wanawake 3,323) walipewa ushauri nasaha na kupimwa UKIMWI. Wagonjwa 1,051 walisajiliwa katika Kliniki ya kutoa huduma kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI (CTC). Ujenzi wa upanuzi wa Hospitali ya Tumbi

awamu ya pili inayojumuisha ujenzi wa vyumba vyatupasuaji, ofisi na sehemu ya mapokezi uliendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Jukumu la Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2012 mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 1.028 imetolewa kwenye Halmashauri tatu za Lushoto, Mbinga na Mtwara Mikindani na kufanya mikopo yote iliyotolewa kufikia jumla ya shilingi bilioni 5.5 ikilinganishwa na maombi yaliyowasilishwa ya jumla ya shilingi bilioni 25.1 tangu Bodi ianzishwe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho michango ya Akiba ya jumla ya shilingi milioni 322.4 imewasilishwa kati ya shilingi bilioni 1.1 zilizokadiriwa na kufanya michango yote ya akiba kufikia jumla ya shilingi bilioni 4.9 ikilinganishwa na kiasi kilichopaswa kuchangwa cha jumla ya shilingi bilioni 5.6. Kuhusu Mikopo na riba, jumla ya shilingi milioni 279.7 zimerejeshwa na kulipwa kati ya shilingi milioni 958 zilizokadiriwa. Uwasilishaji wa Michango na marejesho ya mikopo umekuwa siyo wa kuridhisha. Hadi tarehe 15 Aprili, 2012, Bodi inazidai Halmashauri 64 jumla ya shilingi bilioni 3.1 kwa viwango tofauti kutokana na Michango ya Akiba (*MCR*) na Mikopo pamoja na Riba.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuchukua hatua za kuufanya marekebisho muundo wa Bodi. Matarajio ya marekebisho haya ni kuwa na chombo cha fedha cha Serikali za Mitaa kilichoimarika na

kinachojitegemea kwa kuwa na uwezo wa kusimamia na kuendesha shughuli zake kwa asilimia 100 katika nyanja zote za utumishi, kifedha na teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza napenda kutoa pole kwa familia ya Marehamu Mzee Mussa kutoka Baraza la Wawakilishi ambaye alikuwepo katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inapenda kuwashukuru wadau wote ilioshirikiana nao katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2011/2012 na inatoa rai waendelee kutoa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii sasa kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano walionipa katika kipindi hiki. Aidha, nawashukuru Watumishi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Ombeni Yohana Sefue kwa kukamilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013. Nawashukuru Watanzania wote na Washirika wetu wa Maendeleo kwa michango yao ambayo imewezesha Serikali kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuwashukuru Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa

Ismani, Waziri wa Nchi (Sera, Uratibu na Bunge); Mheshimiwa Dokta Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, Waziri wa Nchi (Uwekezaji na Uwezeshaji); Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanry, Mbunge wa Siha, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu) kwa ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa jitihada walizoonesha katika kipindi hiki. Nawashukuru vile vile Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya Uongozi wa Makatibu Wakuu, Bwana Peniel Moses Lyimo na Bwana Hussein Athuman Kattanga na Naibu Makatibu Wakuu, Bwana Charles Amos Pallangyo, Jumanne Abdallah Sagini na Alphayo Japan Kidata kwa ushauri wao wa Kitaalam ambao wamenipa mimi na Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi katika kipindi hiki. Nawashukuru kwa kukamilisha maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2012/2013. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda nimshukuru Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu na kuendelea kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Pia, namshukuru Mheshimiwa Dokta Mohamed Gharib Bilal, Makamu

wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dokta Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kuwatumikia Watanzania. Vilevile, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wote wa Kitaifa na wa ngazi nyingine zote kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, napenda kuwashukuru Wapiga Kura wangu kwa imani na ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuleta maendeleo ya Jimbo la Katavi. Naomba vilevile katika kumalizia nimshukuru Mama Tunu Pinda Kidoshambaye muda wote ndiye amekuwa kwa kweli akinipa moyo na kunipa ngumu pamoja na watoto wangu ambao mara nyingine huwa wanajisikia kuumia zaidi ninapopata mitikisiko. Wote hawa nasema ahsante sana kwa kunipa nguvu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge ya Mwaka 2012/2013. Kwa mwaka 2012/2013, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi bilioni mia moja sabini na sita, milioni mia saba tisini na nne, laki nane thelathini na nane elfu (176,794,838,000). Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni sitini na nane, milioni mia tano ishirini na mbili, laki nane sitini na sita elfu (68,522,866,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni mia moja na nane, milioni mia mbili sabini na moja, laki tisa

sabini na mbili elfu (108,271,972,000) ni kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kwa mwaka 2012/2013, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zake inaombewa jumla ya Shilingi bilioni mia moja themanini na sita, milioni mia nane tisini na moja, laki tano tisini na nane elfu (186,891,598,000). Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni mia moja sitini na nne, milioni mia sita kumi na nne, laki saba ishirini na sita elfu (164,614,726,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni ishirini na mbili, milioni mia mbili sabini na sita, laki nane sabini na mbili elfu (22,276,872,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaombewa jumla ya Shilingi bilioni mia moja sabini na tatu, milioni mia mbili sabini na sita, laki saba sitini na moja elfu (173,276,761,000). Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni mia moja arobaini na sita, milioni mia tano hamsini na mbili, laki mbili sitini na mbili elfu (146,552,262,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni ishirini na sita, milioni mia saba ishirini na nne, laki nne tisini na tisa elfu (26,724,499,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Aidha, Halmashauri zote zinaombewa jumla ya shilingi trilioni tatu, bilioni mia mbili sabini na tisa, milioni mia nane; na sabini na tano elfu (3,279,800,075,000). Kati ya fedha hizo, Shilingi trilioni mbili, bilioni mia saba thelathini na tano, milioni mia sita arobaini na sita, laki moja kumi na saba elfu (2,735,646,117,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida

na Shilingi bilioni mia tano arobaini na nne, milioni mia moja hamsini na tatu, laki tisa hamsini na nane elfu (544,153,958,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano inaombewa jumla ya Shilingi bilioni mia moja kumi na tatu, milioni mia mbili ishirini, laki sita hamsini na tatu elfu (113,220,653,000) kwa ajili ya Mfuko wa Bunge ambapo Shilingi billioni mia moja kumi na moja, milioni mia tano themanini na tano, laki sita hamsini na tatu elfu (111,585,653,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni moja na milioni mia sita thelathini na tano (1,635,000,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya kwa muhtasari, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013 ya jumla ya Shilingi bilioni mia moja kumi na tatu, milioni mia mbili ishirini, laki sita hamsini na tatu elfu (113,220,653,000) kwa ajili ya Mfuko wa Bunge, na jumla ya Shilingi triliioni tatu, bilioni mia nane kumi na sita, milioni mia saba sitini na tatu, laki mbili sabini na mbili elfu (3,816,763,272,000) kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiwa ni Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo za Ndani na Nje kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Hotuba hii, yapo Majedwali ambayo yanafafanua kwa kina Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi

zake; Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**  
Mheshimiwa Spika, Naafiki.

(*Hoja lilitolewa lamuliwe*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono na sasa tutaendelea na majadiliano jioni.

Waheshimiwa Wabunge, bahati si nzuri au nini lakini kama nilivyosema asubuhi kwamba leo tunazo hotuba nyingi sana na inakuwa kama vile tunavyowasilisha asubuhi basi ndiyo hivyo hivyo hotuba zitakavyokuwa nyingi. Kwa hiyo, tukirudi mchana atakayezungumza wa kwanza ni Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na hotuba hizi pia na Kamati ya Fedha na Uchumi kwa sababu ina sehemu fulani katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Pia atakuja Kiongozi wa Kambi ya Upinzani atatoa hotuba yake na yeye ana *parts* mbili, atakuwepo yeye na Msemaji mwengine katika eneo la TAMISEMI. Kwa hiyo, utakuta bado tuna vihotuba kama vinne hivi. Kwa hiyo, baada ya hapo tutaingia katika kuchangia hoja hizi.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, kanuni ya 68(7) naomba kupata mwongozo wako.

Wakati Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anawasilisha maelezo ya kiutendaji katika ukurasa wa 28 wa kitabu cha hotuba kuna kiambatanisho kwanza kabisa ambacho naona kinaweza kunyofoka na kudondoka wakati wowote, sijui kama kimewekwa makusudi au lah! Lakini *headline* yake imeitwa fedha za chenji ya Rada.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mwongozo wako ili kuweka kumbukumbu sahihi kwa ajili ya vizazi vijavyo, Tanzania ilifanya biashara gani na Uingereza hadi tukapata fedha hii? Lakini kimsingi *export* za namna hii Tanzania sisi hatuna. Fedha za chenji ya Rada hii ilipaswa isomeke hizi ni fedha za rushwa ya Rada na mle ndani kuna maelezo yanatolewa kwamba Serikali ilipokea fedha za fidia ya ununuzi, tulifikiwa nini sisi? Kwa hiyo, kwa hakika nadhani *para* hii inapaswa kuitwa fedha za rushwa ya ununuzi wa Rada. Hiyo ni sehemu ya kwanza.

Sehemu ya pili, wenzetu wa Uingereza wamekuwa makini wamechukua hatua kwa wale ambao wamebainika na makosa ya rushwa. Nataka Bunge lako lituambie hapa ndani sisi tumechukua hatua gani kwa waliohusika kwenye hii biashara ya rushwa na kama hawajachukuliwa hatua *way forward* ni nini?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge hakuna mwongozo, wewe umeanza kujadili hotuba kabla haijaanza kujadiliwa. Kwa hiyo, utakapopata muda wa kujadili unaweza kujadili hayo unayoyasema kwa sababu hakuna cha mwongozo hapa, hiyo umesoma hotuba ya watu wameandika, wewe una uhuru wa *ku-challenge* hotuba hii na hayo uliyoyasema una uhuru wa kuyasema wakati wake. Kwa hiyo, sina mwongozo wala siwezi kutoa mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo dogo tu, hawa wenzetu wa maeneo yanayolima Pamba nadhani walikuwa wawe na kikao chao leo, lakini nimeombwa nieleze kwamba, naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge na Wakuu wa Mikoa wa maeneo yanayolima pamba kwamba kikao chao hakitakuwepo leo kwa sababu viongozi wawakilishi wa Chama cha Wakulima wa Pamba kinaitwa *TACOGA* hawajafika, kwa hiyo wanatarajiwa muda wowote kufika leo. Kwa hiyo, kesho inawezekana kuwepo kikao lakini saa watatangaza kesho asubuhi baada ya viongozi wengine kufika. Kwa hiyo, leo hakuna kikao lakini kesho mtakuwa na kikao, lakini kuhusu saa kamili nadhani asubuhi wakati wa kikao watakuwa wamejua ni saa ngapi na mkutane katika Ukumbi gani. Kwa hiyo, leo hakuna kikao.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tukirudi hapa zile hotuba za makundi mbalimbali bado wataendelea halafu tutaanza na mjadala jioni.

Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge.

*(Saa 6.52 mchana Bunge lilitifungwa mpaka  
saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama)  
Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, karibuni tena kwenye kipindi chetu cha jioni. Kwa mujibu wa ratiba iliyowekwa Mezani kwa siku hii ya leo asubuhi, tumeshamsikia mtoa hoja ambaye ni Waziri Mkuu akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake na baadaye akafuatiwa na Waziri, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na uchambuzi wa makadirio hayo kutoka katika Kamati za Bunge lakini vilevile kutoka upande wa Wasemaji wa Upinzani. Mheshimiwa Spika alitoa Mwongozo tutakuwa na wachangiaji takribani watatu (3) na kwa upande wa Upinzani tutapata Mwongozo kutoka kwao kama na wao watajigawa katika makundi mawili kama vile bajeti ilivyowasilishwa. Kwa hali hiyo, naomba sasa tuanze na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi H. Chana ambaye atakuwa na dakika thelathini (30), Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, naomba ajiandae. Mheshimiwa Pindi Chana!

**MHE. PINDI H. CHANA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za 99 (7) na 114 (11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge letu Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 kwa Fungu 25 – Waziri Mkuu; Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu; Fungu 42 – Mfuko wa Bunge; Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyaa na Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawasilisha maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, kwa Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Mafungu 36, 47, 54, 63, 70 – 89 na 95 kwa ajili ya Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kueleza, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu, kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Aidha,

nawapongeza Mawaziri wote walioteuliwa hivi karibuni, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na nawatakia uwajibikaji mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Baada ya kuletewa kazi ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilikutana Dar es Salaam na kupokea taarifa ya utekelezaji ya Mwaka 2011/2012 pamoja na maelezo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Taasisi zake yaliwasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Nchi, Mheshimiwa William Lukubi. Pamoja na mambo mengine, Kamati ilielezwa kuhusu makusanyo ya maduhuli hadi kufikia mwezi Aprili, 2012 na matumizi kwa Mafungu yote. Aidha, Kamati ilielezwa changamoto zilizoikabili Ofisi hii na Taasisi zake katika utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji na utendaji kazi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

(i) Kuiongezea uwezo Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (*CDA*) ili iimarishe miundombinu kwa

lengo la kupunguza misongamano. Kamati ilielezwa kwamba mpango kabambe wa Mji wa Dodoma umefanyiwa mapitio ili uendane na hali halisi ya ukuaji wa mji wa Dodoma. Mapitio hayo yanaiwezesha *CDA* sasa kupanga vizuri mji kwa kupima viwanja katika maeneo yanayozunguka mji ili kuondoa msongamano unaoanza kujitokeza katikati ya mji.

(ii) Kukamilisha mapema kwa ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge Majimboni. Kamati ilielezwa kwamba Serikali kupitia Hazina imeahidi kuipatia Ofisi ya Bunge kiasi cha Shilingi Bilioni Moja kilichotengwa kwa madhumuni hayo. Pamoja na hayo Serikali kupitia Ofisi ya Bunge inaandaa Mpango wa kuwezesha kujenga Ofisi zote kwa mara moja kwa mkopo (*Build & Transfer*) na baadaye kuendelea kulipa deni kidogo kidogo.

(iii) Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*CDCF*) kuhamishiwa Ofisi ya Bunge. Kamati ilielezwa kwamba Serikali bado inaendelea na mchakato wa kuhamishia fedha za maendeleo ya Jimbo *CDCF* Ofisi ya Bunge kama ilivyopendekezwa hapo awali. Aidha, Kamati ilipokea taarifa kuwa mchakato huu hakuweza kufanyika mapema kama ilivyokuwa kwenye ujenzi wa Ofisi za Wabunge kwa sababu *CDCF* iliundwa kwa Sheria, hivyo lazima kwanza yafanyike marekebisho ya Sheria kabla ya kukamilisha zoezi la kuhamisha Mfuko huu.

(iv) Wabunge kujeunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Bunge kupitia Tume ya Huduma za Bunge ipo kwenye

mchakato wa kuboresha huduma za Matibabu kwa Wabunge ikiwa ni pamoja na kuandaa Mpango Mahususi wa Bima ya Afya kwa Waheshimiwa Wabunge na familia zao.

(v) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ishirikiane na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kutoa Elimu ya mpiga kura mapema kwa kuzingatia kwamba kuna Sheria mbili katika uendeshaji wa uchaguzi wa Zanzibar. Kamati ilielezwa kwamba Serikali imepokea ushauri wa Kamati na kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaimarisha ushirikiano na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar wakati wote wa zoezi la uchaguzi.

(vi) Nafasi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwenye kesi za uchaguzi. Kamati ilielezwa kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, Sura ya 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawajibika kugharamia mashahidi wote wanaoitwa kwa upande wa Serikali katika kesi za uchaguzi za Ubunge. Aidha kwa kesi za uchaguzi za Madiwani, Tume inagharimia si mashahidi tu, bali pia Wanasheria wa Serikali wanaoendesha kesi hizo.

(vii) Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi na ugawaji wa Majimbo na Kata ufanyike mapema kabla ya uchaguzi ili kuondoa usumbufu na kuongeza ufanisi. Kamati ilielezwa kuwa ushauri wa Kamati umepokelewa na Serikali na hivyo Sheria za Uchaguzi zinakusudiwa kurekebishwa ili kuweka ukomo wa muda wa kugawa maeneo ya uchaguzi (Kata).

(viii) Ofisi ya Tume ya kuratibu udhibiti wa dawa za kulevyia ijengewe uwezo wa kutambua dawa hizi badala ya kumtegemea Mkemia Mkuu wa Serikali ili kupunguza urasimu na mazingira ya rushwa. Kamati ilielezwa kwamba suala hili limeingizwa kwenye mchakato wa Marekebisho ya Sheria ya Tume itakayowezesha kuundwa kwa Chombo kipycha chenye nguvu za kudhibiti Dawa za Kulevyia.

(ix) Shughuli za Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyia zielekezwe hadi Wilayani kama ilivyo TACA/IDS ili kurahisisha utendaji kazi wao. Kamati ilielezwa kwamba suala hili litazingatiwa kwenye Mchakato wa uundwaji wa Chombo kipycha cha Udhibiti wa Dawa za Kulevyia.

(x) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu iwe na Mitaala ya Elimu ya UKIMWI kwa Shule za Msingi na Sekondari. Kamati ilielezwa kwamba Mitaala ya elimu kuanzia darasa la tano na kuendelea hadi Sekondari ina masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazoikabili Ofisi ya Waziri Mkuu. Pamoja na utekelezaji wa majukumu yake kama ilivyoonyeshwa kwenye vipaumbele kwa Mwaka 2011/2012, Ofisi ya Waziri Mkuu inakabiliwa na Changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Matukio ya maafa ya mara kwa mara yaliyosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi. Mfano mafuriko yaliyotokea mwaka jana katika bonde la Mto Msimbazi, Dar es Salaam na kusababisha waliokuwa

wakazi wa eneo hilo kuhamishiwa maeneo ya Mabwepande ambapo hata hivyo hadi leo kumekuwapo na malalamiko ya fidia, ugawaji wa viwanja na ukosefu wa huduma za kijamii katika makazi hayo.

(ii) Ukosefu wa majengo mengi ya Serikali na kupelekea kulipa kodi kubwa ya pango kama vile Jengo la Ofisi ya Tume ya Uchaguzi unaosababisha Tume kwa hivi sasa kupanga katika jengo la Mamlaka ya Posta na Simu, Tanzania (Posta House) na katika majengo ya Wakala wa Manunuzi Serikalini (*GSPA*) kwa ajili ya kutunzia Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Vifaa vya Uchaguzi. Hali hii imefanya Tume kuwa na Ofisi tatu maeneo tofauti na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa uratibu na utendaji wa shughuli za Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

(iii) Kutokubalika kikamilifu kwa mikakati ya kudhibiti maambukizi ya VVU mionganoni mwa jamii pamoja na kutojulikana kwa ukubwa wa tatizo la matumizi ya Dawa za Kulevya kitaifa.

(iv) Unyanyapaa na kubaguliwa kwa watumiaji wa Dawa za Kulevya, uhaba wa Wataalamu wa Tiba ya Waathirika wa Dawa za Kulevya pamoja na maambukizi ya VVU mionganoni mwa watumiaji wa Dawa za Kulevya kuonekana kuwa ni suala geni.

(v) Ruzuku ndogo kwa Halmashauri kwa ajili ya shughuli za maendeleo ukilinganisha na fedha zinazoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo. Kufuatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati yangu na kwa kuzingatia dhima, azma na majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 63(2), inayotoa madaraka ya kuisimamia na kuishauri Serikali, kwa niaba ya Bunge Kamati inashauri na kuagiza Ofisi hii na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 25 – Waziri Mkuu na Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati inashauri na kuagiza yafuatayo:-

(i) Pamoja na kutoa masikitiko ya ucheleweshaji wa vitabu vya bajeti kwa mwaka jana, bado tatizo hilo limeendelea kutokea kwa mwaka huu na hivyo kusababisha Wajumbe wasipate nafasi ya kusoma vitabu hivyo kwa usahihi na kutoa ushauri wa kina kwa Serikali. Kamati inazidi kusisitiza kwamba utaratibu wa kuleta vitabu Ofisi ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 96 (1), Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la 2007) uzingatiwe, kwani kutofanya hivyo ni kuvunja Kanuni ambazo tumezitunga wenyewe.

(ii) Kamati imepitia vitabu vya Bajeti, *Volume IV, Public Expenditure Estimates Development Votes (Part-A), Ministerial and Regional Development Programmes for the year from 1st July, 2012 to 30th June, 2013 Page 243*, Fungu 84, ambalo ni Mkoa wa Singida na kubaini kwamba Kifungu 5402, kinachohusu ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida kimetengewa Sh.1,805,154,000. Kamati ilipata nafasi ya kutembelea

Mkoa wa Singida na hivyo kujionea ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ambao unahusisha pia ujenzi wa jengo la kitengo cha uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza (*Center for non communicable diseases*).

Kamati inaipongeza Serikali kwa kubuni mradi huo ambao inaamini kwamba baada ya ujenzi wake kukamilika, utaweza kusaidia utoaji wa huduma kwa Mikoa ya Magharibi na Kati na hivyo kuzipa unafuu Hospitali za *Ocean Road* na Muhimbili katika kutibu baadhi ya magonjwa. Kamati inaiomba Serikali kuingia mikataba na Taasisi za kifedha ili ziweze kusaidia ujenzi wa hospitali hii kwani kwa kutegemea fedha za bajeti ya Serikali, itachukua takribani miaka 75 kukamilisha ujenzi wa hospitali hii.

(iii) Kamati imepitia vitabu vya Bajeti na kugundua kwamba fedha nyingi zimebekwa kwenye malipo ya pango kama inavyojionyesha katika Mafungu ya 25, 27 na 61. Kamati inaitaka Serikali kutoa ufanuzi wa hali hii na sababu zinazofanya taasisi hizo zisijenge majengo yao wenyewe ili kupunguza gharama za kulipia majengo ya kukodi kwa kila mwaka.

(iv) Kumekuwepo na taarifa kwa baadhi ya maeneo kwamba wanakabiliwa na matatizo ya ukosefu wa chakula. Hata hivyo kumekuwepo na taarifa nyingine kwamba baadhi ya maeneo na hasa kwenye maghala, kuna hifadhi ya chakula kingi ambacho hushindwa kusafirishwa kwenye maeneo ya

uhaba wa chakula. Kamati inaagiza Serikali kuitia Kitengo cha Maafa kutafuta njia mbadala za kusafirisha chakula kwenda kwenye maeneo ambayo yana upungufu. Aidha, wafanyakazi wa Kitengo hicho wajitahidi kufanya utafiti na siyo kukaa ofisini. Kwa kufanya hivyo watabaini maeneo yenyé matatizo ya chakula ili wananchi wanaohusika waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na hivyo inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kamati inashauri Serikali kuongeza Bajeti iliyotengwa ya Sh.19,488,941,000 kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ili aweze kumudu majukumu yake ambayo ni pamoja na kutoa Elimu kwa Vyama vya Siasa. Tazama *Public Expenditure Consolidated Fund Service (Sec.1) and Supply Votes (Ministerial) for the year from 1st July, 2012 to 30th June, 2013 Page 128*. Aidha Serikali iangalie uwezekano wa kutafuta eneo la ujenzi wa Ofisi za Msajili wa Vyama vya Siasa kwani alipo sasa ni pafinyu sana na hivyo kusababisha utendaji kazi kuwa mgumu.

(ii) Ili kuboresha muundo wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Kamati inashauri Serikali kuwezesha kila kanda nchini kuwa na waratibu watakaosaidia kuratibu shughuli za Vyama vya Siasa Mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 42 - Mfuko wa Bunge, Kamati inashauri na kupendekeza yafuatayo:-

(i) Kamati inazidi kuishauri Ofisi ya Bunge, kupitia Idara ya Shughuli za Bunge ambayo ndiyo yenye jukumu la kuratibu maswali ya Wabunge, kuweka utaratibu mzuri utakaowawezesha Wabunge kuuliza maswali yakiwemo maswali kwa Waziri Mkuu, kwani uzoefu uliopo sasa unaonesha kuwa utaratibu wa kuwahi mapema kabla ya muda wa Bunge na kijiandikisha majina unaleta usumbufu mkubwa kwa Wabunge wanaohitaji kuuliza maswali hayo. Aidha, muda wa majuma mawili kwa shughuli za Kamati hasa kabla ya Mkutano wa Bajeti ni mfupi sana hususan Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo inasimamia Wizara na Ofisi saba na hivyo Kamati inashauri Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Serikali kufikiria kuongeza muda huo ili kuwawezesha Wabunge kupitia na kujadili Bajeti za Wizara na Idara kwa ufanisi zaidi.

(ii) Ofisi ya Bunge iharakishe mchakato wa kuwezesha Wabunge waweze kujiunga na matibabu kwa njia ya Huduma ya Bima ya Afya. Aidha, huduma hiyo iwe ni kwa Hospitali zote za binafsi na Serikali ili kupunguza gharama kubwa zinazotumika kuwasafirisha na kuwatibia nje ya nchi. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unakidhi mahitaji ya Wabunge ya Bima ya Afya.

(iii) Kamati inazidi kusisitiza mafunzo zaidi kwa watumishi wa ngazi zote wa Bunge na hasa Makatibu wa Kamati ili kuwajengea uwezo wa kuzihudumia Kamati na kukidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa. Aidha, kwa kuwa Makatibu Kamati ni wafanyakazi wa

kudumu, ni vema wakapewa mafunzo na elimu bora kuhusu mambo muhimu, kama vile uchambuzi wa bajeti, uchambuzi wa Miswada, Uandishi wa Taarifa pamoja na Utafiti ili waweze kuwasaidia Wabunge ambao huhitaji msaada na ushauri katika eneo husika. Safari za mafunzo (*Study Tours*) kwa Makatibu wa Kamati kwenda kuona wenzao katika Mabunge ya nchi zilizoendelea zitaongeza ufanisi na ni muhimu.

(iv) Muda wa kuchangia Bungeni ni mfupi sana na hivyo kufanya wawakilishi wa wananchi kutofanya kazi yao vizuri. Kamati inashauri jambo hilo liangaliwe ili ikibidi muda au siku za kuchangia ziongezwe.

(v) Kwa kuwa hivi sasa mabasi ya Bunge yamechakaa na hivyo kusababisha Ofisi ya Bunge kukodi magari zinapotokea safari za Wabunge, hususan Mikoani; Kamati inashauri mipango ifanyike ili mabasi mengine yanunuliwe kuliko kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kukodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge ni mashahidi kutokana na adha mbalimbali wanazokabiliana nazo wanapotumia mabasi ya Bunge ambayo bila shaka ni ya muda mrefu na pengine kwa vigezo vya matumizi ya magari ya Serikali yasingestahili kutumiwa hivi sasa.

(vi) Bado suala la maegesho ya magari na kumbi za mikutano limekuwa ni tatizo sugu hasa wakati wa vikao vya Kamati vinapofanyika Dar es Salaam. Kamati inazidi kusositiza kwamba Bunge lifanye mipango ya kutafuta eneo la maegesho kwa ajili ya

Wabunge, Wafanyakazi wa Bunge pamoja na wageni wanaokuja Bungeni kuhudhuria mikutano ya Kamati. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli za Kamati kufanyikia Dar es Salaam na kwa kuzingatia msongamano mkubwa wa majengo na magari uliopo hivi sasa, uangaliwe uwezekano pia wa kutafuta eneo lingine kubwa nje ya sehemu iliyopo ili kukidhi mahitaji ya shughuli za Kamati na Bunge kwa miaka ijayo. (*Future long term plans*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Kamati inapendekeza na kushauri yafuatayo:-

(i) Kamati imepata nafasi ya kutembelea Tume hii na kujionea mazingira magumu wanayoishi. Pamoja na ugumu huo wa mazingira, bado wanatumia fedha nyingi kulipia kodi ya pango kwa ajili ya majengo wanayoyatumia. Kamati inaiomba Serikali kutafuta kiwanja na hivyo kuanza mapema iwezekanavyo ujenzi wa Ofisi na Maghala yatakayotumiwa na Ofisi hii.

(ii) Kamati imefuatilia Bajeti ya Mwaka 2012/2013 na kuona Sh.3,763,681,000 iliyopangwa kwa ajili ya Tume hii na kupewa taarifa kwamba fedha nyingi kiasi cha TSh.741,321,000/= zinatumika kwa ajili ya kulipia kodi ya pango ya maghala yanayotumiwa na Tume hii. Tazama *Estimates of public expenditure Consolidated Fund Services (Sec. 1) and Supply Votes (Ministerial) for the year from 1st July, 2012 to 30th June, 2013 Page 384*. Kwa kuwa maghala yanayotumika ni majengo ya Serikali, Kamati inaiomba Serikali kufanya mipango ya

kuondoa kodi hiyo au kumilikisha majengo haya kwa Tume ya Uchaguzi ili fedha zinazotumika kulipia majengo hayo ziweze kutumika kwenye shughuli nyingine za maendeleo ya Tume.

(iii) Kamati imepewa taarifa na Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi tarehe 29/05/2012 kwamba Daftari la Kudumu la Wapiga Kura bado halijaboreshwu tangu kukamilishwa kwa Uchaguzi Mkuu, 2010. Kamati inaona kuwa jambo hilo ni kasoro kubwa kwa uhai na ukuzaji wa demokrasia nchini kwani zinapotokea chaguzi ndogo, watu wengi wananyimwa nafasi na haki ya kupiga kura kwa sababu hawajajilandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kamati inaishauri Serikali kulichukulia jambo hili kwa uzito unaostahili ili kuongeza fedha kwenye Bajeti ya Tume zitakazofanikisha mchakato wa uboreshaji wa Daftari hilo ili kuendana na Kifungu cha 15 (1) na (5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 inayotaka Daftari hilo kuboreshwa mara mbili kati ya chaguzi kuu mbili. Kamati inaamini kwamba kujitokeza kwa idadi ndogo ya Wapiga Kura kama ilivyojidhihirisha katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 na chaguzi ndogo za hivi karibuni za Igunga na Arumeru Mashariki, pamoja na mambo mengine, kumechangiwa pia na kutoboreshwu kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba mwaka 2014 tunategemea kuwa na Kura ya Maoni ya Katiba katika nchi yetu. Daftari la Kudumu la Wapiga kura litategemewa sana katika kura hii hivyo ni vema

kufanya maboresho mapema ili kuondoa tofauti zilizopo.

(i) Kamati inasikitishwa sana na vurugu na fupo ambazo zimekuwa zinajitokeza pindi chaguzi ndogo zinapofanyika. Kamati inaiagiza Serikali pamoja na Tume ya Uchaguzi kutoa elimu zaidi kwa Wapiga Kura na Vyama vya Siasa ili wananchi waelewe kwamba wakati wa uchaguzi siyo fursa ya uvunjaji wa Sheria na kwamba kila mwananchi anayo nafasi ya kutumia demokrasia katika kumchagua mtu anayemtaka.

(ii) Kamati inashauri Serikali kuiwezesha Tume ili iweze kujimarisha hadi kwenye Halmashauri zote nchini hivyo kuiwezesha Tume iwe na Ofisi na Watumishi wa kutosha. Hili litaendana na utaratibu mzuri wa kuhifadhi vifaa pamoja na kuwa na Maghala kwani uzoefu unaonyesha kwamba baada ya Uchaguzi kupita hakuna jitihada za kutosha za kuvihifadhi, kuvifuatilia na kuvisimamia vifaa vinavyotumika kwenye chaguzi. Hali hii haitoi picha nzuri kwa matumizi bora ya vifaa vya umma na fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyo. Kamati inapenda kueleza masikitiko yake kwamba maoni na ushauri uliotolewa mwaka jana kuhusu Tume hii kwa kiasi kikubwa hayajatekelezwa. Kamati inazidi kusisitiza na kuagiza kwamba maoni na ushauri huo utekelezwe na Kamati ipewe taarifa ya utekelezaji wake kila mara. Ushauri na maoni yaliyotolewa yalihu utatuzi wa changamoto nyingi zinazohusu Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Upungufu wa Rasilimali Watu wenyе taaluma pamoja na ukosefu wa mafunzo ya marа kwa marа.

(ii) Huduma ya matibabu kwa wathirika wa Madawa ya Kulevya kupatikana kwenye Hospitali zote za Wilaya.

(iii) Vita dhidi ya Madawa ya Kulevya itangazwe kama janga la Taifa kwani hivi sasa vijana wengi wameingia kwenye utumiaji wa Dawa za Kulevya na hivyo kusababisha ongezeko la maambukizi ya UKIMWI pamoja na ukosekanaji wa nguvu kazi.

(iv) Kuonyesha ni kwa jinsi gani Dawa za Kulevya zimeathiri jamii na uchumi na mikakati gani iliyopo katika kupambana na janga hili kwani wanaofanya biashara hii wana fedha nyingi na hivyo kuibua mbinu mpya kila marа.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACA/DS*) Kamati inaelekeza na kushauri ifuatavyo:-

(i) UKIMWI umeendelea kuwa janga la Kitaifa. Kamati inaiomba Serikali kuendelea kuongeza kasi ya utoaji wa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya kondomu pamoja na hatari ya kuwa na wapenzi wengi kwani ni kichocheo cha maambukizi mapya kwa jamii.

(ii) Kamati imesikitishwa na taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji, Tume ya Kudhibiti UKIMWI aliyoitao March,

2012 kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Benjaminsi Mkapa House, kwamba hivi sasa wahisani wengi wamejitoa kufadhili miradi ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kupunguza fedha zilizokuwa zinatolewa kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa huu. Kamati inapenda kupata ufanuzi wa Serikali kuhusiana na taarifa hizo ikiwa ni pamoja na kuelezea mikakati mbadala inayochukuliwa ili kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI.

(iii) Kamati inapenda kuiasa jamii kuondokana na fikra potofu za misemo kwamba UKIMWI ni sawa na ajali kazini na hivyo kila mwananchi awe mstari wa mbele kupiga vita maambukizi mapya ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonyesha kwamba mambukizi ya makusudi ya UKIMWI yameendelea pamoja na uwepo wa Sheria ya *HIV and AIDS (Prevention and Control) Act No. 28 of 2008, Sec. 47*, inayotoa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitano. Kamati inazidi kusitiza kwamba Serikali ifanye utafiti kujuu ni kwa kiasi gani baadhi ya watu wanasantaza UKIMWI kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI. Baada ya kueleza Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, sasa naomba kuelezea Bajeti ya Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 07 Juni, 2012, Kamati ilikutana Dar es Salaam ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri

Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Katika Kikao hicho, Kamati ilipokea maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, (Mb) - Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, Kamati pia ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa Mwaka 2012/2013 na Mikoa kwa Mafungu 36, 47, 54, 63, 70 – 89 na Fungu 95, yaliyowasilishwa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa. Aidha, Mheshimiwa Waziri alieleza kuhusu mpango mkakati wa Wizara, Dira na Dhima, mapato na matumizi na majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Shule za Msingi na Sekondari na kusimamia Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam. Pia, Mheshimiwa Waziri alifafanua kuhusu kazi zilizofanyika kwa kipindi cha Julai 2011 hadi Machi, 2012 na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha utekelezaji wa Mipango ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa Mwaka 2011/2012. Wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii na Mikoa kwa Mwaka 2011/2012 kama ilivyo ada, Kamati ya

Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ilitoa Maoni na Ushauri mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba tena kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri uliotolewa japo maeneo mengine yanahitaji kuboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati hii ilipokutana na Mheshimiwa Waziri, ilipata taarifa kwamba wakimbizi wapatao 162,256 kutoka Makambi ya Wakimbizi ya Mishamo na Katumba wamepatiwa uraia kati ya wakimbizi 218,000 walioomba. Kamati ilielezwa pia kwamba Serikali iliagiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuandaa waraka utakaozingatia maoni ya Kamati yangu yaliyotolewa mwaka jana na kuwasilishwa kwa Baraza la Mawaziri. Kamati inapenda kupata ufanuzi wa hatua iliyofikiwa hadi sasa ikiwa ni pamoja na tathmini iliyofanywa ili kujua madhara na faida za jambo hili kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiusalama kwa maeneo ambayo wakimbizi waliopata uraia watapelekwa au kama wameshapelekwa.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imepata taarifa kwa wadau mbalimbali kuwa kutokana na ufinyu wa fedha baadhi ya Halmashauri zinashindwa kufanya vikao vya kisheria kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 ya Mwaka 1982 wakati mwingine hupelekea Halmashauri kutowalipa Waheshimiwa Madiwani haki zao za vikao na hivyo kuwakopa Waheshimiwa Madiwani hao. Kamati inashauri jambo

hili liangaliwe kwa makini ili vikao vifanyike kwa wakati na Waheshimiwa Madiwani walipwe haki zao kama inavyostahili.

(iii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati ambao imekuwa ikiutoa mara kwa mara na hivyo hatimaye kupandisha posho ya madaraka ya Madiwani kutoka Sh.120,000 hadi 250,000 kwa mwezi. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri wa TAMISEMI kwa Kamati iliyotolewa tarehe 08/06/2012 katika Ukumbi wa Makumbusho, Dar es salaam. Hata hivyo, Kamati inazidi kusitiza kuwa suala la elimu na mafunzo kwa Madiwani lizidi kuzingatiwa kwani wao ndio wasimamizi wakubwa wa fedha zinazotolewa na Serikali kwenye Halmashauri zetu ambako ni moja ya maeneo ambayo yamekuwa yakilalamikiwa kwa matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

(iv) Kamati imepitia kwa makini taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ripoti Kuu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 2010/2011, Ukurasa wa 61-66. Ripoti hiyo imeainisha upungufu mwingi unaofanywa na Halmashauri nchini kama vile katika maandalizi na uwasilishaji wa taarifa za fedha, ulegevu katika usimamizi wa mapato na matumizi, upungufu katika udhibiti wa mishahara, upungufu katika usimamizi wa rasilimali watu, Sheria na Kanuni za Manunuzi kutofuatwa na upungufu katika uendeshaji wa Mifuko na usimamizi wa miradi.

Kamati inaishauri Serikali kuelekeza Maafisa Maduhuli kuhakikisha kwamba Sheria zote zinazoongoza matumizi ya rasilimali za umma

zinazingatiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba rasilimali hizo zinatumika katika namna bora ya kukidhi malengo kwa ufanisi. Aidha, Kamati inashauri kuwa kwa wafanyakazi ambao wamethibitika wameenda kinyume na taratibu za matumizi ya fedha, yaani ubadhirifu wachukuliwe hatua na sio kuhamishwa kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine maana ni kuhamisha tatizo.

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kujadili bajeti, Kamati ihoji juu ya fedha ya maendeleo kwa Mikoa mipyä na Wilaya mpyä. Hata hivyo, ilielezwa kuwa zipo shilingi billioni 70 kwa Mikoa hiyo mipyä na Wilaya mpyä. Kamati inaomba ufanuzi wa kujua fedha za maendeleo kwa Mikoa na Wilaya mpyä ziko katika ViFungu gani vyä bajeti.

(vi) Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji tunaomba liangaliwe upya, kwani Mabaraza hayo hayapangiwi fedha wala kuwezeshwa kielimu (*technical support*) na hasa ukizingatia kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 107, suala la kutoa haki ni jukumu la Mahakama. Hivyo Kamati inashauri kuwa Mabaraza ya Ardhi Vijijini yafanyiwe utafiti kama yanakidhi haja na Kamati ipewe taarifa.

(vii) Kamati imepokea taarifa ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, tarehe 8 Juni, 2012 katika Ukumbi wa Makumbusho, Dar es Salaam, kwamba mawasiliano yamefanyika na Hazina kuhakikisha kuwa makato ya mikopo ya Watumishi hayafanyiki hadi pale Hazina watakpopata maelekezo kutoka kwa waajiri

na siyo wakopeshaji. Hata hivyo, Kamati inazidi kusisitiza kwamba tatizo la kukopa kupita kiasi kwa wafanyakazi wa Halmashauri bado ni sugu kwani kuna baadhi ya Taasisi za Fedha zinatoa mikopo pasipo kumshirikisha mwajiri na hivyo kufanya baadhi ya wafanyakazi kutolipwa chochote wakati wa kupokea mshahara. Hii ni kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhusu Ripoti Kuu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 2010/2011, ukurasa wa 66&101. Kamati inatoa rai kwa Halmashauri zote nchini kusimamia na kutoa elimu kuhusiana na Waraka wa Utumishi wenye Kumb. Na. CCE.45/271/01/87 wa tarehe 19/03/2009 unaotaka makato ya mishahara ya wafanyakazi yasizidi 2/3 ya mishahara yao.

Kamati imesikitishwa na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011, ukurasa wa 101, kwamba katika jumla ya Halmashauri 55 zilizokaguliwa, kumebainika kuwepo jumla ya watumishi 8827 ambao wanapokea chini ya 2/3 ya mishahara yao. Watumishi wanapaswa kuelewa kwamba ukopaji unaozidi kiwango licha ya kwamba ni ukiukaji wa Sheria bali pia unapunguza heshima na morali ya kufanya kazi kwa ufanisi. Kamati inaiomba Serikali ichukue hatua za haraka kudhibiti makampuni yanayokopesha kwani makampuni mengi ya ukopeshaji yanawahadaa wananchi.

(viii) Kamati imepitia vitabu vya Bajeti na randama zilizowasilishwa na Wakuu wa Mikoa na kugundua kwamba malipo ya posho kwa watendaji ni makubwa. Kamati inaishauri Serikali kurejea upya miongozo ya

matumizi ya fedha kwenye miradi inayotekelzwa na Halmashauri kama vile *TASAF*, *UKIMWI*, Miradi ya Kilimo (*DADPs*), Miradi ya Maendeleo (*CDG*) na miradi ya uhifadhi wa mazingira. Aidha, Kamati inaagiza watendaji wa Halmashauri na hasa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wasimamie kikamilifu utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopo chini yao. Vilevile Kitengo cha Ukaguzi wa Serikali za Mitaa ambacho kipo chini ya OWM – *TAMISEMI* kiimarishe pamoja na Kamati za Fedha, Mipango na Utawala na kujengewa uwezo wa kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelzwa na Halmashauri. Pia Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI* kuangalia uwezekano wa kuwezesha kila Kamati husika za Madiwani kutembelea miradi yao na hivyo kuondoa mazoea ya Kamati ya Fedha na Utawala tu kufanya kazi hiyo kama ilivyo sasa.

(ix) Pamoja na azma nzuri ya Serikali ya kuendeleza na kukuza kilimo kupitia Sera ya Kilimo Kwanza, ili kuongeza mazao ya kilimo na biashara, bado Sera hii haijatekelezwa vema na hivyo kuongeza idadi ya sera zilizowahi kuanzishwa bila mafanikio. Hali hiyo inadhihirishwa na wingi wa matrekta ambayo yako kwenye maghala kwa Mikoa ya Dar es Salaam na hapa Dodoma. Kamati inapenda kupata ufanuzi ili kujua mkakati wa dhati uliopo katika kutekeleza sera hii pamoja na sababu zinazofanya matrekta kuendelea kuwa kwenye maghala kwa muda mrefu na siyo mashambani kwa wakulima.

(x) Mradi wa Mabasi yaendayo kasi (*DART*) bado unatekelezwa kwa kasi ndogo sana na inatia shaka kwa wananchi kuhusu muda kamili wa kukamilika

mradi huu. Kamati inapenda kupata ufanuzi wa vikwazo vinavyosababisha mradi huu usikamilike kwa wakati ili uweze kuanza kutoa huduma ya usafiri na hivyo kupunguza msongamano wa magari kwa jiji la Dar es Salaam ambao umekuwa ni usumbufu mkubwa.

(xi) Kamati inasikitishwa na upungufu wa ruzuku ya Serikali ikilinganishwa na bajeti inayoidhinishwa na Bunge. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011, ukurasa wa 73, inaonyesha kuwa katika mwaka wa Fedha 2010/2011, ukaguzi wa bajeti katika Halmashauri 18 ulibaini kuwa kiasi cha Sh.163,361,311,033 kiliidhinihswa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya matumizi ya Mafungu mbalimbali na utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, kiasi cha Sh.130,326,225,146 tu ndicho kilichopokelewa na kubakiza kiasi kisichopokelewa cha Sh.33,035,085,889 sawa na 20% ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, taarifa ya Waziri mwenye dhamana iliyotolewa mbele ya Kamati tarehe 08/06/2012 katika Ukumbi wa Makumbusho, Dar es Salaam, inaonyesha kwamba fedha zilizopokelewa hadi robo ya tatu ni Sh.44,633,161,580 ambazo ni sawa na asilimia 40 ya bajeti ya mwaka 2011/2012. Hali hii imekuwa ikisababisha shughuli nyingi za maendeleo zillizopangwa kwenye Halmashauri zisitekelezwe. Kamati inaiagiza Serikali kutoa ufanuzi kuhusu sababu zilizofanya fedha za bajeti zilizoidhinishwa na Bunge, zisipelekwe kutekeleza shughuli zilizokusudiwa.

(xii) Kamati inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa taarifa yake kwamba Hati zenye Mashaka zimepungua na Hati Safi zimeongezeka. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa 2010/2011, ukurasa wa XV. Hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kwamba pamoja na ongezeko hili bado si kigezo kwamba shughuli zilizokusudiwa zimefanyika vema na hivyo kuelekeza Wakuu wa Wilaya na Mikoa kusimamia vema utekelezaji wa bajeti kwenye maeneo yao. Mifano ambayo imejidhihirisha kuwa na kiwango kikubwa cha ufujaji wa fedha za Serikali ni kwenye ruzuku ya maendeleo kwa shule (*Capitation Grant*), fidia za vijiji na kwenye vyanzo vyatuhafisha mapato ambako fedha nyingi zinakusanywa lakini huishia kwenye Mikono ya wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushukuru wewe, Mheshimiwa Mwenyekiti, *Madam Speaker* kwa kunipa nafasi hii adhimu kuwasilisha maoni ya Kamati. Kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo limeendelea kuwa imara. Hongera sana Mheshimiwa Jenista Mhagama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza, kwa jinsi anavyosimamia na kufuatilia kwa karibu shughuli mbalimbali zinazotekeliza na Wizara zote na pili kuwa msikivu na kuwa tayari kuyashughulikia matatizo ya Kamati za Bunge wakati zilipotekeliza majukumu yake kwa niaba ya Bunge. Vilevile namshukuru kwa mchango wake mkubwa kwa Kamati yangu ya Katiba na Sheria na mawasiliano ya mara

kwa mara wakati wa uchambuzi wa bajeti kutuwezesha kufika hapa tulipo leo. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana. Uongozi wake umesaidia kuweka mambo mbalimbali katika hali iliyo sawa na kulingana na uwezo wa Serikali. Pili, namshukuru kwa ushirikiano wake mkubwa kwa Kamati yangu wakati wa uchambuzi wa bajeti kutuwezesha kufikia hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri na Mheshimiwa Majaliwa K. Majaliwa, Naibu Mawaziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Taasisi, Idara na vitengo pamoja na Maafisa wote, kwa maelezo na ufanuzi wa kina walioutoa kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio haya. Lakini kikubwa zaldi niwashukuru sana kwa busara na hekima walizooonesha na kuwa wavumilivu hasa pale walipopata vitabu kwa muda mfupi. Umahiri na uzoefu wa muda mrefu katika masuala ya sheria, utawala na sekta nyingine mbalimbali ndio uliofanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mwenyekiti,  
Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Makamu Mwenyekiti.  
*(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Abbas Zuberi  
Mtemvu, Mheshimiwa Mohamed S. Mohamed,  
Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa  
Halima J. Mdee, Mheshimiwa Fakharia K. Shomar,  
Mheshimiwa Zahra A. Hamadi, Mheshimiwa Mussa H.  
Kombo, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali,  
Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Azza H.  
Hamad, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay,  
Mheshimiwa Jaddy S. Jaddy, Mheshimiwa Tundu A.  
Mughwai Lissu, Mheshimiwa Deogratias A.  
Ntukamazina, Mheshimiwa Jasson S. Rweikiza,  
Mheshimiwa Rashid Abdalah na Mheshimiwa Dkt. Haji  
Hussein Mponda. Aidha, napenda kuwashukuru kwa  
dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa  
Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa  
kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee,  
nawashukuru Ndugu Peter Magati, Katibu wa Kamati  
hii na Catherine Kitutu, Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu  
vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii  
inakamilika kwa wakati uliopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo,  
sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha  
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri  
Mkuu ambayo sisi Kamati tumeyapitia na  
kuyachambua pamoja na Taasisi zake kama  
yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Bunge letu Tukufu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Pindi Hazara Chana kwa uwasilishaji wako mahiri lakini hasa kwa pongezi nzito ulizonipa hapa Mezani ninaamini zimewafikia wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa sababu ndio wenye heshima hii. Ahsante sana Mheshimiwa Pindi Chana.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nitakupa nafasi ya mwongozo, tunaendelea na ninaomba sasa nimwite msemaji anayefuata, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na yeye aweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati yake. Atakuja Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Kitandula, karibu sana.

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati Bunge ya Fedha na Uchumi, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37 - Uwezeshaji na Uwekezaji kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa vikao vyatubu na Kamati vilivyofanyika Dar es Salaam, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Uendelezaji wa Sekta Binafsi, Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka 2011/12 na Makadirio ya Bajeti 2012/2013. Kamati ilipokea na kujadili kwa kina taarifa hiyo na hatimaye kuishauri Ofisi hiyo ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Serikali ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa sekta binafsi inakuwa mhimili wa uchumi wa Taifa, sambamba na Dira ya Maendeleo ya Taifa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Jitihada za kukuza uwekezaji, kuendeleza sekta binafsi na kuwezesha wananchi kiuchumi, ni masuala muhimu yanayohitaji msukumo wa kipekee kwa Taifa kuwa na uchumi imara. Katika kufanikisha haya, Serikali iliweza kutekeleza yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia maendeleo ya sekta binafsi nchini chini ya uratibu wa Taasisi ya Sekta Binafsi (*TPSF*);
- Kudurusu Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 na Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997;
- Kuweka mfumo thabiti wa kisera, kisheria na kitaasisi kama hatua muhimu ya utekelezaji wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;

- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Azma ya Kilimo Kwanza na Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini (*SAGCOT*);
- Kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji nchini;
- Kuhamasisha na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje nchi kupitia Kituo cha Uwekezaji (*TIC*); na
- Kuratibu na kusimamia programu na mifuko mbalimbali ya uvezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, Ofisi ya Waziri Mkuu inakabiliwa na changamoto kadhaa zifutazo:-

- Kuwepo kwa Sera, Sheria na Mifumo ya Kitaasi inayokinzana na mazingira wezeshi kwa sekta binafsi;
- Fikra potufu kuhusu uwekezaji kuwa lengo lake ni kupora rasilimali za nchi;
- Uhaba mkubwa wa miundombinu ya msingi kama vile maji, umeme, barabara, reli na bandari hali inayoongeza kwa kiasi kikubwa gharama za kufanya biashara na kuwekeza nchini;
- Ufanisi mdogo wa Mahakama katika kutoa hukumu za kesi zinazohusu masuala ya biashara na uwekezaji nchini; na

- Ushindani mkubwa wa upatikanaji wa mitaji kutoka nje kunakosababishwa na kuyumba kwa uchumi na mtikisiko wa fedha Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imeendelea kutoa michango, ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo yamelenga kuimarisha sera na mifumo mizuri ya kufanya biashara, uwekezaji na uvezeshaji wa wananchi wenyewe kipato cha chini ambao utachochaea ukuaji wa uchumi jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kamati inakubaliana na misingi na shabaha ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika utekelezaji wa bajeti kwenye Fungu la 37 ambazo kimsingi zinalenga kutatua changamoto zinazopaswa kuangaliwa na Serikali katika masuala ya uwekezaji na uvezeshaji ambayo kimsingi ndiyo yatakayosaidia katika kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia na kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011. Mwenendo wa Hali ya Uchumi unaonyesha kuwa katika mwaka 2011, pato halisi la Taifa lilikuwa kwa kiwango cha asilimia 6.4 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010 ikiwa ni pungufu ya asilimia 0.6 ya pato la Taifa. Kiwango cha juu cha ukuaji kilikuwa katika shughuli za sekta ya mawasiliano asilimia 19; huduma za fedha asilimia 10.7; ujenzi asilimia 9.0; uzalishaji viwandani asilimia 7.8 na elimu asilimia 7.4. Kwa upande wa sekta ya kilimo kasi ya ukuaji imepungua hadi asilimia 3.6 kutoka asilimia 4.2 kwa mwaka 2010. Aidha, sekta ya

mifugo ilikua kwa asilimia 3.9 kutoka asilimia 3.4 mwaka 2010. Ukuaji wa wastani wa kipato kwa wananchi umeongezeka. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa bado tuna safari ndefu ya kumkomboa mwananchi mwenye kipato cha chini ili aweze kufaidika na Rasilimali ya Taifa. Shughuli za sekta mbalimbali zinazosaidia uwekezaji na uvezeshaji zinazofanyika bado hazijaweza kuwasaidia wananchi walio wengi hasa wa vijiji katika kuwapunguzia makali ya maisha. Hii inatokana na ukweli kwamba shughuli za sekta hizo zinawagusa wananchi wachache tu. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwamba pamoja na nia nzuri iliyonayo ya kuhamasisha uwekezaji na uvezeshaji wa wananchi, msisitizo mkubwa uwekwe kwenye shughuli za sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji ambazo zinaajiri na kutegemewa na Watanzania wengi. Kuimarika kwa sekta hizi kutasaidia kuleta uwiano kati ya ukuaji wa uchumi na kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine linalopaswa kupewa kipaumbele ni lile la Sekta ya Fedha hasa katika kuendeleza upatikanaji wa mikopo na hatua nyingine za uvezeshaji. Pamoja na kuongezeka kwa mikopo inayotolewa kwa sekta binafsi, sehemu kubwa ya mikopo hiyo bado haiwafikii walengwa na hivyo *impact* yake kutoonekana katika kukuza uchumi na hivyo kumwezesha mwananchi wa kawaida. Aidha, mikopo hii ina riba kubwa na hivyo kuwa kikwazo kikubwa katika kumkwamua mwananachi kiuchumi. Kamati inashauri Serikali iwe makini katika kutoa mikopo kwa sekta binafsi, kwa kuhakikisha kuwa inaelekezwa kwenye maeneo ya wananchi wenye kipato cha chini, badala ya kuielekeza kwa

wafanyabiashara wachache. Pia Serikali inashauriwa ifanye tathmini ya fedha za mikopo inayotolewa kuitia mifuko mbalimbali ili kuona kama malengo yaliyokusudiwa yamefikiwa ikiwemo wakopaji kurudisha fedha ili wengine wakope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la uwekezaji mkubwa wa viwanda na biashara katika maeneo mbalimbali nchini. Hali hii inasababishwa na kutokuwa na uhakika wa upatikanaji wa miundombinu bora ya uwekezaji pamoja na umeme wa uhakika kwa kipindi chote cha mwaka. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha mazingira bora uwekezaji yanaendelea kuboreshwa pamoja na kupatikana vyanzo mbadala vya umeme kama vile nishati ya umeme itokanayo na makaa ya mawe, juu, upepo na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu bado inakabiliwa na gharama kubwa za ufanyaji biashara na kuwekeza (*cost of doing business*) ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Ni dhahiri kuwa hatutaweza kuendelea bila ya kuwa na msukumo wa hali ya juu wa kuboresha mazingira ya kufanya wa biashara na kuwekeza ili kuongeza kasi ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Hatua hii lazima iambatane na kuondoa urasimu, ucheleweshaji au kutokutoa maamuzi kwa wakati pamoja na kurekebisha baadhi ya sheria zetu na kuimarisha miundombinu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa, bado idadi kubwa ya Watanzania hawajafaidika na mikakati mbalimbali ya Serikali ya kuwawezesha

kiuchumi. Programu mbalimbali kama vile Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; Mfuko wa Wafanyabiashara Wadogo Wananchi (*NEDF*); Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake; Mfuko wa Rais wa Kusaidia Wananchi; Mfuko wa Uwezeshaji wa Wajasiriamali Wadogo (*SELF*); Mpango wa Udhamini wa Mikopo kwa Mauzo ya Nje (*Export Credit Gurantee Scheme*); Mpango wa Kudhamini Miradi Midogo na ya Kati (*Small and Medium Enterprises Credit Gurantee Scheme – SME-CGS*); Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (*BEST project*) na mingine mingi yenye lengo sahihi la kuwasaidia na kuwawezesha wananchi wengi wenye kipato cha chini bado hazijaweza kuwanufaisha wananchi kwa kuwa utekelezaji wake hausimamiwi ipasavyo hivyo kutowafikia walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, baadhi ya mifuko hii mitaji yake ni midogo kuweza kutosheleza mahitaji ya wananchi na baadhi ya mifuko hiyo inaongozwa na watu wasio na ujuzi wa elimu ya ujasiriamali. Kamati inashauri Serikali kufuatilia suala hili na kuhakikisha malengo ya programu hizo yanafikiwa ikiwemo kusaidia kuongeza mitaji ya mikopo hiyo pamoja na kuhakikisha kuwa inaongozwa na watu wenye ujuzi na uzoefu katika masula ya ujasiriliamali. Kwa mfano, yapo maelewano kati ya Serikali yetu na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuhusiana na *SELF*. Chini ya mkataba huo, pande zote mbili zilikubaliana *SELF* iwe taasisi inayojitegemea, lakini suala hili mpaka sasa halijatekelezwa na kwa maaana hiyo fedha ambazo zinapaswa kupatikana ili kuongeza au kukuza mtaji wa

*SELF* hazijaweza kupatikana. Kamati inaishauri Serikali itekeleze makubaliano yake na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuhusiana na *SELF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa kuhakikisha inasimamia vizuri Sera, Programu na Mifuko mbalimbali iliyoanzisha kwa nia ya kuwajengea uwezo wananchi kushiriki kikamilifu katika uendeshaji, usimamiaji na umiliki wa uchumi. Juhudi hizi zilenge kuinua uwezo wa wananchi kupata mitaji, teknolojia na masoko ili waweze kutumia ipasavyo fursa za uwekezaji zilizopo na hivyo kufanikisha upatikanaji wa maisha bora kwa kila Mtanzania hususan vijijini. Mfano Mkakati wa *Rular Financial Services* umeandaliwa muda mrefu kwa madhumuni ya kuendeleza huduma ya fedha vijijini. Hadi sasa Serikali ipo kimya juu ya suala hili, Kamati inataka kupata maelezo kutoka kwa Serikali kuhusu suala hili. Kamati inaitaka Serikali kutoa taarifa kuhusu jitihada zinazoendelea za kuwawezesha wananchi kiuchumi pamoja na jitihada za Serikali katika kuongeza wataalamu wa mikopo pamoja na kusimamia utoaji wa mikopo hiyo ili iwafikie walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kama ilivyosema kwenye Taarifa yake kuhusiana na bajeti, Serikali iangalie misamaha ya kodi iliyopo sasa na itathmini gharama yake jinsi inavyoshabihiana na Pato la Taifa na iangalie faida na hasara za misamaha hiyo kwenye uchumi. Takwimu zinaonyesha kuwa Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (*TIC*) kinachukua sehemu kubwa ya misamaha ya kodi takribani asilimia 39 ya misamaha yote ya kodi. Kamati inasisitiza kuwa Serikali ifanye utafiti wa kina kuhusu faida na hasara inayopatikana

kwenye misamaha ya kodi inayotolewa kupitia Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (*TIC*). Itathmini kwa madhumuni ya kuona kwamba vivutio vilivyotolewa vimeleta matokeo au manufaa yaliyotarajiwa. Aidha, Kamati inashauri, ni vema kuanzia sasa michango ya wawekezaji kwa jamii (*corporate social responsibility*) ihusishe asilimia fulani ya uwekezaji itakayowekwa na isitegemee hisani ya mwekezaji au faida ambayo mwekezaji amepata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado shughuli za uvuvi hazijapewa kipaumbele. Aidha, Serikali imekuwa ikipanga mipango yake katika sekta hii bila kuitekeleza kwa muda uliopangwa na hivyo kutoweza kufikia azma yake ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Mfano katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2011/2012, katika sekta ya uvuvi, Serikali ilipanga kutekeleza yafuatayo; kutekeleza ahadi ya kuchangia Dola za Kimarekani 600,000 kwa ajiri ya doria maalumu ya Kanda ya Ziwa Victoria; kununua meli mbili za doria kwa ajili usimamizi wa uvuvi katika ukanda wa uchumi wa bahari pamoja na kukarabati meli mbili za utafiti wa uvuvi; kujenga maabara ya uvuvi Kurasini. Kamati inasisitiza mipango hii itekelezwe kama ilivyopangwa ili kuongeza tija katika sekta ya uvuvi. Pia Serikali ibuni programu maalumu za uvuvi kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi wakati anazindua Bunge mwezi Novemba, mwaka 2011 na zinazofanana na *SAGCOT* kwa maeneo ya mito, ziwa na bahari kuu ili kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya uvuvi na hatimaye iweze kuchangia ukuaji wa uchumi na kunufaisha wavuvi katika kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasilitiza umuhimu wa ushiriki wa Serikali katika ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na ushiriki wa sekta binafsi kupitia miradi ya *PPP* katika shughuli za uwekezaji na uvezeshaji wa wananchi kiuchumi. Pamoja na mfumo uliopo sasa wa kubaini fursa za uwekezaji katika ngazi za Mikoa na Wilaya, ni vema sasa Serikali ikatenga fedha ili kuwezesha upembuzi yakinifu kufanyika kuhusu miradi hiyo kwa lengo la kuwezesha ushiriki wa wananchi kupitia Halmashauri zao kwa njia ya ubia na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Bunge liliidhinisha Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2012/2013 ambapo lengo ni kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka ujao wa fedha na hivyo kuendelea kuFungulia fursa za ukuaji wa uchumi. Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – Uvezeshaji na Uwekezaji kuhakikisha kuwa inasimamia ipasavyo miongozo inayotolewa na Tume ya Mipango kwa Ofisi hiyo, ili kuhakikisha inatimiza malengo yake iliyojewekea na kuhakikisha inakuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu inahitajika kutolewa kwa wananchi wengi ili waelewe na kushiriki kikamilifu katika ujasiriamali, uwekaji wa akiba, uwekezaji na kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vyaa ushirika. Kwa kuwa shughuli za VICOBA zimeongezeka kwa kasi kubwa nchini, Kamati inashauri Baraza la Taifa la Uvezeshaji Wananchi kiuchumi lianzishe Kitengo Maalumu (*desk*) kwa ajili ya kuratibu shughuli za VICOBA (*Village Community Banks*). Pia Serikali

ihamasishe uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) na VICOBA kama njia bora ya wananchi kijiwekea akiba na kupata mikopo yenye masharti nafuu, kuongeza kipato, ajira, pamoja na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi; Uwekezaji na Uwezeshaji Dkt. Mary Michael Nagu (MB), Katibu Mkuu, pamoja na wataalamu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mwenyekiti, Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula, Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustas Oseler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa

Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdul Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere Mheshimiwa Amina Amour Abdulla, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Alhaj. Mohamed Hamisi Missanga Mheshimiwa Luaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Subira K. Mgatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37-Uwekezaji na Uwezeshaji, kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kitandula.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuhusu taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

**MWENYEKITI:** Hebu isome hiyo Kanuni inasemaje?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Inasema hivi:-

*"Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusuwi kwa mujibu wa taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatorewa papohapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa."*

**MWENYEKITI:** Tatizo ni nini?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria ambayo tulijadili sio hii iliyosomwa hapa. Kuna maagizo mengi sana ambayo tuliyatoa kwa Serikali

hayapo, wameichakachua, wameleta vitu vingine ambavyo hatukukubaliana kwenye Kamati. (*Makati*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako endapo Kamati imekubaliana kwamba mambo haya yapelekwe Bungeni yakaenda kubadilishwa huko, ni hatua gani kitu chako kinachukua. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, taarifa za Kamati kwa mujibu wa Kanuni zote zinawekwa Mezani asubuhi au siku moja kabla ya shughuli hiyo na taarifa hii ya Kamati imewekwa Mezani leo...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe na nidhamu; tumeelekezwa sana kuwa na nidhamu kwa hiyo ningeomba mnisikilize kabla sijamaliza kufanya *ruling* yangu, nisingependa watu kuingilia katikati.

Ninachotaka kusema ni kwamba taarifa hii imewekwa Mezani na baada ya kuwekwa Mezani Kamati husika ndio yenyewe wajibu wao wenyewe kuona taarifa hiyo iko kamilifu na kama haiko kamilifu. Kwa hali hiyo, taarifa hii sisi tumeipokea kama taarifa rasmi ya Kamati na kama Kamati hiyo hairidhiki na hiki kilichowekwa, haikatazwi kurejea tena huko kwenye Kamati yao na kwenda kujadiliana na kujua kama kuna kitu kilipungua ama kuna kitu kiliongezeka lakini sisi sasa hivi tunaichukua taarifa hii kwa sababu ilishawekwa Mezani kama ni taarifa rasmi na tutaendelea nayo na kazi. Kwa hiyo, Wajumbe wa

Kamati hiyo mnayo nafasi ya kukutana kwenye Kamati yenu na kuweza kujadili suala hili kwa uwazi na kwa muda zaidi. Huo ndiyo mwongozo wangu vinginevyo hatuwezi sasa hivi kuanza tena kujadiliana hapa kilichopo na sio kazi ya Bunge zima kuanza hapa kujadili Kifungu kimoja na kingine kama ni sahihi au sio sahihi. Kwa hiyo, ninyi mtajadiliana zaidi kile kilichoijiri na tuna muda wa wiki nzima. Kwa hiyo, hii sio kazi ya Bunge hili kujadili hiki ni kweli ama sio kweli.

Naomba sasa tuendelee na Msemaji wa Kambi ya Upinzani na kwa maelezo niliyoyapata kutoka Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, wao wana saa moja ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani lakini ameniomba msemaji atakayewasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI atatumia dakika kumi na tano na dakika zilizobaki zitatumwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kuwasilisha maoni hayo.

## TAARIFA

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, sasa nitamwomba Mheshimiwa Silinde atumie dakika kumi na tano na baada ya hapo tutaendelea na Mheshimiwa Mbewe. Naomba tuendelee.

**MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge hili ili kutoa

maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, kuhusu Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kanuni ya 99(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kwa imani yake kwangu na hivyo kunateua kuwa Msemaji Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Nami nitajitahidi kwa kadri niwezavyo kuhakikisha kuwa ninafanya kazi zangu za ndani na nje ya Bunge ili kukidhi matarajio ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa kazi kubwa inayofanywa na Katibu wetu Mkuu, Dkt. Wilbrod Slaa, ya kuhakikisha kuwa wananchi wanaelewa nguvu yao katika kusimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 8 (1) (a)-(c) inayosema kuwa:-

*"Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii".* Aidha, niwashukuru viongozi wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Upinzani kwa ushirikiano katika kutekelezaji wa majukumu yetu ya msingi ya kusimamia utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uwepo wangu hapa Bungeni ni kwa ajili ya mchango mkubwa wa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) pamoja na wananchi wa Jimbo langu la

Uchaguzi la Mbozi Magharibi, natoa shukrani na ninaomba tuendelee kuwa na ushirikiano kwani sasa hivi ndio kipindi kinachohitaji utulivu na mshikamano mkubwa katika kujenga Jimbo letu. Nguvu ya Umma mara zote ndiyo inayoshinda hata kama kutakuwepo na ghiliba na udanganyifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa familia yangu na ninawaambia nipo pamoja nao kwa sala na maombi na Mwenyezi Mungu atawalinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kuangalia baadhi ya masuala kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Dhana ya Maendeleo Vijijini na Utekelezaji wake. Mojawapo ya majukumu ya Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ni kusimamia Sera ya Maendeleo Vijijini. Suala la Maendeleo Vijijini, ni jambo ambalo Kambi ya upinzani tumelipa kipaumbele na ndio maana katika hotuba yetu ya Bajeti Kivuli ya Uchumi na Fedha tumesitisiza sana suala la kukuza uchumi vijijini kwa kuzingatia ukweli kwamba maendeleo vijijini ndio msingi wa uchumi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) ya 2008 juu ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia, nchi ya Tanzania iko nje kabisa ya mstari wa kuwapunguzia wananchi umaskini wa kipato na chakula. Tafsiri ya

taarifa hii ni kwamba Serikali ya Awamu ya Nne imeshindwa kuwekeza katika maeneo ya vijijini hususani katika kilimo, miundombinu, nishati na maji. Kushindwa kwa Serikali kuwekeza katika sekta hizo muhimu, ndio chanzo cha wananchi wa vijijini kuendelea kuwa maskini. Kambi ya Upinzani, inaendelea kusisitiza pendekezo lake la kuanzishwa kwa Mamlaka ya Maendeleo Vijijini ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia, kuondoa umaskini na kukuza maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango na maendeleo. Kama Taifa ni lazima tukubali kuwa tuna udhaifu mkubwa katika mipango yetu na udhaifu huu kwa kiasi kikubwa unatokana na kushindwa kuzingatia uhalisia wa matatizo na fursa zilizopo katika ngazi zote nchini. Hali hii inapelekea upangaji wa mipango ya kitaifa katika ngazi za juu kutowiana na hali halisi ya maisha ya wananchi, ilihali taarifa za hali ya uchumi nchini zinaonyesha uchumi kukua zaidi ya asilimia sita (6) kila mwaka wakati hali halisi ilivyo kwa Watanzania waishio vijijini ni duni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu ina Programu ya Kujenga Uwezo wa Upangaji wa Mipango ambayo imekuwa ikitengewa fedha nyingi kwa mfano katika Kasma namba 6281 imetengewa jumla ya Tshs.327,096,000/- kwa mwaka wa fedha 2012/2013, wakati mwaka 2011/2012 ilitengewa Tshs 640,000,000/- na mwaka 2010/2011 zilitengwa Tshs. 603,052,760/-. Kwa ujumla fedha hizo ni nyingi sana lakini utumikaji wake haujaongeza ufanisi dhahiri katika mipango ya maendeleo. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa

matumizi ya fedha hizo yawekwe wazi kwa Watanzania wote ili tija ya kujenga uwezo na upangaji wa mipango iweze kudhihirika kwa umma. Vilevile Serikali iweke mkazo katika kutumia rasilimali watu kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijiji. Kambi ya Upinzani inaendelea kusisitiza matumizi ya asasi za kiraia kuisimamia Serikali na kuiwajibisha kwa jamii kwa kutumia Mfumo wa Ufuatiliaji na Uwajibikajikwa Jamii (*Social Accountability Monitoring System- SAMS*) na Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma (*Public Expenditure Tracking System-Pets*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, chaguzi za Serikali za Mitaa. Tangu chaguzi za Serikali za Mitaa kufanyika mwaka 2009, sasa hivi kuna maeneo mengi yamebaki bila viongozi kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo viro, kujiuzulu kwa uongozi, viongozi kufukuzwa/kukataliwa na wananchi kutokana na tuhuma na kashfa mbalimbali na kadhalika. Hali hii inaonyesha kuwa Wizara ya TAMISEMI haiko makini na haiko tayari kuzihimiza Halmashauri kuitisha chaguzi katika Vijiji/Vitongoji/Mtaa. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni ama Serikali haijali maendeleo ya watu wake wa chini au inaogopa kushindwa katika chaguzi ndogo, hususanii maeneo ambayo Vyama vyia Upinzani vina nguvu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na vurugu nyingi kwenye maeneo mengi zinazosababishwa na Serikali na vyombo vyake vyia dola kukiuka kwa makusudi taratibu, kanuni na sheria zinazoendesha chaguzi katika baadhi ya Mitaa/Vijiji/Vitongoji wakati wa uchaguzi wa viongozi

wa Serikali ya Mitaa/Vijiji/vitongoji. Kwa mfano, kwa mujibu wa taarifa ya uchaguzi wa Mji Mdogo wa Kichangani-Turiani, Wilaya ya Mvomero ambapo wananchi walitumia mamlaka waliyopewa na sheria kuiondoa madarakani Serikali yao kutokana na kutokujibika, kwa sababu zisizojulikana Mkurugenzi ameendelea kuitambua Serikali haramu na kuipatia ushirikiano Serikali isiyo na uhalali wa kisheria. (Rejea barua ya wananchi wakazi wa Mji Mdogo wa Kichangani kwa Waziri wa TAMISEMI ya tarehe 16.08.2011). Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia TAMISEMI kuamrisha Halmashauri zote ziitishe chaguzi za Mitaa/Vijiji/Vitongoji mara moja kujaza nafasi mbalimbali nchini zilizo wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji kwa fedha za Halmashauri. Pamoja na Kambi ya Upinzani kutokubaliana na mfumo wa sasa wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, bado tuna jukumu la kuangalia na kutolea kauli uwajibikaji katika matumizi ya fedha katika Halmashauri zetu. Pamoja na kwamba fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya shughuli za maendeleo ni chache lakini bado kuna ubadhirifu na ujisadi mkubwa sana wa fedha hizo katika ngazi ya Halmashauri. Kwa mfano, kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2011, kiasi cha Shilingi 46,488,103,680.26 zimetumika vibaya tofauti na malengo yaliyokusudiwa katika sekretarieti za Mikoa. Matumizi haya yasiyo na taarifa za kuaminika, ni ubadhirifu wa fedha za umma na ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya Mikoa na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mkaguzi Mkuu inaonyesha fedha nyingi zilitumika bila vielelezo na mchanganuo wa matumizi, hali inayoashiria wizi na udanganyifu mkubwa wa fedha za umma. Kama ilivyoinishwa tena katika Ripoti ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 2011, jumla ya Halmashauri zilizopata hati yenye shaka ni 56 sawa na asilimia 42 ya Halmashauri zote 133 zilizokaguliwa, wakati zilizopata hati isiyoridhisha ni tano (5) sawa na asilimia nne (4%) ya Halimashauri zote 133 zilizokaguliwa. Ukijumlisha asilimia 42 ya hati zenye shaka na asilimia nne (4%) ya hati zisizoridhisha unapata jumla ya asilimia 46 ya hati zenye matatizo. Hii ina maana kwamba karibu nusu ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya gharama za uendeshaji na maendeleo ya Halmashari zetu hazitumiki kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni tatizo, ni kutotilia mkazo katika miradi ya maendeleo na badala yake kuweka kipaumbele katika matumizi ya kawaida. Kwa mfano, Ripoti ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa iliyowasilishwa Bungeni tarehe 17 Aprili, 2012, jumla ya shilingi bilioni 2,274.1578 zilitengwa na Serikali Kuu kama ruzuku ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa Halmashauri zote 133 nchini. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 1,617.27 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida wakati shilingi billioni 656.887 zilikuwa ni kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu wa kutenga pesa nyingi kwa ajili ya matumizi ya kawaida na chache kwa ajili ya maendeleo, Kambi ya Upinzani inaungana na maoni ya Kamati ya Bunge ya Hesabu

za Serikali za Mitaa kwamba ni vigumu sana kuona maendeleo ya uhakika katika Halmashauri zetu. Hali hii inafanywa kuwa mbaya zaidi na utovu wa uwajibikaji wa watendaji na wataalamu wengi wa Halmashauri; ndio maana hoja yetu kama Kambi ya Upinzani ni kubadili kabisa mfumo wa utawala wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari nyingi zilizobainika katika Ripoti zote mbili yaani Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ile ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, pamoja na kelele nyingi zilizopigwa na wadau mbalimbali vimepelekea Serikali kuchukua hatua za kinidhamu kwa baadhi ya watendaji. Hata hivyo hatua hizi hazitoshi. Kwa mujibu wa Ripoti ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ni kwamba wahusika wa ubadhirifu katika Halmashauri wamekuwa wakihamishwa vituo vyta kazi badala ya kushtakiwa, huu ni udhaifu mkubwa wa Serikali. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali isifanye mzaha na fedha za umma. Kitendo cha kutochukua hatua kali na za wazi dhidi ya watendaji wote wabahirifu, ni kufanya mzaha na fedha za umma, jambo ambalo halivumiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za maendeleo ngazi ya Halmashauri. Kwanza, miradi mingi ya maendeleo inayoibuliwa na wananchi katika Halmashauri nyingi nchini ama haikamiliki kwa wakati au haikamiliki kabisa kutokana na ukosefu na/au ucheleweshaji wa fedha toka Serikali Kuu. Pili, miradi mingi inatekelezwa chini ya viwango, kwa mfano Halmashauri/ mamlaka husika kutofanya uchambuzi

wa kina ili kutambua wakandarasi husika kama wana uwezo wa kutekeleza miradi waliyoomba na kwa wakati. Tatu, ushiriki mdogo wa wananchi katika kuibua vipaumbele vyao. Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kufanya kazi maeneo haya kwa kuzingatia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa uongozi katika Halmashauri zetu. Ni ukweli ulio wazi kuwa Madiwani wanahitaji kujengewa uwezo zaidi ili waweze kusimamia vema uendeshaji wa Halmashauri kwa ujumla. Hii inatokana na ukweli kuwa miradi mingi ya maendeleo inatekelezwa na ngazi ya Kata kwani inaibuliwa huko na kusimamiwa na Kamati za Maendeleo ya Kata (*WDC*). Ifahamike kuwa tukiwajengea uwezo kutawasaidia kusimamia miradi kuwa na ubora zaidi na hivyo kasi ya maendeleo kuweza kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Madiwani wana majukumu mengi kwenye ofisi zao na ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi, Kambi ya Upinzani inaona ni wakati muafaka sasa wakaanza kulipwa mishahara ya kutosha. Tunapendekeza waanzie na shilingi 350,000 kwa mwezi badala ya posho ya sasa ya shilingi 120,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu katika Serikali za Mitaa na Vijiji. Serikali za Mitaa na Vijiji zimekuwa hazisomi taarifa za mapato na matumizi kwa wananchi. Hii inatokana na mazoea yaliyopo ya ujisadi na matumizi mabaya ya michango ya wananchi. Aidha, Kamati za Kijamii zinazoundwa ili kutekeleza miradi mbalimbali mfano *TASAF*, *PADEP* na kadhalika

imekuwa ikitekelezwa kwa kuchelewa ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji wa fedha toka Serikalini. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutoa tamko juu ya Serikali za Mitaa na Vijiji ambavyo vimekuwa na utamaduni wa kutokusoma taarifa za mapato na matumizi kwa wananchi kwa mujibu wa sheria, ikizingatia kuwa sheria na taratibu zipo lakini kwa muda mrefu sasa hazifuatwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya Halmashauri. Halmashauri nyingi ni tegemezi kwa Serikali Kuu kwa kuwa vyanzo vingi vikuu vya mapato vimechukuliwa na Serikali Kuu huku vyanzo ambavyo mapato yake kwa mwaka siyo imara ndivyo vimeachwa katika Halmashauri. Hali hii imepelekea Halmashauri nyingi kubuni vyanzo mbadala vya mapato ambavyo vimekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi kama vile ushuru wa mazao, mifugo, masoko na kadhalika. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuangalia upya suala hili kwani linawafanya wananchi wengi kuendelea kuwa maskini kutozwa na kutozwa kodi nyingi. Tunaitaka Serikali kutoa tamko kuhusiana na ushuru wa mazao ambao wananchi maskini wanatozwa katika kufikisha mazao na bidhaa mbalimbali sokoni. Pia ni wakati muafaka sasa kwa Halmashauri zetu kuweza kushindanishwa katika utoaji wa huduma bora na viwango vya kuchangia maendeleo. Ushindani huu utazihamasisha Halmashauri kuongeza juhudi na ubunifu katika uibuzi na usimamizi wa vyanzo vipyta vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Msingi na Sekondari. Sekta ya elimu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo imekuwa ikitengewa asilimia 15 ya bajeti,

ambayo ni karibu na wastani wa bajeti katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ambayo ni asilimia 20. Hata hivyo, ubora wa elimu kwa miaka mitatu mfululizo umekuwa ni wa chini kabisa ukilinganisha na nchi jirani. Hii inadhihirishwa na ukweli kwamba zaidi ya asilimia 90 ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne wana madaraja ya nne na sifuri na hivyo hawana sifa ya kuendelea na masomo ya juu. La kutisha zaidi ni kwamba baadhi ya wale wanaomaliza elimu ya msingi wamekuwa wakifaulu wakati hawajui kusoma wala kuandika na huu ni muujiza mwingine kwenye elimu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizo, ni dhahiri kuwa sekta ya elimu kwa ujumla wake ina matatizo mengine zaidi ya ukosefu wa bajeti ya uendeshaji. Kambi ya Upinzani inaona kuwa tatizo kubwa linalosababisha sekta hii kufanya vibaya ni ukweli kuwa inakosa usimamizi ulio madhubuti toka TAMISEMI. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutumia utaratibu utakaohakikisha kuwa wanafunzi wa sekondari wanaofaulu kwa daraja la kwanza hadi la tatu kuijunga moja kwa moja kwenye kozi ya Ualimu, ikiwemo kusoma bure. Mfumo huu ndio unaotumika katika nchi za Botswana na Ujeruman. Lakini ili kufikia hapo ni lazima maslahi ya Walimu yawe mazuri zaidi ili kutoa motisha zaidi kwa wanafunzi wengi wanaofaulu kuijunga na fani hii. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kiwango cha mishahara ya kima cha chini wanachopendekeza Walimu kinawezekana, hivyo tunaiomba Serikali ifanyie kazi mapendelezo yao kwa mustakabali wa ubora wa elimu yetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Kutokana na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) mwaka 2002, Sekta ya elimu imekuwa ikitengewa rasilimali nyingi, zaidi ya Shilingi bilioni 80 zilitengwa mwaka 2009/2010 kwa ajili ya ruzuku, pamoja na kuwa Sera iliyopitishwa awali ya ugawaji wa ruzuku kwa wanafunzi ya Dola 10 za Kimarekani kwa kila mwanafunzi haikuwahi kufuatwa na kutekelezwa kikamilifu. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulipa fedha hizo moja kwa moja katika akaunti za shule ili ziweze kusaidia uendeshaji shulenii tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo ya Sekondari (MMES). Kama ilivyo katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi, Serikali imeendelea kushindwa kupeleka fedha za ruzuku katika elimu ya sekondari kama ilivyopitishwa kwa mwanafunzi mmoja kulipiwa shilingi 25,000. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulipa fedha hizo moja kwa moja shulenii kama tulivyoainisha katika MMEM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka Serikali kuweka mazingira linganifu katika stahiki za kazi ili kuboresha maslahi ya Walimu. Hili litasaidia kufuta mtazamo wa kuwa Ualimu ni chaguo la mwisho kutokana na stahiki ndogo na mazingira mabovu ya kazi ikilinganishwa na kada zingine. Tunaendelea kushauri kuboresha mazingira ya kazi kwa Walimu ili kuvutia na kutoa motisha kwa wanafunzi kuingia katika fani ya Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya fedha za kujikimu Walimu wapya. Katika hotuba ya bajeti kuu ya Waziri wa Fedha ameainisha idadi ya Walimu wapya walioajiriwa mwaka 2011 ikiwa ni Walimu wa Shule za Sekondari na Msingi 25,000 pia katika randama ya ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - Fungu la 56 iliyowalishwa kwenye Kamati katika kipindi cha mwaka 2011, nanukuu:-

*“...ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliwapangia vituo Walimu 11,243...”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha Serikali kutojua idadi ya Walimu walioajiriwa kwa mwaka 2011. Pamoja na Serikali kuajiri Walimu wapya walioripoti kwenye vituo vyao vya kazi kuanzia Februari 2 hadi 14, limejitokeza tatizo la Walimu hawa kutolipwa stahiki zao kama fedha za kujikimu baada ya kuripoti vituoni kama ilivyoagizwa na Wizara. Mpaka sasa Serikali imeshindwa kulipa stahiki hizi katika baadhi ya Halmashauri, mfano Halmashauri ya Mbinga, Mbozi na Rungwe baadhi ya Walimu hawajalipwa, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kushughulikia malipo haya kwa haraka, ikizingatiwa kuwa Walimu hawa wapo katika mazingira mapya ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu. Suala la malipo ya madai ya Walimu bado taarifa zake zina mkanganyiko kutokana na taarifa ya hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha 2012/2013, ukurasa wa 22, aya ya 4, naukuu:-

*"... Serikali ililipa kiasi cha shilingi bilioni 44.0 za madai ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari yaliyohakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani..."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini taarifa iliyomo kwenye randama ya matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu la 56, ukurasa wa 12, inasema:-

*"...jumla ya malipo yote kuwa shilingi bilioni 19.2...."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi mbili zina utata mkubwa na hivyo tunaitaka Serikali itoe ufanuzi wa malipo ya madai haya ya Walimu kuwa ni kiasi gani cha fedha kililipwa na walilipwa Walimu wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Rada. Taarifa za Serikali zinazeleza kuwa fedha za Rada zilizokuwa zimeporwa na Kampuni ya *BAE Systems* ya Uingereza inayotengeneza na kuuza vifaa vya Kijeshi ilirejesha Tshs. 72.3 bilioni ili zitumike katika sekta ya elimu. Katika Kauli ya Serikali iliyotolewa Bungeni na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alisema, nanukuu:-

*"...Serikali ya Uingereza na Serikali yetu zilijadiliana na kukubaliana kuwa ni vyema fedha hizi za wananchi wa Tanzania zikarejeshwa kupitia Serikali ya Tanzania. Serikali hizi mbili zilikubaliana kuwa fedha hiso zitumike kwenye Sekta ya Elimu. Mpango huo ulikuwa moja ya ushahidi muhimu uliotolewa Mahakamani kumshawishi Jaji kutoa uamuzi wa kuridhia makubaliano kati ya SFO na BAE ... kununua vitabu 4.4 milioni kwa ajili ya*

*wanafunzi, vitabu 192,000 Kwa ajili ya Walimu kufundishia, madawati 200,000, kujenga nyumba 1,196 za Walimu wa Shule za Msingi vijijiini, kujenga vyoo 200,000 kwenye shule za msingi".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa ni kwamba, Serikali yetu imekiuka makubaliano waliyofikiwa na hii ni sawa na kusema kuwa lengo lilikuwa ni kumdanganya Jaji ili fedha hizo zirejeshwe Serikalini na haswa ikizingatiwa kuwa Kambi ya Upinzani, wananchi na wadau mbalimbali walipinga suala hilo la fedha kurejeshwa kupitia Serikalini, kwani tulijua kwa uhakika kuwa hazitatumika kwa malengo tarajiwa kama ambavyo sasa inajirihidhisha waziwazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 31.01.2012, wakati Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Majaliwa akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha Mlata kuhusu pesa za Rada alisema, nanukuu:-

*"Mheshimiwa Spika, ni kweli kwenye utaratibu wa bio-Systems, fedha ambazo Mheshimiwa Mlata ametaka kujua, katika fedha zile tumetengewa shilingi 18,400,015,000 ambazo pia zitaingla katika Mpango wa Utengenezaji wa Madawati kwa Shule za Msingi na ndiyo hasa uliopewa kipaumbele".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuipatia nguvu kiutendaji Mamlaka ya Elimu Tanzania sambamba na kuipatia fedha zote za kununulia vitabu vya wanafunzi pamoja na vitabu vya kufundishia ili itekeleze mpango huu kwa mujibu wa

mchanganuo uliotolewa katika taarifa ya Serikali hapa Bungeni. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuipatia JKT fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu vijijini, mradi wa madawati wapewe wajasiriamali wa ndani na sio kuagiza kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizopo ni kwamba zabuni ya kuchapa vitabu imetolewa kwa Kampuni ya Kiingereza ya *Oxford University Press*, kwa maana hiyo fedha zote hizi kwa kiwango cha thamani ya vitabu zitarudi Uingereza. Tunataka vitabu vitengenezwe na wachapaji wa Vitabu wa ndani na sio Waingereza. Tunataka fedha hizi zibakie kwenye uchumi wa ndani kwa kiasi kikubwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.  
*(Makofii)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge namshukuru Mheshimiwa Silinde kwa mchango wake, kabla sijamwita Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, ninaomba niwataje wachangiaji wa mwanzo ili kusudi kama

wapo maeneo mengine nje ya ukumbi huu wa Bunge waweze kijiandaa.

Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Michael Laizer atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Karogeres, Mheshimiwa Anne Killango Malecela, Mchungaji Luckson Mwanjale na Mheshimiwa Kuruthumu Mchuchuli. Kwa hiyo, ningeomba hao niliowataja kama wapo nje ya ukumbi au ndani ya ukumbi basi waelewe utaratibu huu wa kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge baada ya Mheshimiwa Silinde kutumia dakika kumi na tano, sasa nitamwita Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, atatumia dakika zilizobaki kwa maana ya kutimiza saa moja ya hotuba ya Kambi ya Upinzani.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nikitambua na kuamini kuwa "Nyumba asiyoilinda Mwenyezi Mungu, wote wailindao wafanya kazi bure," naomba kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, ulinzi na nguvu na hivyo kuniwezesha kusimama hapa kwa mara nyingine tena kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu mapitio ya kazi za Serikali katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kanuni ya 96(6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wangu kutoa shukrani kwa Wabunge wenzangu wa Upinzani kwa ushirikiano wao na kwa niaba yao wote nawiwa kutoa shukrani kwa Viongozi wenzetu walio nje ya Bunge, Makamanda, wanachama, wepenzi na waumini wote wa mageuzi nchini. Tunawashukuru kwa namna wanavyotutia moyo kwa njia mbalimbali. Tunawaahidi kuwa tutaendelea kuwawakilisha ndani ya Bunge hili kwa unyenyekevu mkubwa, kwa nguvu za hoja ili hatimaye nchi yetu ipate neema aliyokusudia Mwenyezi Mungu juu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii vilevile kuwapongeza wale wote waliopewa dhamana ya kuwa Mawaziri kufuatia mabadiliko ya Baraza la Mawaziri. Ni imani yangu watakuwa wa baraka kwa nchi yetu na kamwe hawatakuwa wa laana. Nawaomba watambue kuwa Kambi ya Upinzani ina nia njema na kila Mtanzania bila kujali itikadi yake na kwa maana hiyo watayapokea kwa dhamira njema yale yote tutakayoshauri kupitia hotuba hii na nyingine zote tutakazowasilisha rasmi kwa kila Wizara na hata Wabunge wengine wote wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzito mkubwa sana, nawashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Hai, nawaahidi kuendelea kuwatumikia wao na nchi yetu yote kwa uadilifu mkubwa. Mwisho lakini kwa uzito wa kipekee, naishukuru sana familia yangu hususan mke wangu Dkt. Lillian na watoto wetu Denis, Nicole na Dudley. Mungu atawalipa kwa kumkosa Baba kwa muda mrefu. Mbarikiwe sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara, Gazeti la Serikali Na. 494 kama lililochapishwa tarehe 17/12/2010 kuhusu Wizara zilizoundwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na Gazeti la Serikali Na. 494A kuhusu majukumu ya kila Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2011/12. Taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa zaidi ya miaka mitatu sasa, zimeendelea kuonyesha upungufu mkubwa juu ya mipango, matumizi na taarifa za utekelezaji mipango hiyo katika ngazi zote za Serikali na Idara zake, zikiwemo Serikali za Mitaa. Ni lazima hali hii itafutiwe mbinu ya kukidhi haja na idhibitiwe ipasavyo. Tatizo kubwa ni kwamba mapendekezo ya *CAG* yamekuwa hayatekelezwi na Serikali au yatekelezwe kwa kiwango kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia randama ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37, mwaka wa fedha 2011/2012, tunaona kuwa Bunge liliidhinisha jumla ya Shillingi 109, 404,476,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Fungu husika. Lakini hadi Aprili mwaka 2012, Fungu hilo lilipokea jumla ya Tshs. Bilioni 15,351,640,429.12 ambazo ni sawa na asilimia 14.03 ya bajeti iliyopangwa. Mwaka huu wa fedha, kwa Fungu hilo linaomba Tshs.bilioni 108,271,972,000. Kambi ya Upinzani inahoji, ni kwa kiasi gani maombi haya yanawiana na utekelezaji wa mipango yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ilipanga shilingi 134,375,960,000/- kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Fungu ya 27 (Vyama vya Siasa) Fungu 37 (Ofisi ya Waziri Mkuu), Fungu 42 (Mfuko wa Bunge), Fungu 91 (Tume ya Kuratibu Dawa za Kulevyta) na Fungu 92 (Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania). Hata hivyo, hadi Aprili 2012 na Tshs. Bilioni 24,301,571,108 zilikuwa zimetolewa na zilizotumika ni Tshs. 19,689,920,292.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Randama ya Taarifa ya Waziri wa Nchi Sera, Uratibu na Bunge, ukurasa wa 9, nanukuu:-

*"Jedwali Na. 3 linaonyesha mchanganuo wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo hadi Aprili, 2011".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia jedwali tajwa hapo juu, tunaona kuwa badala ya kuonyesha miradi ya maendeleo kwa 2011/2012 linaonyesha mgawanyo wa fedha kwa Mafungu tajwa. Aidha, taarifa ya utekelezaji wa miradi kwa Fungu 37, ukurasa wa 10-12 wa randama ya Waziri wa Nchi, haionyeshi mchanganuo wa fedha kwa kila mradi, jambo ambalo linatia shaka kwa matumizi au kuwepo wa miradi husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo ingekuwa mfano wa kuigwa katika uwazi wa utekelezwaji wa miradi, ili wananchi waone thamani ya fedha kwa miradi husika, lakini kwa mujibu wa randama hiyo imekuwa ni kinyume. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani

inaitaka Serikali kuweka wazi gharama za utekelezaji kwa kila mradi kama miradi ilivyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona hapa kuna tatizo kubwa sana, kwani katika bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa Mafungu tajwa hapo juu, fedha zilizotolewa hadi April, 2012 ni asilimia 18.08 tu. Je, ni kweli kuwa Serikali itaweza kutoa asilimia 81.92 zilizobaki kwa miezi iliyobaki toka April hadi Juni (mwezi unaokaribia kuisha) ili kutekeleza miradi iliyokuwa imepangwa? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kuhusu shughuli za maendeleo zilizoathirika na ucheleweshwaji huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza ni kwamba katika mwaka huu wa fedha, zimeombwa jumla ya Tshs 109,906,972,000/- kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kama mwaka uliopita zilitengwa Tshs Bilioni 134,375,960,000/- kwa miezi tisa (9) wakatapa asilimia 18.08, ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wanapoteza muda kuitisha Mafungu hapa lakini utekelezaji haufikii hata asilimia 20. Hii inaonyesha kuwa bajeti inayopitishwa siyo halisi, kama Mafungu hayo yameweza kuishia asilimia 18 ya maombi yake, hakuna haja ya kumpa fedha kulingana na maombi yake. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itoe ufanuzi wa kina na mchanganuo wa matumizi katika miradi yote hasa kwa Fungu la 37 ili Mafungu hayo kwa Waziri Mkuu yaweze kuidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora na demokrasia. Ni dhahiri kuwa sasa nchi yetu imeamua

kuendelea na utamaduni wa kutokuheshimu misingi ya utawala bora na demokrasia ya mfumo wa vyama vingi. Jambo hili linakuwa la hatari zaidi kama Ofisi ya Waziri Mkuu ndio inaongoza kwa kutoa maelekezo na miongozo ya kukiuka misingi ya utawala bora na demokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo kimsingi Msajili wa Vyama vyaa Siasa anawajibika kwayo moja kwa moja, inapoamua kusimamisha chaguzi za Kiserikali kwa kuwa eti CCM inaendesha uchaguzi wake wa ndani, ni jambo ambalo halipaswi kufumbiwa macho hata kidogo. Hili ni sehemu ya uthibitisho wa madai yetu ya muda mrefu kuwa vyombo vyaa kusimamia chaguzi havipo huru na huwa vinakipendelea Chama cha Mapinduzi (CCM) kutokana na maelekezo wanayopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu sehemu ya barua ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Ndugu B.B Kichinda, ya tarehe 23 Mei 2012 Kumb. Na FA.291/300/08/25 kwenda kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na nakala zake kusambazwa kwa Wakuu wote wa Wilaya za Mkoa wa Mara iliyokuwa na kichwa kisemacho:-

*"Yah: Kusimamisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua inasema hivi:-

*"Nyote mnataarifiwa kuwa kutokana na mwingiliano wa uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi*

*katika ngazi mbalimbali na ule wa Serikali za Mitaa, mnatakiwa kusimamisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kupisha uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa nafasi zilizo wazi ufanyike mara baada ya uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi” (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa barua hii, ni dhahiri kuwa Katibu huyu amepewa maagizo kutoka ngazi ya juu na kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na.51 la tarehe 17 Disemba 2010, mwenye dhamana ya kutoa maelekezo hayo ni Waziri Mkuu kwani ndio Msimamizi Mkuu wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua hii ilifuatiwa na agizo la Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri mbalimbali za Wilaya za Mkoa wa Mara na kusimamisha chaguzi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri Mkuu; moja, kutoa kauli ya Serikali juu ya kusimamishwa kwa chaguzi zinazojitokeza za Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji ili kupisha uchaguzi wa CCM. Pili, ni lini chaguzi hizo zitafanyika, kwani nchi nzima zimesimamishwa? Tatu, Waziri Mkuu anachukua hatua gani kutokana na jambo hili ambalo ni kinyume cha Katiba, sheria na misingi ya utawala bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sherehe za Kitaifa. Nchi yetu ina matukio mengi ya kihistoria, pamoja na matukio mengine ya kimataifa, ambayo kutokana na unyeti wake, imepelekea kila mwaka matukio hayo kuadhimishwa kitaifa. Maadhimisho hayo yanahuisha

kusherehekea kumbukumbu za Tanganyika kupata Uhuru wake, maadhimisho ya siku ya Muungano, maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei mosi), maadhimisho ya Sabasaba, maadhimisho ya Nanenane, maadhimisho ya Sikukuu ya Mashujaa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadhimisho hayo yote hufanyika kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Wilaya kwa kufanya sherehe mbalimbali zinazohusisha viongozi wa Kiserikali na hivyo ni dhahiri matumizi ya kodi za wananchi hutumika. Kambi ya Upinzani inasema kuwa matukio hayo ya kihistoria ni muhimu yaeleweke kwa vizazi vyetu vya sasa na vijavyo. Katika kufikia azma hiyo, si lazima tutumie fedha nyingi za walipa kodi wakati Serikali inashindwa kutimiza wajibu wake muhimu zaidi wa kutoa huduma za msingi kwa wananchi wake, kama vile huduma ya maji safi na salama, elimu bora kuanzia ngazi ya msingi hadi elimu ya juu, kupeleka nishati kwenye maeneo ya uzalishaji na kwa Watanzania waishio vijijini na kadhalika. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali badala ya kufanya maadhimisho ya Sherehe hizo zote, tuchague ni sherehe zipi zinatoa tija kwa Watanzania na zipi hazileti tija na maadhimisho yake yafanyike kila baada ya miaka miwili au mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyandoikwa na Ndungu Mkinga Mkinga na kutolewa na "Gazeti la *The Citizen*" linalochapwa na Kampuni ya Mwananchi *Communication* ya Jijini Dar es Salaam, zilidai kwamba mwaka jana Serikali ilitumia kiasi cha shilingi bilioni 64 kwa ajili maadhimisho

ya sherehe za uhuru. Tangu kumalizika kwa sherehe hizo, Serikali hajapinga taarifa hiyo na hajatoa taarifa rasmi kwa umma kuhusu matumizi hayo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tamko kuhusu matumizi hayo pamoja na mchanganuo wake ili kutekeleza dhana nzima ya uwazi na ukweli, ambayo ni msingi muhimu wa utawala bora. Ni vyema vilevile taarifa za gharama za sherehe hizi za Kitaifa zikawekwa hadharani, zikiwemo gharama za mbio za mwenge ili umma wa Watanzania waweze kuchambua na kuona kama kweli bado ni tija na kipaumbele kwa Taifa kuendeleza sherehe hizi kwa mfumo tulio nao leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge kama mhimili wa Kuisimamia na kuishauri Serikali. Mamlaka ya Bunge yameainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara za 62 hadi 64 lakini kwa kufanya kazi ya kuisimamia na kuishauri Serikali Ibara ya 63(2). Hili ni jukumu kubwa sana ambalo linahitaji kuwa na raslimali na umakini katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inauliza ni kwa vipi Bunge linaweza kuisimamia na kuishauri Serikali wakati Bunge (Wabunge) halina taarifa za kutosheleza kuhusiana na utendaji wa Serikali? Ni mara nyingi Bunge limedai kupatiwa nakala za mikataba ambayo Serikali imeingia na Makampuni na wadau mbalimbali lakini ombi hilo limeshindikana. Aidha, Kifungu cha 10 cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge ya mwaka 1988 na marejeo yake ya mwaka 2002, kinatoa haki kwa Mbunge kuomba na kupatiwa taarifa kutoka kwa mtumishi yejote katika taasisi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara chache sana Kifungu hiki kinaheshimiwa na watendaji kwani Waheshimiwa Wabunge mara kadhaa wamekuwa wakiomba kupatiwa taarifa kutoka kwa watendaji Serikalini bila mafanikio. Kambi ya Upinzani inauliza ni kwa vipi tutaisimamia Serikali kama hatuna taarifa sahihi kuhusiana na utendaji wa Serikali? Pengine Serikali itamke wazi ni nini kifanywe na Wabunge ili upatikanaji wa taarifa zake usiwe wa vikwazo kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba Mpya na changamoto zake. Kwa kuangalia uzoefu wa nchi nyingine ambazo zimepitia mchakato wa mabadiliko ya Katiba katika miaka ya hivi karibuni, ni vyema kutambua kuwa mchakato huu siyo mwepesi. Ni mchakato unaohitaji kupambanua mapema changamoto zinazoweza kujitokeza katikati ya mchakato na hivyo kuandaa mazingira mbadala ya kukabiliana na changamoto husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya kuwa na Katiba mpya ifikapo 2014, ni dhahiri kuwa hakuna uhakika wa asilimia mia moja wa kuipata kwa wakati. Aidha, kupata Katiba mpya ni jambo moja na kuanza kuitumia ni jambo jingine. Kuanza kuitumia Katiba mpya kutahusisha mabadiliko ya sheria nyingine kadhaa zikiwemo za uchaguzi na taasisi zinazohusiana na uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi ni jambo tete wakati wote. Ni dhahiri kuwa ushuhuda uliopatikana

katika chaguzi ndogo za marudio za Ubunge katika Majimbo ya Igunga Mkoani Tabora na Arumeru Mashariki Mkoani Arusha pamoja na uchaguzi wa marudio wa Madiwani katika Kata kadhaa nchini; uchaguzi wa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Jimbo la Uzini, Zanzibar zimeonyesha ushindani ambao ufumbuzi wake ni kuwa na taasisi makini sambamba na mifumo ya haki katika kuzisimamia chaguzi hizi. Matumizi ya nguvu za ziada za vyombo vy'a dola hususan Polisi katika kudhibiti chaguzi hizi hautoi viashiria vizuri vy'a uwepo wa amani katika chaguzi siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko mengi katika chaguzi hizi yamegusa maeneo yafuatayo:-

- (i) Daftari la kudumu la wapiga kura. Raia kadhaa wenyе umri na sifa nyinginezo za kupiga kura wamezuiwa haki yao ya Kikatiba ya kupiga kura bila sababu za msingi.
- (ii) Tume ya Uchaguzi kuonyesha vitendo mbalimbali vy'a upendeleo wa wazi kwa Chama Tawala. Ni dhahiri kuwa Tume ya Uchaguzi haiko huru na ni hatari kuendelea kuitegemea kwa njia yoyote kuratibu chaguzi zozote za mbele hata katika mchakato mzima wa Katiba.
- (iii) Kushindikana kwa kiasi kikubwa kutekelezwa kwa Sheria ya Gharama za Uchaguzi kunakoendana na mkanganyiko wa Sheria yenyewe baina ya Uchaguzi Mkuu na Chaguzi Ndogo.

(iv) Kushindikana kwa kiasi kikubwa kutekelezwa kwa maadili ya uchaguzi kunakosababishwa pamoja na mambo mengine upendeleo wa taasisi kadhaa zenyet dhamana ya kusimamia chaguzi mbalimbali ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya marekebisco ya Katiba ya Mpito. Ili kuweka tahadhari ya kudumisha amani na utulivu kabla, wakati na baada ya uchaguzi, hatuna budi kama Taifa kuchukua hatua za dharura kurekebisha usimamizi wa chaguzi zetu katika sasa na hapo tutakapokuwa na Katiba mpya. Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa na marekebisco ya mpito ya Katiba yetu yatakayowezesha Tume yetu ya Uchaguzi kuwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya *pension* kwa wazee. Kabla ya kutoa maelezo zaidi, naomba kunukuu kauli ya Waziri Mkuu aliyoitoa hapa Dodoma akiwahutubia Wazee wakati wa maadhisho ya kilele cha siku ya Wazee Duniani tarehe 1 Oktoba 2009. Nanukuu:-

*"Serikali inatambua umuhimu wa Wazee katika maendeleo ya nchi yetu, inatambua **Wazee ni rasilimali na hazina** kubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu na kuleta mabadiliko ya kiuchumi. Wazee ndio mliotujengea misingi ya Taifa tuliyonayo hivi sasa".* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inakubaliana kabisa na kauli hiyo ya Waziri Mkuu. Hoja ya msingi ni kuiuliza Serikali ni kwa nini Wazee ambao ni

rasilimali na hazina kubwa ya Taifa letu iendelee kufa kihoro wakati walikwishawekeza zamani katika nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani wakati tunawasilisha hotuba yetu kwa Wizara ya Kazi mwaka 2011/2012 tulisema yafuatayo, nanukuu:-

*"Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dhana ya hifadhi ya jamii ni pana sana, Kambi ya upinzani tunaitaka Serikali kuzingatia pendekezo letu kuweka mfumo utakaowafanya wazee wote kupata pesheni (universal pension) kila mwezi kwa kiasi cha shillingi ishirini elfu kwa kuanzia ili kuwapunguzia wazee wetu hasa waishio vijiji ni gharama kubwa za maisha". Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasilitiza kuwa pensheni hii ni muhimu kwa kuwa itasaidia kuongeza kipato kwa wanaoishi vijiji ni ambako umaskini wa kipato umejikita na kupunguza umasikini kwa kiwango cha takriban asilimia 57.9 kwa wazee walio na umri zaidi ya miaka 65. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kauli ya Waziri Mkuu kuwa:-

*"Idadi hii ya wazee inajumuisha waliokuwa wanafanya kazi za kuajiriwa au waliojajiri wenyewe na walioko vijiji ni wakijishughulisha na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Hili ni kundi kubwa ambalo likitumiwa vizuri na hasa kwenye maeneo maalum linaweza kuinua kasi ya maendeleo ya Taifa hili". Mwisho wa kumukuu Waziri Mkuu.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya utafiti ulifanywa na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia masuala ya wazee liitwalo (*HelpAge International*) na kutolewa mwezi May 2010, Idadi ya wazee ni 1,327,883. Tunaamini hili linawezekana kutekelezwa katika mwaka huu wa bajeti kama Serikali ina nia ya kweli ya kulitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mahesabu rahisi ni kwamba kwa jumla ya wazee 1,327,883, kama kila mmoja akipata Sh.20,000/- (kiasi kinachopendekezwa) kwa mwezi malipo yatakuwa shilingi  $1,327,883 \times 20,000 = 26,557,660,000/-$  (bilioni 26.557) na kwa mwaka malipo yatakuwa shilingi  $26,557,660,000/- \times 12 = 318,691,920,000/-$  (bilioni 318.691). Kama tukiongeza 5% ya fedha hizi kama gharama za utawala kuhakikisha wazee wote wanapata fedha hizo kwa mwaka taifa litatumia shilingi  $334,626,516,000/-$  (bilioni 334.626) kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzito wa Kauli aliyoitoa Waziri Mkuu wakati akiwahutubia Wazee tarehe 1 ktoba 2009 kuwa:-

*"Wazee ni rasilimali na hazina kubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu na kuleta mabadiliko ya kiuchumi".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kiasi hicho kwa mwaka Serikali ina uwezo wa kukipata. Kwa kuwa tunatarajia kufanya sensa mwaka huu pamoja na

kuanzisha utambuzi wa wananchi wote kwa kutoa vitambulisho vya uraia, Kambi ya Upinzani inaona kuwa, takwimu halisi na za kuaminika za wazee wetu zitapatikana kwa ajili ya kutekeleza azma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora na haki za binadamu. Mauaji ya raia. Kambi ya Upinzani katika hotuba yetu ya mwaka uliopita katika ofisi hii, tulitoa takwimu na majina ya wananchi waliouwawa kutokana na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliofanywa na vyombo vya dola likiwemo Jeshi la Polisi kama ifuatavyo, naomba kunukuu:-

*"Mheshimiwa Spika, mauaji ya raia mikononi mwa Polisi yameendelea kuongezeka kwa kasi ya kutisha sana kutoka matukio ya kuuawa watu watano (5) mwaka 2008, watu 15 mwaka 2009 hadi watu 52 mwaka 2010. Kwa kasi hiyohiyo, mwaka huu pekee, kwa miezi ya Januari hadi Mei 2011, tayari watu tisa (9) wameripotiwa kuuawa na Polisi katika eneo moja tu la Nyamongo, Tarime na kushuhudia matukio ya unyama wa kutisha yakifanyanywa na chombo cha dola kwa kutupa miilli ya marehemu hao barabarani na kuitelekeza.*

*Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunataka hali hii ichukuliwe hatua na kuangaliwa kwa umakini mkubwa hasa ikizingatiwa kuwa mwaka huu pia kumefanyika mauaji ya raia watatu (3) huko Arusha ambao walipigwa risasi na Polisi kwa kile kilichodaiwa kuwa walitaka kuleta vurugu na uvunjaji amani.*

*Mheshimiwa Spika, wananchi wengine tisa (9) wameshauawa Tarime, wawili Kisarawe, mmoja*

*Sumbawanga na mwingine Tabora. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, matukio haya yameainishwa kama ifuatavyo:-*

(i) *Mnamo Januari 5, 2011 watu watatu ambao ni Denis Michael, Ismail Omary na Paul Njuguna Kaiyele waliuwawa na wengine 21 kuumizwa vibaya wakati wa maandamano mjini Arusha.*

(ii) *Mnamo tarehe 16 Mei, 2011 polisi waliwaua watu watano (5) katika eneo la Mgodi wa North Mara Wilayani Tarime unaomilikiwa na Kampuni ya African Barrick Gold Mine na kufanya idadi ya watu waliouliwa katika eneo hilo toka mwaka 2009 hadi Juni 2011 kuwa 34. Kama hiyo haitoshi, mnamo tarehe 9 Juni, 2011 kijana ajulikanaye kama Nyaitore mkazi wa kijiji cha Nyangoto Wilayani Tarime alipigwa risasi ya bega na Polisi wa mgodi na kulazwa hospitali ya Sungusungu.*

(iii) *Mwezi Mei, 2011 katika kijiji cha Namanga Wilayani Nachingwea, Askari wa Wanyamapori walimpiga risasi kwenye miguu yote Juma James (27) ambaye anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea.*

(v) *Mkoani Tabora, Wilayani Urambo mnamo tarehe 28 Mei, 2011 Askari Polisi walimuua Juma Saidi na kujeruhi wengine kadhaa katika kijiji cha Usinge. Tukio hilo lilitanguliwa na kipigo kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Shela na wenzake mnamo tarehe 26 Mei, 2011 vitendo vilivyofanywa na Askari walioenda kukamata mifugo.*

(vi) Mnamo Aprili 2, 2011, mkazi wa kijiji cha Mwanza Buriga, Kata ya Kukirango, Wilaya ya Musoma vijijini, Mwabia Zome (40) aliuawa kwa kupigwa risasi chini ya titi la kushoto na Askari Magereza wa Gereza la Kiabakari.

(vii) Watu wengine wa umri kati ya miaka 25- 30 walipigwa risasi tarehe 7 Machi, 2011 ambapo Sese Kabanzi, alifia njiani wakati akipelekwa hospitali na July Hamisi alikufa hapo hapo baada ya kupigwa risasi maeneo ya kifuani.

(viii) Mnamo tarehe 5 Februari, 2011 Askari wa Wanyama Pori katika Hifadhi ya Selou wameripotiwa kuuwa watu wawili na kujeruhi mmoja Wilayani Kisarawe Mkoani Pwani. Waliokufa ni Hamisi Boy na Mohamed Suta na anayeuguza majeraha ni Mohamed Kigwiso.

Mheshimiwa Spika, kuna ushahidi kuwa Askari hawa wanashutumiwa kwa kuendeleza matukio ya ukatili dhidi ya wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo kwa makusudi huku Jeshi la Polisi likishindwa kuwasaidia raia kulinda usalama wao. Wilayani Kisarawe Askari hawa wanadaiwa kuwauwa na kuwatupa mtoni na kupelekea raia wafuatao waliwe na mamba, ambao ni Ndugu Majengo, Mohamed Kibavu, Adamu Feruzi, Semeni Abdala Kube, Hemed Kassim, Mzee Hussein, Ramadhani Mgeto na Bwana Mkala.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha zaidi, kuna matukio mengi ambapo ndugu za waathirika hao wa ukatili wamekuwa wakinyanyaswa pale wanapofuatilia

*haki au uwajibikaji katika vyombo vyaya usalama. Aidha, matukio ya uchomaji moto miili ya marehemu, kulishwa mamba na kutupwa na kutelekezwa barabarani maiti ni matukio yanayotuingiza katika historia mpya ya kutojali haki za binadamu.*

*Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miezi mitano ya mwaka 2011 tayari Watanzania 21 wameuwawa kwa kupigwa risasi maeneo mbalimbali ya nchi yetu na wengine wengi kuumizwa kwa kupigwa risasi wakiwemo wanafunzi wa shule za Sekondari na Vyuo Vikuu mbalimbali hapa nchini.*

*Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ifanye mambo yafuatayo ili kukomesha mauaji haya:-*

*(i) Kulipa fidia stahili kwa mujibu wa sheria husika za nchi kwa ndugu na/au jamaa wa wale wote waliouawa kutokana na vitendo vyaya Jeshi la Polisi la Tanzania na kwa wale wote waliouumizwa kwa namna yoyote ile na/au kuharibiwa mali zao kutokana na vitendo hivyo.*

*(ii) Kuwachukulia hatua Askari Polisi, Askari Magereza na wale wa Wanyamaporu ambao wamehusika katika mauaji haya kwani hali hii ikiachwa iendelee kama ilivyo sasa ni hatari kwa usalama wa Watanzania na inalifanya Taifa letu kuingia kwenye rekodi mbaya ya kukiuka haki za binadamu.*

*(iii) lundwe Tume Huru ya Uchunguzi ya Kimahakama (Judicial Commission of Inquiry)*

*itakayoundwa na Majaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania ili kufanya uchunguzi huru. Tunapenda kusisitiza kuwa tunataka iundwe Tume ya Uchunguzi ya Kimahakama kwani hufanya kazi zake kwa uwazi na huruhusu wananchi kuhudhuria na/au kushiriki moja kwa moja katika kazi za Tume kama mashahidi na/au kwa kuhoji mashahidi wengine wanaotoa taarifa kwenye Tume hiyo.*

*Chanzo: Taarifa ya Mwenendo wa Haki za Binadamu ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ya mwaka 2010.” Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuonyesha ukiukwaji wa haki za binadamu kwa mwaka uliopita, naomba kunukuu kauli ya Waziri Mkuu aliyoitoa wakati akifanya majumuisho ya hoja yake katika Bunge la Bajeti Julai Mosi mwaka uliopita kama inavyoonekana katika Taarifa Rasmi za Bunge hili (*Hansard*) kama ifuatavyo:-

*“Mheshimiwa Mwenyekiti, katika madai yaliyowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, hususan wa kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu mauaji yanayodaiwa kufanya na baadhi ya Vyombo vya Dola, ni vyema ikaeleweka kuwa, Serikali haina nia ya kupuuza shutuma hizi za mauaji ya raia wake. Katika kulishughulikia suala hili, suala la mauaji ya raia yanayodaiwa kufanya na baadhi ya Vyombo vya Dola, Serikali imefikia uamuzi sasa wa kuvichunguza vifo hivyo kwa kupitia Sheria husika ya Inquest kwa kadri itakavyowezekana. Inawezekana kwa muda mrefu*

*utaratibu huo hauzingatiwi lakini kwa sasa, ni lazima tuufuate na ni lazima sasa tuutekeleze ili kutokana na maamuzi ya uchunguzi huo watu waweze kupelekwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi pale itakapobainika kwamba vifo hivyo au mauaji hayo hayakuwa na sababu za msingi.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu tukatambua kuwa kila kifo cha mtu ni tofauti na cha mwingine na hutokea katika mazingira tofauti. Hivyo, kwa kuzingatia kilio cha wananchi ambao Serikali ina wajibu wa kuwalinda, vifo vyote ambavyo vimetokea kwa sababu ya matumizi ya nguvu, kikiwamo kifo cha raia kilichotokea akiwa chini ya uangalizi wa Vyombo vya Dola, ni vema Serikali ikazingatia mazingira husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kauli hii nzito ya Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi wa Shughuli zote za Serikali ndani ya Bunge, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa agizo hili juu ya hatua stahiki zilizochukuliwa dhidi ya mauaji ya raia kama tulivyoonyesha katika hotuba yetu mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2011 hali ya kuheshimu na kuzingatia haki za binadamu haikuwa tofauti na mwaka 2010 kwa sababu bado taarifa zinaonyesha kuwa yapo mauaji yenye kutia shaka ambayo yaliripotiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ya mwaka 2011 ukurasa wa 17 na 18 kipengele cha 2.1.2, kutoka mwezi

Januari hadi Desemba takribani watu 25 wamefariki wakiwa mikononi mwa Polisi na Maafisa wengine wa ulinzi. Hali kadhalika matukio yote haya yamewaacha zaidi ya watu 50 kubaki na majeraha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa zilizopo ni kuwa mauaji yameripotiwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo mwendelezo wa mauaji katika mgodi wa *North Mara*, unyanyasaji wa Polisi wa tarehe 28/05/2011 na kuwaweka kizuizini viongozi wa *CUF* akiwemo Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge, mauaji ya mtu mmoja eneo la Ubaruku katika Wilaya ya Mbarali na manyanyaso ya Polisi kwa wachimbaji wadogowadogo katika Wilaya ya Liwale Mkoani Lindi. (Taarifa ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu 2011, ukurasa wa 19, 20 kipengele cha 2.1.2.2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunatambua kuwa taarifa hizi za mauaji zinawagusa Askari Polisi pia kwa kuwa kwa mwaka uliopita katika maeneo ya Tarime, Tabora, Shinyanga, Arusha na Rukwa, Polisi watano waliuwawa na wananchi. (Taarifa ya Kituo cha Haki za Binadamu mwaka 2011, ukurasa wa 18 kipengele cha 2.1.2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi kwa ujumla wake zinaligusa Jeshi letu la Polisi kwa kiasi kikubwa. Kambi ya Upinzani tunaamini kuwa kuacha kuchukua hatua dhidi ya Polisi wachache wanaolichafua Jeshi la Polisi kwa ujumla inasababisha picha mbaya ya Taifa letu Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji na unyanyasaji wa kisiasa. Hivi karibuni kumekuwa na manyanyaso na hata mauaji ambayo kwa namna moja ama nyingine yamekuwa yakihuushwa na siasa dhidi ya wananchi wanaojiunga na Vyama vya Upinzani. Hili linadhihirika hasa katika chaguzi ndogo za Madiwani na Ubunge au hata za Vijiji na Vitongoji hapa nchini. Hivi karibuni Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa Highness Kiwia - Illemelela na Mheshimiwa Salvatory Machemli - Ukerewe, walikatwa mapanga wakati wa Uchaguzi Mdogo wa Udiwani wa Kata ya Kirumba, Jimbo la Illemela Mkoani Mwanza na wanaosadikiwa kuwa wafiasi wa Chama cha Mapinduzi, huku Polisi wakishindwa kuzuia hali hiyo pamoja na kuwa walifika katika eneo la tukio tena wakiwa na silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa kesi ya kuwajeruhi Waheshimiwa Wabunge ipo Mahakamani, Kambi ya Upinzani imeona ni vema kurejea tukio hilo kwa kuwa linahusiana moja kwa moja na hali ya siasa nchini. Manyanyaso hayo yanazidi kushamiri siku hadi siku ambapo mpaka sasa katika Wilaya ya Kilosa wanachama na baadhi ya viongozi wa CHADEMA wapo jela na kuwekewa masharti magumu ya dhamana kwa sababu za kisiasa. Katika Wilaya Rungwe waliokuwa wagombea Udiwani katika baadhi ya Kata wamebambikiwa kesi mbalimbali zinazohuushwa na siasa na pia katika Kijiji cha Bermi, Wilaya Babati, baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Meatu ambapo wafiasi wa Vyama vya Upinzani wamekuwa wakibambikiwa kesi za uongo mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika chaguzi ndogo za Igunga na Arumeru Mashariki, vifo vilivyotokea kwa sababu za kisiasa viliripotiwa mathalani kifo cha marehemu Mbwana Masoud na taarifa kupelekwa Polisi lakini hadi leo hakuna hatua zilizochukuliwa. Mara tu baada ya uchaguzi mdogo wa Arumeru Mashariki, yalitokea mauaji mengine ya kiongozi wa CHADEMA Msafiri Mbwambo na vifo vingine vinne ambapo mauaji hayo yanahusishwa na siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, manyanyaso haya hayawezi kuvumiliwa tena, ni lazima kama Taifa, tujue kuwa nchi hii ni ya Vyama vingi vya Siasa na hivyo kila raia ana haki ya kujunga na Chama chochote cha Siasa bila shinikizo.

Hii ni kwa sababu bado Mikutano ya kisiasa na hata Mikutano ya Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani inavamiwa mara kwa mara, mathalan uvamizi aliofanyiwa Mbunge wa Iringa Mjini Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Magereza na Haki za Wafungwa katika taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala ya mwezi Septemba, 2011 kama ilivyonukuliwa na Taarifa ya Haki za Binadamu ya Marekani kuhusu Tanzania ya (*United States, Department of State, Human Rights Report - Tanzania May, 2012* (ukurasa wa 4 - 5) kuwa kuna matatizo makubwa sana katika Magereza yetu nchini ambapo matatizo kama msongamano wa kutisha, magonjwa mbalimbali, mahabusu wengi kukaa muda mrefu Gerezani bila kesi zao kusikilizwa, na chakula kibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mahabusu wa Gereza la Keko Jijini Dar es Salaam wamewasilisha malalamiko yao kwa Jaji Mkuu kwa barua yao ya tarehe 11 Julai, 2011 ambapo wameonyesha kuwa tatizo lao kubwa ni:-

- (i) Msongamano uliokithiri unaosababishwa na kusuasua kwa uendeshaji wa kesi kutoka Mahakama za Mwanzo, Wilaya, Mkoa na Mahakama Kuu;
- (ii) Kubambikiwa kesi na Jeshi la Polisi hasa Kitengo cha Upelelezi; na
- (iii) Rushwa iliyokithiri kwa baadhi ya Maofisa na Makarani wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa kwa hali hii ya gereza moja tu katika Jiji la Dar es Salaam ni wazi kuwa Magereza mengi nchini yapo katika hali mbaya sana. Mathalani Gereza la Karanga lililopo Mjini Moshi, Mkoani Kilimanjaro linakabiliwa na msongamano mkubwa kutokana na kuwahifadhi wafungwa kutoka Wilaya za Hai, Rombo, Moshi Mjini, Moshi Vijijini na Siha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Karanga pia linakabiliwa na changamoto kubwa ya usafiri ambapo lipo gari moja (Karandinga) linalotumika kuwapeleka na kuwarudisha mahabusu katika Wilaya zote.

Kwa maana hii, Karandinga huhudumia Wilaya moja kwa siku moja na kusababisha mahabusu kutoka Wilaya nyingine zote kutokakupelekwa Mahakamani kusikiliza mashauri yao, na kwa maana hiyo, mahabusu

hupelekwa katika Mahakama za Wilaya zao mara moja tu kwa wiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ya Magereza nchini imesababisha wafungwa wengi kukaa Gerezani kwa muda mrefu kwa kisingizio cha kusubiri kesi zao kusikilizwa au kutokamilika kwa upelelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza, yafanyike marekebisho ya kisheria ili uwepo ukomo wa ukaaji katika Magereza wakati mtuhumiwa akisubiri hicho kinachoitwa upelelezi kukamilika.

Hii itapunguza tatizo la msongamano katika Magereza mengi nchini na kuhakikisha kila mtuhumiwa/mfungwa, anatendewa haki kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya pia yanachangiwa na kuwepo kwa maslahi madogo wanayoyapata Askari Polisi na Askari Magereza hata baada ya kufanya kazi katika mazingira magumu na makazi duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuboresha maslahi ya Jeshi la Polisi na Magereza kwa sababu, kwa kushindwa kufanya hivyo, kunawaathiri wananchi wengine ambao kwa namna moja ama nyingine ndiyo waathirika wakubwa wa matatizo hayo.

Kambi ya Upinzani tunaamini kuwa hata kushindwa kuboresha mazingira ya kazi kwa Askari Polisi

na Askari Magereza ni kinyume na haki za binadamu kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta taarifa rasmi ya namna ya kuboresha hali ya Magereza nchini ili kukidhi dhana ya Chuo cha Mafunzo na siyo Chuo cha Unyanyasaji na Ubambikaji wa Kesi kwa Wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya Magereza nchini yamesababisha watu wengi kufariki Magerezani, kupata ulemavu wa kudumu na wengi kukaa Magerezani kwa muda mrefu bila kupata haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaisisitiza Serikali kuchukua hatua za haraka kunusuru Idara ya Magereza na kutoa taarifa katika Bunge hili, na kama hatua za haraka hazitachukuliwa, tutalazimika kuomba kuleta hoja binafsi ili kuliomba Bunge kuazimia kuunda Tume Maalumu kushughulikia mateso na ukiukwaji mkubwa wa haki za mahabusu na wafungwa kwa upande mmoja na Askari Magereza kwa upande wa pili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gharama za Uendeshaji Serikali, kwa mujibu wa Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa hapa Bungeni tarehe 14 Juni 2012, katika bajeti ya Shilingi trilioni 15.1, Shilingi trilioni 10.6 ni gharama za uendeshaji na salio la Shilingi trilioni 4.5 ndio linalokwenda kwenye maendeleo. Kwa uhalsia huu ni wazi kwamba maendeleo yatakuwa kwa kasi ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haipingi matumizi ya kawaida ya msingi katika Serikali, ila inapinga matumizi ambayo kimsingi siyo ya lazima.

Kwa mfano, posho za vikao ni matumizi ambayo yasiyo ya lazima kwa sababu mtumishi anayelipwa mshahara, kuhudhuria vikao ni sehemu ya kazi yake. Jedwali hapa chini linaonyesha posho za vikao katika Idara za Ofisi ya Waziri Mkuu ambapo fedha hizo zingeweza kutumika katika shughuli za maendeleo kama posho hiyo ingefutwa:-

**KASMA IDARA**

**VIKAO**

210314 Utawala  
95,000,000.00

Fedha na Uhasibu  
20,250,000.00

Sera na Mipango  
31,500,000.00

Ukaguzi wa Ndani  
17,400,000.00

Habari, Elimu na Mawasiliano  
3,000,000.00

Ugavi  
20,000,000.00

Sheria  
1,500,000.00

**POSHO YA**

Menejimenti ya Mifumo ya Habari	
800,000.00	
Uratibu wa Maafa	
39,000,000.00	
Maadhimisho ya Sherehe za	
47,000,000.00	Kitaifa
Bunge na Siasa	
15,000,000.00	
Maendeleo ya Sekta Binafsi	
24,000,000.00	
Uratibu wa Shughuli za Serikali	
100,500,000.00	
Mpiga Chapa wa Serikali	
55,100,000.00	
JUMLA	
470,050,000.00	

**Chanzo:** Randama Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Sh. 470,050,000/= zitatumika kama posho ya vikao katika Ofisi ya Waziri Mkuu fungu 37 peke yake. Hapa hatujaangalia fungu 56 ambalo pia liko chini ya Ofisi yake, na Wizara nyingine.

Hii ina maana kwamba kuna fedha nyingi sana zinazotumika kama posho ya vikao kwa watumishi ambao tayari wana mishahara. Kuna matumizi mengine ambayo Kambi ya Upinzani inaona pia kuwa

siyo ya lazima kama posho ya mavazi kwa safari za nje, sare za kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na matumizi makubwa ya Serikali katika posho mbalimbali, mbali na kutokuwepo kwa sera madhubuti inayosimamia ununuzi na aina ya magari kwa kada mbalimbali katika utumishi wa umma, Serikali ina tatizo lingine kubwa la matumizi makubwa yasiyoratibiwa katika matengenezo na ununuzi wa mafuta ya magari.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Kiufanisi na Kiuchunguzi kama ilivyotolewa na CAG ya tarehe 31Machi, 2012 ni kwamba Wizara ya Ujenzi ndiyo yenyeye jukumu la kununua, kusajili na kufanya matengenezo ya magari ya Serikali, ikisaidiana na Wakala wake TEMESA (*Tanzania, Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya CAG inaonyesha kwamba Wizara ya Ujenzi hajjaweka mfumo wa kusimamia matengenezo ya magari.

Pia, hakuna sera yoyote ya ununuzi na matengenezo ya magari na hivyo hakuna mwongozo toshelezi juu ya usimamizi wa ununuzi na matengenezo ya magari. Wizara hajjatoa mwongozo kwa TEMESA juu ya hatua na michakato ya kufuata na wala Wizara haisimamii utendaji wa TEMESA ipasavyo.

Wizara pia haina kumbukumbu za kila wakati kama chombo cha usimamzi wa matengenezo ya magari. Mfumo wa matengenezo ya magari ya Serikali hausimamiwi ipasavyo na TEMESA kwa kuwa magari ya

Serikali hayakaguliwi kabla na baada ya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu huu wa Wizara na *TEMESA* katika kusimamia matengenezo ya magari ya Serikali kunapelekea Serikali kupoteza fedha nyingi sana, kwani licha ya kuwa hakuna usimamizi wa kutosha, lakini pia hakuna taarifa au kumbukumbu za matengenezo ya magari na gharama zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na matumizi makubwa ya fedha za walipa kodi kwa matengenezo ya magari ya Serikali ambayo hayana usimamizi madhubuti. Gharama kubwa sana inatumika kwa mafuta na matengenezo ya magari kama jedwali linavyoonyesha hapa chini:

### **Mafuta na Matengenezo**

<b>IDARA MAFUTA</b>	<b>KASMA 220300</b>	<b>KASMA 230400</b>
	<b>MATENGENEZO</b>	
Utawala	126,500,000	91,000,000
Kitengo cha Fedha Uhasibu	13,250,000	4,150,000 na
Sera na Mipango	30,000,000	20,000,000
Ukaguzi wa Ndani	10,920,000	12,000,000
Habari, Elimu na Mawasiliano	15,000,000	15,000,000
Ugavi	9,627,500	10,000,000
Kitengo cha Sheria	5,625,000	

Menejimenti ya Mifumo Habari	550,000	1,000,000	ya
Uratibu wa Maafa	45,000,000	19,400,000	
Maadhimisho ya Sherehe Kitaifa	25,000,000	11,000,000	za
Bunge na Siasa	30,000,000	36,000,000	
Maendeleo ya Sekta Binafsi	51,000,000		
	20,000,000		
Uratibu wa Shughuli za Serikali	49,500,000		
	39,000,000		
Mpiga Chapa wa Serikali	45,000,000		
	25,080,000		
JUMLA	456,972,500		
	303,630,000		
JUMLA KUU	760,602,500		

**Chanzo:** Randama, Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Sh. 660,602,500/= zitahitajika kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu pekee kama gharama ya mafuta na matengenezo ya magari kwa mwaka huu pekee wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe ni mhanga wa tatizo hili. Kwa miezi sita niliacha kutumia gari la Serikali aina ya *Toyota Land Cruiser V8* ambalo nilipewa kwa matumizi ya kazi kwa nafasi yangu kama Kiongozi wa Upinzani Bungeni nikitaka nipewe gari la gharama nafuu zaidi. Stahili hii niliipata kupitia waraka

wenye masharti ya kazi ya Kiongozi wa Upinzani, Bungeni uliotolewa 25 Oktoba, 2010, kabla hata ya Uchaguzi Mkuu wa 2010. Mazingira kama haya, yalimfika pia Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Pinda siku za nyuma ilipodaiwa kukataa kutumia gari aina ya *Land Cruiser VX* na akakusudia kutumia gari ya gharama nafuu zaidi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la magari ni suala la kisera zaidi kuliko la utashi wa mtu binafsi. Pamoja na kususa kwa muda gari hili, Serikali haikujali kubadilisha sera yake ya matumizi ya magari ya gharama kubwa pamoja na kutoa matamko mara kwa mara kuashiria azma hiyo. Wakati kwa nafasi yangu sikuwa na uwezo wa kubadilisha sera, upande wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni dhahiri mamlaka ya kubadilisha sera anayo na amekuwa akishuhudia Serikali anayoiongoza ikiendelea kununua na kutumia magari haya ya gharama kubwa. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ahadi yake leo sasa tutasubiri utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mshikamano wa Taifa Vyama vya Siasa, Vyama vya Siasa nchini vinasimamiwa na Sheria Na. 5 ya mwaka 1992 pamoja na marekebisho yake. Sheria hii, kifungu cha 9 (2) inakataza uwepo wa Vyama vya Siasa vilivyopo kwa misingi ya ukabila, udini, au ukanda. Msajili wa Vyama vya Siasa amepewa mamlaka na sheria kusimamia msingi huu muhimu wa mshikamano wetu kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, kumekuwepo *propaganda* nyingi na za kimkakati na kwa bahati mbaya zaidi zikiongozwa na baadhi ya

Viongozi wa Chama Tawala na Vyama washirika wake kueneza chuki mionganini mwa Watanzania kuwa vyama makini vya upinzani ni vya kikabila, kidini na hata vya kimaeneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa propaganda hii inakusudia kujenga uhalali wa Chama Tawala na washirika wake dhidi ya Upinzani makini, ni hakika kuwa inapanda mbegu mbaya ya chuki na mpasuko mionganini mwa Watanzania kwani maneno huumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio mbalimbali ya siasa za aina hii barani Afrika yanatukumbusha mauaji ya halaiki Rwanda 1994 baina ya Wahutu na Watusti, Sudan hasa eneo la Darfur, Nigeria, mapambano baina ya Waislamu na Wakristo, Somalia na hata Kenya machafuko ya mwaka 2008 baada ya uchaguzi yalisababishwa na kuchochewa sana na siasa za kibaguzi na kikabila baina ya watokao Mlima Meru na watokao eneo la Bonde la Ufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kauli mbalimbali ambazo zimekuwa zikitolewa na baadhi ya wanasiada zikiashiria kuwagawa Watanzania katika misingi ya udini, ukabila na ukanda. Hata katika mijadala yetu ndani ya Bunge hili Tukufu, dalili za baadhi ya masuala haya yameanza kujitokeza kwa Waheshimiwa Wabunge katika kujadili masuala mbalimbali kujikita kwenye siasa za ukanda na hata mara nyingine ukabila. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni ya hatari sana na italigawa Taifa letu kama sisi viongozi hatutachukua

hatua mapema na kama tukiendeleza kuukoleza wimbo huu wa udini, ukabila na ukanda, hakika Tanzania yetu haitakuwa moja tena. (*Makofii*)

Kambi ya Upinzani inatahadharisha Vyama vyote vya Siasa na viongozi wote ambao katika kuficha udhaifu wa Vyama vyao na Utendaji wao wamekuwa wakijikita kwenye propaganda hizi, waache mara moja kwani Watanzania ni wamoja na tusifiche madhaifu yetu kwa kuwagawa Watanzania katika misingi ya kidini, kikanda na kikabila kwani madhara yake ni makubwa sana na hakuna hata mmoja wetu ambaye atakuwa salama. Aidha, tunamtaka Msajili wa Vyama vya Siasa nchini kuchukua hatua mara moja dhidi ya Vyama vya Siasa na vyama ambavyo vimekuwa na tabia hii ya uchochezi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa. Kadhalika, kama kweli kuna chama chochote kinachoonekana kuwepo kwa misingi hii ya kibaguzi kifutwe haraka ili kuliepusha Taifa letu na uchafu huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari ya kuligawa Taifa sasa haiko katika siasa pekee, bali hata ndani ya dini zetu. Yanayowasukuma baadhi ya viongozi wetu wa dini kuendeleza na kukoleza vita hii ya kiimani ni pamoja na udhaifu wa Serikali kukemea na kuchukua hatua stahiki kadri matukio yanavyojitokeza. Kuna ushahidi tosha vile vile kuwa baadhi ya viongozi wetu wa dini wametumiwa na kufadhiliwa na watu mashuhuri wakiwepo wafanyabiashara wakubwa kwa niaba ya viongozi wa Kiserikali na Vyama vya Siasa kueneza propaganda hizi kwa malengo ya kisiasa.

Vipo vyombo vyahabari vinavyomilikiwa na Taasisi za Dini ambavyo wakati mwingine vimekuwa vikieneza uchochezi wa wazi dhidi ya dini nyingine bila mamlaka za Kiserikali kuchukua hatua stahiki. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tamko kukemea hali hii na iahidi ndani ya Bunge kutokuvumilia dini, kiongozi au muumuni yejote wa dini yejote atakayeshindwa kuheshimu haki ya mwenye imani tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu unyanyapaa wa Fikra Vyuo Vikuu; Kambi ya Upinzani inasikitika sana kuwa hadi sasa baadhi wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) waliokuwa wanapinga kumaliza masomo yao bila kufanya elimu kwa njia ya vitendo (*Field Practical*) wako majumbani baada ya kusimamishwa masomo na Uongozi wa Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukumbu zinatuonyesha kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundis walikutana na Viongozi wa Wanafunzi na wakakubalina na madai ya wanafunzi kuhusiana na wanachuo kupatiwa mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na juhudzi za Serikali kwa kutumia baadhi ya Viongozi wa Vyuo Vikuu hususan vyahabari umma, kuwanyima haki za kifika wanafunzi wanaohisiwa kuwa wafuasi au wapenzi wa Vyama vyahabari Upinzani. Hoja ya kupiga marufuku siasa vyuoni inaonekana kuwahuusu tu wale wasio wanachama cha CHADEMA huku Chama cha Mapinduzi nacho kikikazana kufungua matawi katika Vyuo Vikuu.

Mbali na kujenga tabaka la kibaguzi mionganoni mwa vijana wetu, hakika vitisho, manyanyaso na hofu wanayojengewa vijana hawa inawadumaza kifikra vijana wetu katika kuhoji, kudadisi na hata kuthubutu. Tunaharibu viongozi wa kesho na hakika dhambi hii italitafuna Taifa letu hususan watekelezaji wa mkakati huu kwa miaka mingi ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa kauli ya ni kwa nini ubaguzi huu unaendekezwa katika Vyuo vyetu Vikuu na kwa kupitia Uongozi wa Vyuo Vikuu nchi kuwarudisha Chuoni/Vyuoni wanafunzi wote wapatao 260 ili wamalizie masomo yao waliostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, kwa mujibu wa kifungu cha 19 (1) cha Sheria No. 9 ilioanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ni wajibu wa kila mtu aliyenufaika na mikopo ya elimu ya juu kurejesha mikopo Serikalini kupitia Bodi ya mikopo. Pamoja na changamoto ya urejeshwaji wa mikopo kwa walionufaika, Bodi imeshindwa kuwa na mfumo wezeshi wa kirejesha mikopo kwa wakati. Zoezi la kutafuta kampuni za madalali wa minada ili kukamata mali za wahusika, ni kuonyesha kushindwa kuwa na njia mbadala ya kurejesha mikopo na kuiongezea Bodi gharama zisizo za msingi, pia kutowatendea haki Watanzania wasio na ajira rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima itambue walionufaika na mikopo, wengi ni vijana wasio na mali. Tatizo la kutorejesha mikopo ni kukosekana kwa ajira kwa wahitimu wa elimu ya juu. Kambi ya Upinzani

inaishauri Serikali kutumia mfumo rafiki wa urejeshaji mikopo kwa kutumia technolojia ya benki na mitandao ya simu kama *M-PESA, TIGO PESA, Airtel Money* na kadhalika, kuwarahisishia wadaiwa walioko pembezoni mwa Dar es Salaam kwa kuainisha viwango vyatupaji kwa wadaiwa pamoja na Serikali kulitafutia ufumbuzi tatizo la ajira ili mikopo irejeshwe kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali kuhamishia shughuli za kiserikali Dodoma imekuwa na miaka mingi sana, na kauli hiyo ndiyo ilipelekeza kuundwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (*CDA*) kwa tangazo la Serikali Na. 230 la tarehe 12 Oktoba, 1973. Hadi mwaka huu ni miaka 39. Ni kweli kuna mipango ambayo inaweza kutumia muda wote huo kabla ya kutekelezwa na kuendelea kuitwa Mpango. Wakati huo huo Serikali hii inajenga mji mpya Kigamboni kule Dar es Salaam, kwanini nguvu hizo zisingewekezwa Dodoma kama kuna dhamira ya kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itangaze rasmi kuwa mpango huo umeshindwa kutekelezeka na hivyo ikubaliane na Sera na Mpango wa CHADEMA kuwa Dodoma iendelee kuwa Jiji la Elimu na Bunge, Dar es Salaam uwe ni mji Mkuu wa Biashara na Utendaji wa Shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ndiyo Wizara kiungo kati ya Serikali Kuu na wananchi (Halmashauri), hivyo ni ukweli ulio wazi kuwa mashauriano ya karibu kati ya Wizara mbalimbali zilizo Dar es Salaam ni muhimu sana katika kufanikisha taarifa kutoka juu hadi chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa TAMISEMI ndiyo Wizara kiunganishi na Wizara nyingine zote zilizopo Dar es Salaam, kwa namna moja au nyingine imekuwa ikiingia ikitumia gharama kubwa kwa ajili ya kufanya uratibu ili miongozo yote inayotolewa, Serikali Kuu iwafikie Watendaji walioko ngazi za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tufikirie kuwa kila siku gari liko safarini (posho ya Mkurugenzi na dereva, mafuta na uchakavu wa gari). Kwa umbali ni kilimeta 450 kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam, kwa magari ya *Land Cruiser* kwa safari hii litatumia lita 100 kwenda tu. Hivyo kwa mwezi mmoja wa siku 22 za kazi kwa safari ya kwenda na kurudi mafuta ni Sh. 9,680,000/= kwa mwaka mzima, kwa mafuta ni Sh.116,160,000/=. Hizi ni gharama za mafuta tu kwa gari moja. Hapo bado gharama za kuwawezesha Wakurugenzi au Maafisa kuishi Dodoma ama Dar es Salaam. Hii ni mojawapo ya sababu zinazosababisha fungu linaloombwa na TAMISEMI kwa ajili ya mafuta yanayoombwa kwa mwaka 2012/2013 kufika Sh. 709,887,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri Mkuu akihitimisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2011/2012 hapa Bungeni alisema, nanukuu: "Kwa maelekezo haya ya Mheshimiwa Rais, uamuzi wa kuhamia Dodoma hauna budi kutekelezwa. Kwa maana hiyo, hata kama fedha zimetengwa, napenda kuwahakikishia kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu itajengwa Dodoma. Aidha, Wizara zote ambazo zimetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi zianze kujenga Dodoma.

Jambo muhimu ni kuvuta subira. Tutaendelea kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais kwa lengo la kuhamia Dodoma kama ilivyokwishapangwa." Kambi ya Upinzani tunahoji utekelezaji wa kauli hii umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutangaza adhma yake ya kuhamishia shughuli zake Makao Makuu Dodoma toka mwaka 1973 ambayo ni miaka 39 sasa, lakini bado shughuli zake zote zinafanywa Dar es Salaam. Nchi nyingi hutaja miji yake mikuu kwenye katiba na kuitungia sheria maalum ya kuiongoza, hii inasaidia utendaji na maendeleo ya miji mikubwa kama Dar es Salaam kupata "*attention*" ya kutosha. Hii haipo kwa Tanzania. Dar es Salaam inayobeba majukumu yote ya "kimji mkuu" (Ikulu, Wizara 90%, Benki Kuu na Makao Makuu ya Benki zote, Balozi zote, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, Makao Makuu ya Vyombo vyta Ulinzi na Usalama na kadhalika.)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ina muundo wa kipekee duniani, ambapo kuna Halmashauri tatu za kiutendaji (Manispaa ya Ilala, Temeke, Kinondoni) na Halmashauri moja ya kiitifikasi, "*ceremonial*" inayoitwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na wala haina madaraka ya Jiji. Ina majukumu ya kuitambulisha Dar es Salaam kiitifikasi. Ili kujiendesha, imepewa mapato ya *UDA*, Soko la Kariakoo, *Ubungo Bus Terminal*, *DDC*. Halmashauri hii haina wananchi wala Madiwani. Inaundwa na Madiwani watatu watatu toka kila Manispaa, Mameya na Wabunge.

Kinachotokea ni kuifanya ifanye mambo shaghalabaghala kwa kuwa haina "*political responsibility*". Tarehe 30 Novemba, 2010 kupitia GN No 416/2010, Serikali ilivunja Halmashauri ya Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, Serikali imeendelea kupeleka fedha kwenye chombo ambacho hakipo. Kwa kushtuka na kuendesha mambo holela 3 Februari, 2012 kupitia GN No. 36/2012, Serikali imetangaza kuunda Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam bila kulihusisha Bunge. Hapa ndipo wameongeza tatizo badala ya kupunguza tatizo.

Sasa kwa kuwa ni dhahiri Serikali imeshindwa kuhamia Dodoma, sasa itangaze rasmi kuwa Dodoma ni Jiji la Bunge na Dar es Salaam itangazwe Mji Mkuu wa kiutawala na kibishara na itungwe Sheria Maalum ya utawala wa Dar es Salaam ili iwe na viongozi na Watendaji mahiri, wabunifu na wenye nguvu ya sheria ili mji huu upate heshima, uwe msafi, na huduma zifanane na hadhi ya majiji mengine duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu bado ni nchi ya Kilimo licha ya kwamba mchango wa sekta nzima ya Kilimo katika Pato la Taifa umeshuka mpaka asilimia 23.7 mwaka 2011 kutoka asilimia 24.1 mwaka 2010. Kushuka huku kwa mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa ni matokeo ya kuendelea kuperomoka kwa Sekta ya Kilimo na kuongezeka kwa kasi kwa Sekta ya huduma katika Uchumi wa nchi yetu.

Hata hivyo, Kilimo bado kimeendelea kuwa Sekta inayoendesha maisha ya Watanzania wengi, takribani asilimia 75 ya Wananchi wote. Hivyo, kitendawili cha

umasikini katika uchumi unaokua kitateguliwa na Sekta ya Kilimo na hivyo kuwaondoa Watanzania katika dimbwi la Umasikini. Mipango ya Uwekezaji katika Uchumi na Uwezeshaji wa wananchi ni lazima uzingatie Sekta Mama katika nchi yetu ambayo ni Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 umeshuhudia kuporomoka kwa kiasi kikubwa kwa uzalishaji kwenye mazao makuu ya chakula nchini ambayo ni mahindi na mpunga/mchele. Wakati uzalishaji wa mahindi umepungua kwa 3% kutoka tani milioni 4.5 mwaka 2010, mpaka milioni tani 4.3 mwaka 2011; uzalishaji wa mchele ulipungua kwa asilimia 14.1 kutoka milioni tani 1.7 mwaka 2010 mpaka milioni tani 1.4 mwaka 2011. Uzalishaji wa mazao mengine ulikuwa wa kuridhisha kiasi. Ni dhahiri kwamba uwezo wa nchi kuzalisha chakula ni mkubwa sana na hata mara 20 ya kiwango kinachozalishwa sasa. Tanzania inao uwezo wa kuzalisha chakula kwa matumizi ya nyumbani na hata kuuza nje ziada na kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa Serikali katika miundombinu ya Kilimo ili kuwezesha wananchi kuzalisha chakula kingi zaidi ni mdogo mno. Serikali imegubikwa na suala la Kilimo Kwanza na hasa Mpango wa *SAGCOT* kama mwarobaini wa kuongeza uzalishaji wa Kilimo. Kambi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba uzalishaji endelevu utakaoondoa umaskini vijijini ni uzalishaji utakaofanywa na wananchi wakulima wadogo wadogo na wa kati badala ya Mashirika makubwa ya kimataifa ambayo yanaendeshwa kwa lengo la kupata faida zaidi. Uzalishaji endelevu ni ule unaowafanya wananchi

wamiliki ardhi yao badala ya ule unaowafanya wananchi kuwa 'manamba' katika nchi yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao yote ya Biashara uliongezeka ingawa kwa baadhi ya mazao isipokuwa Karafuu, bei katika Soko la Dunia liliathiri sana thamani ya mauzo yetu nje. Mazao ya Kilimo yanachangia Dola za Kimarekani milioni 669 tu, yaani chini ya Dola za Kimarekani bilioni moja kwa mwaka. Ni dhahiri kwamba iwapo tukiongeza uzalishaji kilimo kinaweza kuchangia mara tatu ya sasa katika mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la Tumbaku ndiyo linaoongoza kwa mauzo nje likiingiza Dola za Kimarekani milioni 281, likifuatiwa na Kahawa kwa kuingiza Dola milioni 143, Korosho Dola milioni 107, Pamba Dola milioni 61.6, Chai Dola milioni 47.2 na Karafuu Dola milioni 29. Kwa mujibu wa taarifa wa hali ya kiuchumi katika nchi yetu toleo la mwisho ambalo Wabunge tumekabidhiwa, mauzo ya Katani katika Soko la Dunia yalikuwa ni madogo sana kiasi cha kutoonyeshwa katika Kitabu cha Hali ya Uchumi mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo tukiweka mkakati maalum wa kuongeza uzalishaji katika kilimo na kuongeza thamani hapa nchini, ni dhahiri kwamba tutaweza kuongeza mauzo yetu nje na kuwafanya wakulima wetu wapate fedha na kuweza kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa tuliyonayo ni kwamba mfumo wetu wa Kilimo cha

mazao ya biashara kimehodhiwa na Bodi za Mazao ambazo kazi na mipango yake inaelekea ni kunyonya (*extractive behaviour*) wakulima badala ya kuwaendeleza. Bodi za Mazao yote hapa nchini kama zilivyoundwa baada ya kuvunja Mamlaka za Mazao zimeonyesha kushindwa kabisa kusimamia Mazao yao. Mkulima ndio anaathirika na Bodi za Mazao kutokana na maamuzi yao ambayo hayazingatii haki za Wakulima na Bodi hizi kuongozwa kisiasa zaidi na makada wa CCM wakiwamo Wabunge kuliko utaalam. Ni hakika basi kuwa Chama cha Mapinduzi hakiwezi kukwepa lawama ya kilio cha wakulima nchi hii kwa kushindwa kuongoza Bodi hizi na kuzigeuza vitega uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma katika Sekta ya Kilimo ilitekelekezwa vibaya kiasi cha kutapanya hovyo mali za Taifa kwa kuza hovyo viwanda vilivyojengwa kwa mkakati maalum wa kulifanya Taifa kuongeza thamani ya Mazao, kuza mashamba ya Umma hovyo bila hata kujali wenyiji waliotoa ardhi kwa Shirika la NAFCO (rejea migogoro ya mashamba ya Basutu na Kapunga ambapo Serikali iliiza mpaka Kijiji na wananchi wake kwa mwekezaji) na kuachia mali nyingine za Umma bila uangalizi, (Mfano, ni vinu vyatatu kusaga nafaka katika Mkoa wa Iringa, Mwanza na Arusha). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba tuangalie upya namna tunavyoendesha Sekta ya Kilimo kuitia Bodi za Mazao. Ni lazima tuangalie upya majukumu ya Bodi za Mazao katika kuendeleza mazao wanayoyasimamia,

ikibidi kuondokana kabisa na Bodi za Mazao na kurejesha ushirika wenyewe nguvu unaoendeshwa na wananchi wenyewe bila kuingiliwa na wanasiasa. (*Makofi*)

Mifano ya Chama cha Ushirika cha Kanyovu kule Kigoma ni moja ya mifano inayoweza kutumika katika kuangalia upya usimamizi wa mazao yetu ya kilimo. Chama hiki kinajiendesha kibiashara, kimejenga kiwanda chake cha kukboa kahawa na hata kupata soko la kuuza '*specialty coffee*' moja kwa moja kwa makampuni makubwa kama *Sturbacks* huko Marekani kwa jina la *Gombe Coffee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama changu kilipotembelea Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara kabla ya Bunge hili la Bajeti, tumeshuhudia umasikini wa kutupwa wa wananchi wetu. Wananchi wa Lindi na Mtwara wangekuwa wanafahamu kwamba zao la Korosho ni zao la tatu kwa kuingiza fedha za kigeni nchini (Dola milioni 107 mwaka 2011) baada ya Tumbaku na Kahawa, hakika wasingekubali kubaki katika umasikini wa namna ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, juhudzi za Serikali ya Awamu ya Kwanza ya nchi yetu kujenga viwanda vya Korosho ili kuongeza thamani na kumfanya mwananchi apate fedha, zilikwamishwa na sera mbovu za ubinafsishaji. Katika Viwanda 12 vya korosho nchini, ni viwili tu vinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana korosho ya thamani ya zaidi ya Dola milioni 185 ilibaki kwenye maghala bila kuuzwa. Wakulima walipewa bei ndogo

ilhali bei katika Soko la Dunia ilipanda kutoka Dola 963 kwa tani mpaka Dola 1110 kwa tani. Bodi ya Korosho iliendelea na ukiritimba wa kutoa zabuni ya kuuza dawa ya *Sulphur* kwa wakulima kwa bei kubwa isiyoendana na uhalisia. Kambi ya Upinzani inataka kuwepo na mfumo bora wa soko la Korosho ikiwemo kuzuia kuuza nje korosho ghafi na kujenga viwanda vidogo vidogo vya kubangua korosho vijijini ambavyo mbali na kuongeza thamani ya zao la korosho, vitaongeza kwa kiasi kikubwa ajira kwani viwanda vya kubangua korosho ni "*labour intensive*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Waheshimiwa abunge wanaotoka Mikoa inayolima Pamba wakiongea kwa uchungu kuhusu bei ya Pamba. Ni dhahiri kwamba bei ya Pamba katika Soko la Dunia imeporomoka sana. Mara ya Mwisho tumeangalia Soko la *Liverpool* tumeona bei imefikia senti za Dola za Marekani 67 kwa Pauni moja. Hivyo, ni dhahiri kwamba Bei ya Pamba mwaka huu itakuwa ni mgogoro mkubwa sana. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke mkakati maalum ili kuepuka mkulima kuumizwa na wanunuzi wa Pamba ambao wengine ni wanasiasa. Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha mfumo maalum wa kuweka sawa bei za mazao (*Stabilization Fund*) ili kuhakikisha mkulima analindwa na kubadilika kwa bei katika Soko la Dunia. Hata hivyo, silaha kubwa kuliko zote za kudhibiti bei ni kuongeza thamani hapa nchini kwa kufufua viwanda vyote vya nguo na kutoa motisha maalum kwa wenye viwanda wa ndani ili wazalishe kwa kutumia malighafi za hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya uwekezaji nchini bado hayaridhishi kutokana na sababu mbalimbali. Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 Wizara iliweza kuanzisha kituo kimoja tu cha utoaji huduma kwenye Bandari ya Dar es Salaam, na bado mizigo imeendelea kukaa bandarini kutoka siku 12 - 13 mwezi Mei, 2011, hadi kufikia siku tisa mwezi Machi, 2012. (*Makofii*)

Jambo hili linafanya uwekezaji katika nchi yetu kuwa mgumu sana hasa kutokana na mizigo kukaa muda mrefu bandarini na hivyo wawekezaji kujikuta wanakaa muda mrefu bila kupata mizigo yao na hivyo kuchelewesha miradi ya wawekezaji. Pia wawekezaji wamejikuta wakiwa na vikwazo vyta kudumu katika barabara kuu wakati wa kusafirisha mizigo yao mbalimbali kutoka bandarini na hasa kutokana na kukosekana kwa usafiri wa reli nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Nchi, Uwekezaji na Uwezeshaji, ni kuwa kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 jumla ya Shilingi bilioni 9.9 zilitolewa kwa wawekezaji kwa ajili ya mradi wa kukuza ushindani wa Sekta Binafsi (*PSCP*), na fedha hizi walipewa wajasiriamali 2,780 na kupewa ruzuku ya mbegu na mitaji. Wakati huo huo jumla ya Shilingi bilioni 7.8 zilitolewa kwa kampuni 786 chini ya mpango uitwao programu ya ruzuku ya kuchangia (*Matching Grants Programme*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwepo mifuko mingi sana ambayo inasemekana kukusudia kuwezesha wananchi kushiriki shughuli za kiuchumi. Mifuko hii kama vile *MEF (Mwananchi Empowerment Fund)*, *JK Fund*

(Mabilioni ya Kikwete), *SELF*, *ECGS (Export Credit Guarantee Scheme)*, Dirisha la Kilimo (*TIB*), Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (*AGITF*) na kadhalika, imekuwa ikitoa mikopo na misaada mingi katika mfumo kwa usiri mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi hawaelewi uwepo wa Mifuko hii tukiwemo sisi Wabunge. Mifuko hii ni mingi mno inayofanya kazi inayofanana na ingeweza kuunganishwa na kuokoa fedha nyingi ambazo sasa zinaishia katika utawala. Mifuko hii vilevile inahudumia Watanzania na hata wasio Watanzania wanaouna mkono kwa njia moja au nyingine itikadi moja. Ubaguzi huu ni bora uangaliwe usilete madhara kwa umoja wetu kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inataka kujua utaratibu ambao umekuwa ukitumiwa na Serikali katika kuchagua wajasiriamali hawa na kampuni hizi, kwani ni kiasi kikubwa sana cha fedha za walipakodi kwa mabilioni ambacho kimekuwa kimetolewa. Hii itasaidia Watanzania wengine kujua njia wanazopaswa kutumia ili waweze kupata fedha hizi. Je, Kampuni zinazopaswa kupatiwa fedha hizi wanapaswa kuwa na sifa gani mahususi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) katika kipindi cha mwezi Januari, 2011 hadi Aprili, 2012 imetekeleza majukumu mbalimbali, mojawapo likiwa ni kuhamasisha wawekezaji kutoka nje ambapo waliweza kupata wawekezaji katika miradi mitatu ambayo ni mradi wa makaa ya mawe, mchuchuma na chuma liganga, mradi wa makaa ya

mawe Ngaka na mradi wa *Kilwa Energy Co. Ltd* unaotarajiwa kuwekeza katika kuzalisha umeme kiasi cha Megawati 318 kwa kutumia gesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na *World Investment Report, 2011*, mitaji kutoka nje imeongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 646 mwaka 2009 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 700 mwaka 2010. Hii ni sawa na ongezeko la Dola milioni 53 kwa mwaka mzima. Taarifa hii imekuja wakati ambapo nchi yetu imekuwa na wawekezaji kwenye Sekta ya Gesi na Mafuta ambao wamejitokeza katika kipindi husika. Waziri Mkuu – Mheshimiwa Mizengo Pinda aliwahi kusema, na nanukuu: “Tubadilishe tabia, itabidi tujitolee tu, kama vile mtu anataka kujua na tuwasaidie wakulima, wafugaji na wavuvi... katika bajeti tusiulizane, tuelekeze nguvu katika maeneo hayo...” *Akifungua mikutano wa siku tatu wa wadau wa mifugo mjini Dodoma (Jumatatu, Sept. 28, 2009)*.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, taarifa za “*Doing Business Report*”, inayoandaliwa na Benki ya Dunia, pamoja na ile ya “*Global Competitiveness Report*”, inayoandaliwa na *World Economic Forum*, zinaonyesha kuwa Tanzania haifanyi vizuri katika kujenga mazingira ya kuvutia wawekezaji. Hali hii inachangiwa sana na urasimu wa Taasisi za Serikali katika kuwashudumia wawekezaji ili kutoa huduma bora na za haraka, ukosefu wa miundombinu kama maji, barabara, umeme, usafiri na hasa ikizingatiwa kuwa ikishafika saa 12.00 jioni uchumi wa nchi yetu huwa unalala, kwani hakuna usafiri ama wa ndege au mabasi kwa muda wa usiku, na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inahoji, kama kwa mwaka mzima mitaji inaongezeka kwa kiwango hicho, kuna haja gani ya Serikali kuendelea kusitiza kuwa ziara za Mheshimiwa Rais nje ya nchi zimekuwa na mafanikio makubwa ya kuvutia wawekezaji? Je ni kiasi gani cha fedha kilitumika katika mwaka husika kwa ajili ya ziara za Mheshimiwa Rais na viongozi wengine nje ya nchi kwa ajili ya kutafuta wawekezaji?

Hata kama Mheshimiwa Raisi akienda nje kila siku, kama hatujaboresha mazingira ya uwekezaji katika nchi yetu, tutakuwa tunaendeleza matumizi mabaya ya rasilimali za Taifa letu tu. Pamoja na Mheshimiwa Rais kwenda G8 na kurejea akisema kuwa tumepata mafanikio makubwa, lakini taarifa ya Benki ya Dunia ya Mazingira ya kufanya biashara inaonyesha kuwa Tanzania mwaka 2011 ilikuwa ya 125, na mwaka huu 2012 imekuwa nafasi ya 127, huku ni kurudi nyuma, na hii ni dalili ya wazi kuwa kwenda nje ya nchi siyo suluhisho la kupata wawekezaji, bali njia pekee ni kuboresha mazingira yetu ya uwekezaji hasa kwa kuimarisha miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndiyo maneno ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yanakuwa na maana. Nanukuu: "Kama Bunge, lakini mmoja mmoja kama Watumishi wa Wmma, tunao wajibu mkubwa sana wa kuishi na kutenda kwa mfano. Tujiepushe na tamaa zinazoweza kuliingizia Taifa hili hasara kubwa."

**Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kauli ya  
Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuhitimisha mjadala wa**

**Richmond, Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge,  
tarehe 10 Februari, 2010.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** nchi yetu sasa imebarikiwa kuhusiana na suala la Mafuta na gesi asilia. Hivi sasa kuna Mikataba 29 na leseni 18 zimetolewa kwa Kampuni mbalimbali za Kimataifa kutafuta mafuta na gesi asilia kwa niaba ya Shirika la Petroli Tanzania (*TPDC*). Kwa taarifa za *TPDC*, hivi sasa nchi yetu ina utajiri wa gesi asilia wa jumla futi za ujazo trillioni 29.5 (*Trillion Cubic Feet – TCF*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bei ya sasa ya gesi katika Soko la Dunia, Tanzania inaweza kuwa na gesi asilia yenye thamani kati ya zaidi ya Dola za Kimarekani trillioni 3.5 kwa kuchukua kiwango cha chini cha '*recoverable gas*' na trillioni sita. Ugunduzi zaidi bado unaendelea ambapo Kampuni za *BG/Ophir*, *Ophir/Mubadala* na *Shell/Petrobras* zinaendelea na zoezi la utafutaji zaidi. Katika eneo la Ziwa Tanganyika Kampuni ya *Beach Petroleum* imeanza zoezi la kukusanya, '*seismic data*.'

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la vitalu namba 9, 10, 11 na 12 Mashariki mwa Kisiwa cha Unguja na eneo la Pemba *channel*, shughuli za utafutaji bado hazijaanza kufanyika kutohana na mgogoro usiokwisha wa suala la mafuta na gesi kuwa suala la Muungano au hapana. Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kuitahadharisha Serikali kwamba masuala ya utafutaji wa mafuta na gesi ni masuala ya Msimu na hivyo kuchelewa kutoa maamuzi kuhusu suala la mafuta na gesi kuwa suala la Muungano au la

kunaweza kuondoa uwezekano wa eneo hili la Zanzibar kufanya zoezi la utafutaji hivi karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatoa mapendekezo yafuatayo katika kuimarisha na kuboresha sekta ya gesi na mafuta hapa nchini ili kuitayarisha nchi kwa utajiri huu mkubwa:-

(i) Suala la mafuta na gesi ni muhimu sana likawekewa utaratibu maalum na hatua zichukuliwe haraka ili kuandaa sera na sheria ya sekta ya gesi itakayosimamia uendeshaji wa sekta hii muhimu kwa uchumi wa Taifa. Muswada wa sheria husika uwasilishwe kwenye Bunge mapema iwezekanavyo. Kumekuwa na ahadi nyingi za Serikali kuhusu jambo hili, sasa utekelezaji ufanyike.

(ii) Pawepo na Mpango Maalum wa Maendeleo ya Gesi (*Gas Master Plan*) nchini kuanzia utafutaji, uchimbaji na umuhimu wa gesi asilia kwa manufaa ya Taifa na kukuza uchumi wetu. Lengo ni kujua ni gesi kiasi gani tutaitumia kuzalisha Umeme, kuzalisha Mbolea na bidhaa nyingine, matumizi ya viwandani na kiasi gani tutauza nje ya nchi.

(iii) Wananchi wanaozunguka maeneo yanayopatikana au yanayopitia gesi asili wawe sehemu ya mipango ya maendeleo ya gesi asili na hivyo kunufaika na matumizi ya gesi badala ya kuachwa, hali inayoleta manung'uniko na tishio la uendelevu wa sekta husika na hasa ikizingatiwa kuwa uwekezaji unaofanywa katika sekta hii kama wananchi hawataona kuwa na wao ni wafaidika ni rahisi sana

kuweza kuhujumu miundombinu hii na kuhatarisha usalama na hata uhai wa wananchi wengine.

(iv) Ujenzi wa miundombinu ya gesi uwe unazingatia mahitaji ya muda mrefu ili kupunguza gharama na kuondokana na uhaba na uharibifu wa maliasili, mfano, bomba la Songosongo liliwekwa bila kuzingatia mahitaji asili ya gesi na hivyo kujikuta kuwa wanashindwa kusafirisha gesi ya kutosha kutumiwa na wahitaji wote.

(v) Tuwekeze kwenye kuwapa elimu na maarifa vijana wa Kitanzania na hasa kwenye Sekta ya Gesi ili waweze kupata utaalamu wa jinsi ya kusimamia sekta hii kama ambavyo nchi majirani zetu wa Uganda na Msumbiji wamefanya kwa kuwapeleka vijana wao nje ya nchi ili kupata utaalamu juu ya uendeshaji wa sekta hii.

Tunasisitiza umuhimu wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Mtwara ambacho kitajikita kuwaandaa Watanzania kuwa wataalamu wa Sekta ya Mafuta na Gesi kwa nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Ileleweke Chuo hiki hakitahusika na masomo ya Sayansi peke yake, bali pia Sheria, Uchumi na Menejimenti ili kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa na rasilimali watu ya kutosha. Mradi huu wa Chuo Kikuu cha Mtwara uanze mara moja. (*Makofi*)

(vi) Serikali iliahidi kwa Shirika la Fedha la Kimataifa kwamba Sheria ya Usimamizi Bora wa Fedha za Mafuta na Gesi (*Petroleum Revenue Management Act*) italetwa Bungeni mnamo mwezi Novemba.

Kambi ya Upinzani inasisitiza kwamba Sheria hii illetwe haraka ili kuweka wazi mapato yatokanayo na utajiri huu na namna bora ya kutumia fedha hizi ili kuzuia uchumi kuathiriwa na pia kuzuia ufisadi. Hatutaki Tanzania iwe kama nchi nyingine za Kiafrika ambazo utajiri wa mafuta na gesi umekuwa ni laana badala ya neema.

(vii) Serikali iweke mazingira bora ya kujenga uwezo wa Watanzania kutoa huduma kwenye kila hatua ya utafutaji wa mafuta na gesi. Hivi sasa kuna zaidi ya wageni 1,200 kwenye meli za kutafuta mafuta na gesi katika Pwani ya Mtwara, Lindi na Pwani. Kwa masikitiko makubwa sana, wageni hawa wanakula hata nyanya, mchicha na vitunguu kutoka nje ya Tanzania.

(viii) Vile vile tudhibiti makampuni ya Ulinzi kutoka nje kuwa na silaha kali kali kwa kujenga uwezo wa Jeshi letu la Majini (*Navy*) ili liwe na kikosi maalumu kwa ajili ya kulinda meli za kutafuta mafuta na gesi na Makampuni haya yatozwe tozo maalum. Ni hatari sana makampuni ya kigeni kuwa na silaha kubwa ndani ya ramani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Freeman Mbewe kwa kuwasilisha hotuba yako kwa niaba ya Kamabi ya Upinzani na nakushukuru kwa kuzingatia muda.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee kama nilivyokuwa nimesema hapo awali, nilishaanza kuwataja wachangiaji wa mwanzo, na bila kupoteza muda, sasa naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Michael Laizer na Mheshimiwa Innocent Kalogeris ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi nami nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa Bungeni kwa sababu nilikuwa namuuguza Mama yangu na mpaka sasa bado yupo hospitalini lakini nawashukuru sana Madaktari wanaomtibu pamoja na Ndugu zangu ambao wanamsaidia na wajukuu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hotuba ya Waziri Mkuu, kwa kweli ni nzuri sana na nampongeza hasa kwa kukumbuka mifugo ambapo Mheshimiwa Rais alikubali kuwapa kifuta machozi wananchi wa Jimbo langu na wachache wamepata; lakini bado kuna wananchi wengi sana wanasubiri mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kuna wafanyabiashara ambao wamenunua mifugo kwa ajili ya Serikali kuwagawia wananchi na mpaka sasa mifugo iko kwa wale wafanyabiashara, wamesimamisha biashara hiyo kwa ajili ya hiyo mifugo na hawakuwa na lengo la kufuga bali walikuwa na lengo la hawa mifugo kugawanywa kwa walengwa.

Naomba Serikali izingatie katika bajeti hii ili wale wafanyabiashara ambao wamenunua mifugo wapewe fedha na mifugo igawanywe kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchagia suala la Halmashauri. Halmashauri zetu ziko hoi na nasema kwamba TAMISEMI imechangia kuua Halmashauri na niseme kwa sababu gani. Serikali imegawa maeneo ya utawala tukawa na Kata nyingi, tukawa na Vijiji vingi, lakini Vijiji na Kata havina Watendaji na huku unapeleka fedha kwa ajili ya miradi iliyoko Kijijini unawakuta watu wawili ambao wanasmamia Vijiji.

Unamkuta Mtendaji hakuajiriwa, amekaimishwa tu kwa muda, ni mtu ambaye sio mtaalam, ndiye anasimamia fedha za Halmashauri. Mtu mwingine ni Mwenyekiti ambaye halipwi, hata posho hana, ndiye anasimamia miradi ya Vijiji na tumepeleka fedha nyingi sana Vijijini. Kama tunataka kuimarisha Halmashauri na kuondokana na hizi hati tunazosema ni chafu, Halmashauri ziruhusiwe kuajiri watendaji. Tena nashauri hiyo Sheria ambayo zamani iliwakataza Halmashauri kuajiri, irekebishwe sasa na Halmashauri waruhusiwe kuajiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni huyu Mwenyekiti ambaye ni msimamizi wa Kijiji, alipwe. Wenyeviti wote walipwe, kama tunataka kuimarisha Vijiji vyetu. Hawa Wenyeviti wanafanya kazi kubwa sana, wanastahili malipo na hii Serikali inaweza kulipa kabisa hawa Wenyeviti wa Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuligusia ni suala la mgawanyo wa fedha.

Ukiangalia Halmashauri nyingine, zinapata fedha kidogo sana, ukiangalia Halmashauri ya Longido katika mgawanyo wa fedha za Serikali, sijui kigezo gani kilichosababisha Halmashauri ya Longido ipate fedha kidogo sana halafu kwanza hizo kidogo haziji kwa wakati. Naomba iangaliwe kwa sababu nilikuwa napitia kitabu hiki cha majedwali nikaona kana kwamba tumenyanyasika. Fedha ni kidogo sana tulizopangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni Mabaraza ya Kata. Mabaraza ya Kata ni muhimu sana, lakini imewekwa tu kisheria ikaachwa, hawana vitendea kazi, hawana hata elimu, ni kitengo tu kilicho sema kwamba kuwepo na Mabaraza ya Kata ikaishia hapo. Hata Ofisi wanayofanya kazi, hata wale Wajumbe wanajua tu kwamba ni Wajumbe wa Baraza la Kata, lakini hawajui majukumu yao. Hiki ni chombo muhimu sana, naomba kiboreshwe, na wale Wajumbe nao wawe wanapata posho ili waweze kuendesha hayo Mabaraza ya Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia na Makatibu Tarafa. Makatibu Tarafa wanasimamia sana shughuli za maendeleo Vijiji. Pamoja na kwamba wapo katika Ofisi ya *DC*, lakini ukiangalia kwa upande wa Halmashauri, Halmashauri haiwatambui hao watu, lakini ni watu wanaofanya kazi kubwa sana katika Vijiji. Naomba utaratibu uwepo, Halmashauri nazo ziwatambue kwamba Makatibu Tarafa ni watu muhimu sana katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku moja nilimwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Madiwani ambao Serikali imekuja kutuomba tulipokuwa Bunge lile, kwamba wawepo na Madiwani ambao watachaguliwa kwa kila Halmashauri Madiwani watatu, tukakubali, lakini haijawahi kuleta tena sheria kwamba hao Madiwani imeshindikana. Ningependa Waziri Mkuu anijibu tena leo kwamba wale Madiwani ni kwamba hawafai tena kuwepo au imekuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda umekwisha, nizungumzie suala la rada. Naomba Serikali kuhusu fedha za rada zielekezwe katika ujenzi wa nyumba za Walimu, hiyo ndiyo *priority* kubwa sana ambayo tatizo kubwa la nyumba za walimu katika maeneo mengi walimu wamepelekwa, wamerudishwa kwa sababu hakuna nyumba za Walimu.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nadhani tatizo la nyumba za Walimu siyo Longido tu, hata katika Majimbo yenu, hizi fedha za rada kama tunataka zitumike vizuri na ziwe ni kumbukumbu, isinunue vitabu wala madawati, yote ipelekwe kwenye nyumba za Walimu kwa sababu kero hiyo ya nyumba za Walimu itapungua. Haishi, lakini itapungua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la fedha za Mheshimiwa Rais, JK. Fedha za mikopo. Tulipangiwa sisi Shilingi milioni 250 lakini hizo fedha ziko kwenye benki, hazijatumika. Mpaka sasa ni mabenki tu ndiyo wanapata faida, wanatumia. Naomba zipewe kwa vijana wakope hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwani siku moja tulikuwa tumeka Wabunge watatu wa Mkoa wa Kilimanjaro, mimi, Mheshimiwa Freeman Mbewe kaka yangu na Mheshimiwa Mwanri tukasema Mheshimiwa Rais ametutendea haki kwa kutuchagulia na kutuletea Mkuu wa Mkoa ambaye anafaa Kilimanjaro. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusoma Katiba, sehemu ya II, Ibara ya 8 (b) na (c); lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi. Serikali itawajibika kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kwa masikitiko sana. Serikali kwa takribani miaka miwili, haikufanya kama ilivyoandika kwenye Katiba, kwa wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu lina msitu mkubwa wa asili unaitwa Msitu wa Shengena. Msitu wa Shengena, unazaa mito minne. Mto wa kwanza unaitwa Saseni, mto wa pili unaitwa Yongoma, mto wa tatu unaitwa Hingilili, mto wa nne unaitwa Nakombo. Msitu wa Shengena, ndio chanzo kikuu cha mvua Wilayani Same.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani miaka miwili sasa, kumekuwa kuna majangili wa kutoka Tanzania nzima ambao wamevamia Msitu wa Shengena wakivuna dhahabu. Wanavuna dhahabu kwenye

msitu ule ambao ni mkubwa, ni mnene, una miti mikubwa sana kwa njia ambayo, mimi sio mwanasayansi, wanakausha ile miti kwa kutumia kemikali, miti inakauka yenyewe, wanakwenda wanasukuma tu ile miti, wanavuna dhahabu baada ya ile miti kuanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya utafiti wa kina, nimetengeneza sinema ya hali halisi ya Msitu wa Shengena. Sinema hii nitaigawa kwa Viongozi Wakuu wa Serikali, nitawataja hapa, ili waone ni kiasi gani wanapowapa watu dhamana ya kusimamia Wizara kama ya Maliasili na Utalii, watu wale wanajinufaisha wao, wanaua wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwangalie tarehe nitakazozizungumza; tarehe 23 Desemba, 2012, Waziri wa Utalii na Maliasili, utamwona kwenye hii sinema niliyotengeneza, alikwenda kuona hali halisi. Wakati huo ndiyo uharibifu huo ulikuwa unaanza. Aliona ule uharibifu na utamwona katika hii sinema yuko na Viongozi wengine kama 20 kutoka Wizarani kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 wananchi waliendelea kupiga kelele, Serikali haikuchukua hatua yoyote. Mimi mwenyewe, nakumbuka kuongea na Afisa wa Maliasili na Utalii upande wa Misitu, akiitwa Msusa. Naweza nikawa nimekosea hilo jina kidogo, ananiambia kwenye simu Mheshimiwa Anne Kilango, hapa Ofisini kwangu kuna wananchi wako. Nikamwambia wamefuata nini? Ananiambia, wametoka Misitu wa Shengena. Nikamwambia Msusa, hili jambo la Misitu wa Shengena, mbona Waziri wako

alishakwenda akaona? Nikamwona mwenyewe kwanye *ITV*, kwa nini hamlishughulikii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 mzima hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namwangalia kuku mwenye vifaranga. Kila wakati anafanya hivi...

*(Hapa Msemaji alionesha ishara ya kuku akitanua mabawa)*

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Anakuwa mkali, kumbe ni kwa sababu anaogopa mwewe na yeye ana vifaranga. Mimi ni mkali, watu wananiita mkali, kwa sababu ya kazi. Sipendi mambo ambayo yanaharibu haki ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu takribani miaka miwili wamekuwa wakitumia maji yenye kemikali. Sina uhakika kwamba, wataendelea kuishi, sina uhakika. Mvua zimepungua, vyanzo vyama, mito yote minne inatirisha, maji mekundu na wananchi wanakunywa maji hayo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miti ni mingi sana, ukiangalia kwenye hii sinema niliyoitengeneza, miti mingi imeshakauka. Inangoja wale watu wende waisukume tu wachote dhahabu kutoka kwenye mizizi. Wananchi wamenitura haya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba unisikilize vizuri, Serikali ifanye kila linalowezekana haraka sana, leo hii kusimamisha uharibifu unaofanyika Shengena. La pili, Serikali ifanye kila linalowezekana kuurudisha Msitu wa

Shengena, kwenye umbile lake la mwanzoni kama ulivyokuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe, kwa wale ambao wana kumbukumbu, mwaka 1952 wananchi wa Meru walikwenda *UNO* kudai mambo yao ya ardhi. Nina uhakika Mheshimiwa Mbunge alikuwa hajazaliwa. Mwaka 1952, walikwenda *UNO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko, sasa hivi wananchi wa Same wanafanya taratibu za kwenda kushitaki Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi *UN*, na anayeratibu safari hii anaitwa Greyson Kigonti. Naomba kupitia Bunge hili nimwambie, hakuna haja ya kwenda *UNO*. *UNO* ni mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetengeneza kanda hizi, ziko tatu. Naomba kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa unyenyekevu mkubwa, moja ifike kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili ajue jinsi watu anaowateuwa akawapa nafasi kubwa, wanavyofanya mambo ya ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja iende...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne, zinapitia kwenye Kiti.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zitapitia kwenye Kiti chako. Naelewa Mheshimiwa. Ya pili, iende kwa Makamu wa Rais kwa sababu ni suala la mazingira; ya tatu, iende kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijiulize na tuulizane wote hapa: Hivi Mheshimiwa Waziri

alipokwenda mwaka 2010, akaona kile kitu, kwa nini alinyamaza kimya mpaka leo? Mimi nilikwenda mwezi wa Tano nikaona kile kitendo. Ni kitu kibaya ambacho ndugu zangu, huwezi kuvumulia ukakiangalia. Huwezi! Ni lazima utalia. Baada ya mimi kwenda, eti ndiyo namwona Kamishna, anaitwa sijui Dkt. Kilahama sijui, anakwenda kufanya nini? Juzi mwezi wa Sita tarehe 10, anakwenda baada ya kuona Mbunge wa Same Mashariki nimekwenda. Alikwenda kufanya nini? Wakati alijua lile tatizo tangu mwaka 2010? Kwa nini hakulishughulikia? Anakwenda sasa wakati mchicha umelingana na mbuyu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni kubwa sana. Wananchi wangu wamekunyuwa kemikali kwa miaka miwili. Uhai wa wananchi wangu sasa hivi ni tete. Ukiangalia sinema hii utaona wananchi wangu wanavyolia, wanavyolalama, wanavyolalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina swali kubwa sana, ninaomba kuuliza. Wakati Mkuu wangu wa Mkoa alipokuja Mkoa wa Kilimanjaro, kitu cha kwanza, aliomba kupelekwa Shengena. Swali langu ni hili, Waziri Mkuu nitaomba ulifanyie utafiti, aliyekuwa mwenyeji wake hakumpeleka Shengena, akampeleka mahali pengine. Kwa nini alimficha Mkuu wa Mkoa asione hili tatizo langu la Shengena? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hajui mambo haya yanayofanyika. Waziri Mkuu, hajui mambo yanayofanyika. Makamu wa Rais hajui, lakini viongozi wenzetu wanaopewa dhamana ya kuiongoza Serikali yetu, wengine sio waadilifu. Naomba Serikali

iwachukulie hatua hawa wote waliowafikisha wananchi wangu kwenye hali hii. Tutakuwa tunasikiliza, wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo mnaweza mkaliona ni dogo kwa sababu, hamjaona hii sinema. Lakini mkiiiona hii sinema, mimi mwenyewe nilichukua siku nzima kuitengeneza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba vielelezo vyangu vifike. Ni hizi kanda tatu, kuna Gazeti la Nipashe...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale mlangoni nimeacha...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ya pili.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale mlangoni nimecha machepe...

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Kilango. Waheshimiwa Wabunge, anayefuata katika orodha yangu ni Mheshimiwa Luckson Mwanjale. Naomba vijana, Wahudumu wa Bunge, wanilettee hivyo vielelezo vilivyotolewa na Mheshimiwa Kilango. Mheshimiwa Luckson Mwanjale, tafadhali.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia

katika Hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini la kwanza ambalo ninataka kulisema katika mchango wangu, ilikuwa katika mambo ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi hapa Tanzania, imekuwa ni mikubwa mno kiasi kwamba, hata wananchi wanashindwa ni wapi watapata majibu yao. Kumekuwa na migogoro mingi, kumekuwa na upungufu wa fidia kwa watu ambao wamechukuliwa ardhi yao. Migogoro hiyo ni mara nyingi nafikiri tumeisikia ikisemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano kwangu kule, mgogoro wa ardhi kati ya *TANAPA* na wananchi wa Kata ya Irungu, umekuwa ni mkubwa sana. Nimejaribu kuongea na nilikwenda kwa Waziri kumweleza, Waziri alikuja kule, lakini kwa bahati mbaya hakupata nafasi ya kwenda kuonana na wananchi. Lakini akasema kwamba, angeunda Tume ya kwenda kusikiliza maoni au kero za wananchi, lakini mpaka leo hii hakuna. Lakini hii siyo upande wangu tu, najua migogoro iko kila mahali nchi hii, na kila unaposikiliza redio, unasikia migogoro ilivyokuwa mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kuna mgogoro wa Irungu, kuna mgogoro wa pale *Airport*, kila mahali imekuwa shida. Naiomba Serikali, ijaribu kuchukua hatua za haraka, ili tusiwape hasira hawa wananchi ambao kwa kweli ni kero kubwa sana kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo ninataka kulizungumzia katika Hotuba hii, ilikuwa ni nilitaka niihoji tu Serikali, kumekuwa na miradi pale Mbeya, ambayo imesuasua sana; kumekuwa na

Uwanja wa Ndege wa Songwe, pamoja na kwamba, hela wanasema zimetengwa, kumekuwa na barabara ya kutoka Mbeya kuelekea Lwanjewa mpaka Chunya. Miradi hii ilianza vizuri sana, lakini hatimaye katikati ikasitishwa. Wale Makandarasi wote wamehama. Sasa ninaomba niiulize Serikali, inatoa tamko gani juu ya miradi hii mikubwa ambayo ilianzishwa na ilitengewa hela, bila shaka? Na hii miradi imesababisha hela nyingi sana zitumike kwa sababu, kazi yake haijakamilika kwa wakati wake. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Serikali ijaribu kunieleza hapo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nilitaka nizungumzie kule kwangu, barabara ya Isyonje mpaka Makete na barabara ya kutoka Mbalizi kwenda lleje, ni barabara ambazo ziko katika Kanda ambayo mvua inanyesha mara nyingi. Pengine pesa ambazo zinatengwa kwa ajili ya barabara hizi zimekuwa ni ndogo wakitegemea kwamba, zinaweza kupitika wakati wote. Lakini mvua inanyesha kwa muda mrefu, mvua inasimama kwa miezi michache na hivyo kusababisha kwamba, hata ile hela ambayo wametenga kwa ajili ya kutengeneza barabara hizo, zisiweze kukamilisha kazi. Nilikuwa ninaomba Wizara inapotenga hela kwa ajili ya kutengeneza barabara hizi ambazo bahati mbaya zinakumbwa na wingi wa mvua pale, basi zitengwe hela nyingi zaidi. Hilo lilikuwa ni ombi langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili lilikuwa ni kuhusu maji. Tumepiga kelele sana hapa Bungeni kuhusu maji. Hasa miradi hii ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia. Hii miradi kwa kweli haijawa rafiki sana na wananchi. Kila wakati tumepiga kelele, ni kwa nini

hii miradi haikamiliki wala haizungumzwi? Lakini mwisho wake tunaishia kumalizia hapa tu. Mradi kwa mfano wa Iwindi, ni mradi ambao hata kabla sijawa Mbunge mimi, wameuzungumzia, sijui umetengewa hela! Lakini mpaka leo hii ninapozungumza ule mradi wala hata hela haujatengewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali, pia inipatie majibu kuhusu mradi huu. Lakini kuna miradi mingi ya maji ambayo inakabiliwa na tatizo hilo. Vijiji vingi, hivi vijiji 10 ambavyo walisema, kuna mradi wa kutoka Mbawi, Jojo, lakini mradi ambao umekaa zaidi ya miaka sita, saba, nao hatujui kama lini utaanza kutumika. Wamefanya tathmini, lakini utekelezaji wake umekuwa ni mdogo mno. Nilikuwa naomba Serikali ijitahidi kukamilisha hiyo miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mradi mwingine ambao ningeweza kuusema hapa, ni mradi wa Zahanati. Sisi kama Wanasiasa, tumehamasisha wananchi wajenge Zahanati kila Kijiji, lakini kila wakijenga ikifika mtambaa wa panya, hela hazipo. Nilipokuwa nikisoma makabrasha au vitabu hivi vyahaja zote ambazo zimewasilishwa, sioni kwamba kuna hela ambayo imetengwa rasmi kwa ajili ya kukamilisha Zahanati hizi. Sasa hii kazi itakwisha lini na hela zitapatikana lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi Serikali iangalie, kwa sababu, mwisho tunawahamasisha wananchi wanajenga, halafu wanasubiri, hela hakuna. Wanasubiri kwa muda mrefu na hela hazipo za kuweza kukamilisha kazi ile. Huku tunahitaji kila Kijiji kiwe na Zahanati, kila Kata iwe na Kituo cha Afya. Kama hela

hazitatengwa za kutosha kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo, tutawafanya wananchi wawe na hasira. Kwa sababu, wamejenga nyumba imekwisha, halafu inakaa miaka miwili, mitatu. Kule kwangu, kuna Zahanati nyingi ambazo zimekwisha, lakini zimekosa pesa. Nilikuwa ninaomba Serikali iliangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo nilikuwa naomba nilizungumzie hapa, ilikuwa ni kuhusu ni tamko la Serikali ambalo lilitoka hapa Bungeni, kuhusu ukamilishaji wa ufungaji au kupeleka umeme katika viji, wa *REA*. Nafikiri ni Mabunge mawili yaliyopita. Hapa Waziri alitamka akatoa tamko kwamba, kazi hiyo ya kufunga umeme itakamilika tarehe 8 Mei. Lakini mpaka leo hii nasema, kazi hiyo haijakamilika na wananchi wanasubiri kwamba umeme ule utafunguliwa. Lakini wapi? Hauwashwi na *transformer* hazijawekwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa wanaohusika, wajaribu kuisukuma hii kazi iweze kukamilika, kwa sababu, wananchi mwisho wanasubiri, halafu hawaoni matokeo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine linalofuata, ilikuwa ni kuhusu mambo ya umwagiliaji mashambani. Sera ya Umwagiliaji imekuwa tunazungumza hapa Bungeni sana, lakini tunaona kuna maeneo mengi, mengine ambayo yameainishwa kwa ajili ya kuweza kukamilisha kazi ya kumwagilia, lakini Serikali pia inatenga fedha kidogo. Hii kazi ya umwagiliaji, kuna maeneo mengi ambayo yangesaidia kuweza kujikomboa kwa chakula nchi hii. Lakini suala la Sera ya Umwagiliaji limekuwa dogo sana, ninaomba Serikali

iliangalie na ikiwezekana, basi iweze kutenga fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kuzungumza ilikuwa ni kuhusu mazingira. Inaelekea Serikali kuhusu mazingira, imekuwa na msukumo mdogo sana. Mazingira yanazidi kuharibika na hakuna hata taasisi moja ambayo inashughulikia. Naomba huko katika Halmashauri, kuna vikundi mbalimbali ambavyo vinashughulikia kuhamasisha mazingira, lakini vingepewa uwezo kama ingewezekana. Serikali iwasadie, maana wanasaidia, wanataka kui-*support* Serikali, lakini wao wanashindwa nguvu, hawana vitendea kazi, hawana pesa za kuweza kuwahamasisha wananchi kwa ajili, ya mazingira. Naomba suala la mazingira, Serikali ilitilie mkazo, kwa sababu, tukishaharibu mazingira, kuja kurudisha tena ni kazi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumze kidogo kuhusu mambo ya kahawa. Nimepigiwa simu na Mwenyekiti wangu, hasa kuhusu mambo ya kahawa. Baadhi ya Madiwani wengine, wanasema kwamba, kwa kweli, wananchi wanalamika, kwa nini Kanuni za kumruhusu mtu anunue kahawa mbichi? Zipo? Maana mwisho, sasa hivi watu wameanza kukata hata mamiti kwenye mashamba ya kahawa, wanakwenda kuchuma. Kwa sababu, kila mmoja anakuwa kama mkulima wa kahawa maana kila mmoja anaruhusiwa kuuza kahawa. Naiomba Serikali iliangalie hili, ni suala gumu sana, ni suala ambalo ni zito, linahitaji kwa kweli, uangalizi wa hali ya juu. Tukiruhusu kununua kahawa mbichi, maana yake ni kwamba, kahawa hii itakuwa inaibiwa mashambani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iangalie suala hili na ikiwezekana isitishe hizo kanuni, ijadiliwe upya, ili wananchi waweze kufaidi mauzo ya kahawa. Tunasema tunataka kuongeza thamani ya mazao, lakini mwisho tena tunawapunguzia thamani ya mazao, maana yake ni nini.

Baada ya hapo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ingawa wewe leo umesahau kutuombea, lakini tunakushukuru. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kuchangia, naomba nimwite sasa Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi ajiandae.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeneweza kuniipa afya bora na kuniwezesha leo kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, napenda niishukuru Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kuona tatizo lililotokea katika Tarafa ya Ikwiriri ya mgogoro baina ya wakulima na wafugaji kwa makusudi kabisa kuamua kwenda kuangalia Ikwiriri kuangalia hali halisi na kupata maoni kutoka kwa wakulima na hao wananchi wanakaa katika Tarafa ya Ikwiriri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yako ambayo inaongozwa na Mheshimiwa David Homeli Mwakyusa, lakini kwa msafara ule iliongozwa na Prof. Peter Msolla, nashukuru kwa ziara yenu ya Ikwiriri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapa pole wakazi wote wa Ikwiriri ambao wameathirika kwa namna moja au nyingine kutokana na machafuko yale ambayo yametokana na bugudha za wakulima na wafugaji. Poleni, Mwenyezi Mungu atawapa afya njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo mimi nataka niende katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ukurasa wa 24 na 25. Katika ukurasa wa 24, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza wazi suala la mifugo na ameelezea ile sheria namba 13 na katika sheria ile yameelezwa mambo mengi sana mazuri, ambayo Serikali hii sikivu kama wangeyatimiza, basi migogoro baina ya wafugaji na wakulima wala isingekuwepo tena katika Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria ile pia hata kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Mifugo cha mwaka jana cha Mheshimiwa David Mathayo, alieleza vizuri sana zile sheria na taratibu ambazo zinatakiwa zifuatwe pamoja na wafugaji ili sasa kutoa au kutokuwepo na migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Rufiji, mgogoro wa wakulima na wafugaji Rufiji, nasema dhahiri kwamba umesababishwa kwa makusudi na Serikali hii sikivu ya Chama cha Mapinduzi ambayo inajigeuza kuwa ni kiziwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kitu kama hicho kwa sababu mwaka jana, 2011 wakati Serikali inataka kupeleka mifugo Rufiji, mwaka 2006 ilimwezesha Waziri

wa Mifugo ambaye kipindi kile alikuwa Naibu Waziri – Mheshimiwa Dkt. David Mathayo kwenda Rufiji kueleza kwamba mifugo sasa inataka kuingia na alieleza wazi kwamba itafikia takribani ya 50,000. Lakini Mheshimiwa Waziri alikwenda mbali zaidi, alieza kwamba Serikali imejipanga kikamilifu kabisa katika kuhakikisha kwamba wanajenga miundombinu ambayo ni malambo, mabwawa, majosho. Pia kuleta matengo ya kutengea mbung'o kwa ajili ya maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha, mpaka leo Rufiji ina lambo moja tu ambalo lina ukubwa wa mita 50 kwa 50, lina majosho manne na mifugo. Sasa kwa taarifa ambazo Halmashauri imekabidhi kwa Kamati ya Kilimo na Mifugo, inaonyesha kuna mifugo 167,000. Lakini eneo ambalo ilikuwa limetengwa kwa ajili ya ufugaji Rufiji ambapo mpaka sasa Serikali ilikuwa tayari imeshapima ni kwa ajili ya mifugo 36,000 tu. Ndiyo uone, tatizo hili kwa makusudi kabisa limesababishwa na Serikali hii sikivu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, 2011 wakati wa kikao kama hiki cha Bunge la Bajeti, nilipata bahati ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo swalii kwamba Rufiji sasa hali ilishaanza kuwa tete kwa sababu wafugaji wamehama katika maeneo ambayo walitengewa, ambayo hayana miundombinu, wameingia kwenye bonde la Mto Rufiji. Kwa hiyo, sasa kuna mwingiliano baina ya wafugaji na wakulima na mpaka sasa kuna baadhi ya watu wameshapoteza maisha. Hii ilikuwa mwaka 2011 katika Bunge kama hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii sikivu imebaki kimya. Kumbe mimi nilikuwa sifahamu, kumbe nampigia Mbuzi gitaa wakati hana asili ya kucheza muziki. Serikali hii sikivu haikwenda Rufiji kuangalia sasa jinsi gani wanaweza kutatua migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Mpaka mwaka huu mwezi ule uliopita machafuko yametokea tena baada ya Mzee Mtawangala kufariki, ndiyo Serikali hii sikivu ilipeleka magari ya kikojozi, magari ya washawasha mawili, ikapeleka *FFU* wengi sana, inapeleka mabomu mengi sana kwa ajili ya kwenda kuwapiga wakazi wa Rufiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwa sababu Serikali hii sikivu ilieleza wazi katika vitabu vyake, kwamba sasa wanakwenda kwenye mikakati ya kujenga malambo, kutengeneza majosho, lakini hayo hawakuyatimiza, matokeo yake wamepeleka magari ya washawasha na askari wengi wa *Feed Force* kupiga Rufiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niiase hii Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi kwamba Watanzania wa leo wanajua haki zao za kimsingi, wanasoma hizi taarifa ambazo ninyi mnaziandika, wanasikiliza redio, wanaangalia *TV*, wanaona yote ambayo mnayasema, sasa hamwezi kuwaambia kwamba nyeusi ni sawa sawa na nyeupe. Hiyo imeshapitwa na wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo Ikwiriri limefikia katika hatua mbaya, lakini pia tunashukuru mmekuta Kamati mbalimbali, lakini Kamati zote na viongozi wote ambao wamekuja Rufiji wamesema wazi

kwamba malalamiko haya sasa wanayaleta kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuomba watu wa Rufiji utunusuru katika janga hili kwa sababu sasa kuna baadhi ya viongozi wa ngazi za juu kabisa kutoka kwenye Serikali yako wanakwenda Rufiji kufanya uwanja wa kisiasa, badala ya kwenda kutengeneza amani na utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana na Serikali hii sikivu ambayo kila siku inakuwa kiziwi. Bomu lingine la Rufiji naingia kuliuliza, ni suala la ardhi. Baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya mwaka jana, 2011 kuelezea ule mpango kabambe wa *SAGCOT* na alitaja pia bonde la Rufiji litahusika katika mpango ule. Baada ya kutaja jambo lile, tunashukuru sana tulimwona Mkurugenzi wa Rubada Bwana Masanja na timu yake, wamekuja Rufiji wakafanya *study*, lakini nasikitika kukueleza kwamba kumbe *documents* zile ambazo walichukua Rufiji walikuja nazo ofisini kwao na sasa wao wamegeuka kuwa madalali wa ardhi ya Rufiji badala ya kwenda kuendeleza na kupeleka wawekezaji ambao wako sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana, suala la ardhi ni suala muhimu sana, mimi nilitegemea wananchi wa Rufiji leo au wananchi wa Tanzania wale waliobakia wanategemea ardhi katika kuwakomboa katika umaskini. Lakini kumbe sasa ardhi imekuwa bomu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya ardhi Na. 4 na Na. 5 inaonyesha ukomo wa mipaka. Kwa mfano,

imeeleza kwamba kijiji kinaweza ekari moja mpaka 50 Halmashauri ikatoa 50 mpaka 500, kwa kuwa walitambua wazi kwamba katika ngazi ya kijiji hakuna wataalam ambao wangeweza kufanya vizuri kutoa ushauri katika matumizi ya ardhi. Lakini hao wajanja ambao ndio wasomi, maprofesa, madaktari, wanatumia sheria ile ile, udhaifu ule ule kwenda kudhulamu ardhi za watu na kuwapa wawekezaji kwa kwenda kuwarubuni wanavijiji wachache kwa kuwapikia chai na kuwapa Sh. 5,000/=. Hatufiki! Hatutafika, na hii italeta migogoro mikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ardhi ni bomu. Katika bomu ambalo Tanzania sasa hivi tunaelekea kubaya ni suala la ardhi. Tafadhali tunaomba wananchi wa Rufiji tuangalie katika hili kwa sababu kuna mgogoro pale katika Kata ya Chumbi ambayo iko katika Wilaya ya Rufiji, mgogoro huu wa ardhi kama huo wanakwenda wababaishaji, wawekezaji wanakwenda kwa watu wachache wanawanunulia chai, wanawapa Shilingi elfu tano tano kwa kuwa wanatambau kwamba uelewa wao ni mdogo. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hatutafika katika hili, tunaomba msaada wako. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha*)

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchuchuli, Waheshimiwa Wabunge naomba nimwuite

mchangiaji anayefuata na yeze ni Mheshimiwa Godfrey Zambi na nadhani yeze ndio atakayekuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho jioni ya leo. Lakini kabla sijaendelea, naomba niwaeleze Watanzania kwamba mimi ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, kwamba mimi mwana CCM na wale wote wanaondika kwenye vyombo vyaa habari kwamba ni Mpinzani, wanakosea, maana mimi toka utoto sijajua Upinzani mpaka leo nipo CCM na nitaendelea kuwa CCM. (*Makofi*)

Ninayosema hapa Bungeni nataka kuisaidia Serikali yangu ya CCM ili ijisahihishe pale inapopotoka na Watanzania waendelea kuiamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache ya kuzungumza, lakini pia mazito, na mimi naomba Mheshimiwa Waziri unisikilize vizuri. La kwanza, niombe tu Serikali mwaka huu ihakikishe kwamba pembejeo za kilimo kwa wananchi wote katika nchi hii na hususan kule Mbozi ambako tunazalisha sana Mkao wa Mbeya, na kule Katavi Singida, Ruvuma, Lindi, Iringa, Morogoro wanapata pembejeo mapema. Mwaka jana mbolea zimekwenda pamoja na mbegu, mwezi wa Pili, mwezi wa Tatu. Serikali haikutimiza wajibu wake hapa, ninaomba hili lirekebishwe wananchi wapate pembejeo mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba mwaka huu, msimu huu wananchi wote wanaolima mazao yao, walime kama wanavyoona inafaa.

Kitendo kilichofanywa mwaka jana kilikuwa ni kuwadhalilisha wananchi. Wamelima tukawafungia soko, halafu Serikali ikashindwa kununua mazao yao. Hakikuwa kitendo cha uungwana na kwa Serikali inayowajibika hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka nzungumze kwa kirefu kidogo masuala ya kahawa. Nawaomba Wabunge wenzangu mnisikilize, lakini pia na Watanzania wengine wanisikilize na wana Mbozi wanisikilize. Kahawa ni zao ambalo linaingiza fedha nyingi za kigeni kwa wingi sana kama ambavyo punde hivi tumemsikia kiongozi wa upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha kahawa inaonekana sasa kimeanza kupelekwa ndivyo sivyo. Usimamizi wa kahawa umekuwa ndivyo sivyo, Serikali imetaka kuchukua madaraka na kuamulia wananchi nini kifanyike. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nzungumze hivi; hivi karibuni Waziri aliyekuwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Maghembe, aliteua Bodi ya Kahawa. Kwa mujibu wa Sheria ya Kahawa Na. 23 ya mwaka 2001, imepewa majukumu ya kuendeleza zao la kahawa katika nchi hii. Lakini kwa bahati mbaya, Bodi hii ambayo imepewa jukumu hilo imeteuliwa ndivyo sivyo.

Naomba niwaeleze ndugu zangu, mtu ambaye anaiongoza Bodi ya Kahawa, Mwenyekiti ana-*interest* katika suala la jengo la Bodi ya Kahawa pale Moshi, Serikali imeshitakiwa kwa maana ya kwamba jengo lile linadiwe. Kampuni ya Uwakili ambayo inafanya kazi ya Uwakili, mwenye kampuni hiyo ndiyo ameteuliwa kuwa

Mwenyekiti wa Bodi, yaani yeye ambaye amepewa kazi na Benki ya *EXIM* kulinadi lile jengo ndiyo amepewa kazi kuwa Mwenyekiti wa *TCB*. Mnategemea atafanya kazi gani? Huyu ameteuliwa na Mheshimiwa Maghembe.

Pili, mfanyabiashara mmoja mkubwa ambaye anamiliki Kampuni ya Ununuzi wa Kahawa ambaye wakati wowote amekuwa anahimiza kwamba lazima makampuni yanunue kahawa mbichi, yaani cheli kwa wakulima, naye ameteuliwa kuwa kwenye Bodi ya Kahawa, atatenda kazi gani kwenye Bodi hiyo? (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Bodi ya Kahawa kwa mujibu wa Sheria ya Kahawa inasema kwamba Wajumbe wa Bodi watateuliwa kulingana na maeneo yanayolima kahawa katika nchi hii. Mkoa wa Mbeya ni wa kwanza kwa uzalishaji wa kahawa ya arabica katika nchi hii, lakini haujapata Mjumbe wa Bodi hata mmoja na wengine wakasema mimi nasema kwenye magazeti kwa sababu nalilia ujumbe wa Bodi, sijawahi kulilia ujumbe wa Bodi hata siku moja na wala sina sababu ya kuulilia, lakini nasema kwa maana ya kuwawakilisha Watanzania. (*Makofi*)

Wajumbe wa Bodi Mkoa wa Kilimanjaro na hapa, naomba wale wanaofikiri tunazungumza ukabila, wanisamehe, lakini siyo suala la ukabila, nataka kuwaeleza ukweli. Mkoa wa Kilimanjaro wenye Wajumbe tisa, Mkoa wa Kilimanjaro una Wajumbe watano? (*Kicheko*)

Mmewahi kusikia wapi, Waziri aliyeteua anatoka Kilimanjaro? Unafikiria nini hapo? Unahitaji Roho Mtakatifu akushukie kwamba hapa kuna ukabila au kuna ukanda? (*Makofi*)

Hapa lazima Waziri anayehusika alitumia Ofisi ya Serikali vibaya na mimi nina hakika Wajumbe wa Wabunge wa CCM waliposema baadhi ya Mawaziri hawafai, tulikuwa tunasema kwa misingi hiyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu mfikishie Mheshimiwa Rais kwamba baadhi ya Mawaziri hawatendi wajibu wao sawa sawa, hawawatendei Watanzania sawa sawa. Kama wataendelea kusema hivyo, nitaendelea kuwaambia Watanzania Mawaziri moja, mbili, tatu, hawafai. Msione aibu kuwaondoa, maana hawa ndio wanaoidhalilisha Serikali ya Chama cha Mapinduzi mbele ya uso wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetungwa kanuni za zao la kahawa. Kanuni hizi zinaitwa za mwaka 2012. Katika hali ya kawaida, ulitegemea wadau ndio wamshauri Waziri au Waziri apate mawazo kwa wadau wa kahawa? Hakuna kikao cha *stakeholders* au wadau wa kahawa kilichokaa kushauri kanuni zile au hata baada ya kutungwa zipelekwe kwa kikao cha wadau. Tulikwenda Moshi mwezi Juni, 2010 Wajumbe kama 30 tulialikwa kwa ajili ya *workshop*, wenzetu Wizara wakachukulia kile kikao kama cha wadau na wakasema eti kwenye kikao hicho tulizungumzia suala la cheli kwamba lazima liwekwe kwenye kanuni mpya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba wakupe muhtasari kwenye kikao hicho, kama utaona kuna sahihi ya Mwenyekiti au sahihi ya Katibu,

kinachofanyika pale ni kiini macho. Wametayarisha muhtasari, uonyeshe kwamba kile kikao cha mwezi Juni pale Moshi kilikuwa kikao cha wadau, lakini hakikuwa kikao cha wadau na kwa sababu Waziri alikuwa na nia ya kulisukuma hili, basi wakaona wafanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi haiwezi ikaongozwa namna hiyo hata kidogo! Mimi nilipokuwa kwenye kikao cha wadau Morogoro, tarehe 24 na 25 nilitofautiana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, kwamba kanuni kama zinatungwa na Waziri, anakaa na wataalam wake, hatuwezi tukazichukua kwamba zimetungwa na wadau. Nilimwambia Katibu Mkuu wa Wizara - Ndugu Muya kwamba mimi siko tayari kunyamaza juu ya hili, maana kanuni zimetungwa na binadamu na kanuni siyo Biblia wala *Quran* hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomwambia mwananchi huyu auze kahawa yake kule shambani ambayo ni *semi washed* ile mbichi, maana yake unataka huyu mwananchi aendelee kuwa maskini daima. Kahawa yetu ambayo inakuwa *full washed* kama inapita kwenye *CPUs*, na nataka niwahakikishie Watanzania kwamba Mbozi tuna *CPUs 89* ambazo zinamilikiwa na wananchi wakulima. Lile suala la kwamba wananchi hawa hawawezi kutunza kahawa yao wakakoboa wenyewe siyo la kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la Kanuni zilizotungwa kinyemela na wataalam wa Wizara na Waziri akasaini tarehe 19 zifutwe mara moja ili kanuni zitakazotungwa nyingine zipite kwa wadau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana namna ambavyo Bodi imesukuma hizi kanuni. Bodi imeteuliwa, ikasukuma kanuni wakatoa leseni haraka kwamba ziende kule kwa wananchi na makampuni haya yaanze kununua kahawa mara moja. Kanuni hata hizi zilizotungwa bado zinataka wale wanaokwenda kununua kahawa wapite kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, lakini Bodi ambayo Mheshimiwa Maghembe ameiteua, imelazimisha kwamba ninyi mkishapewa leseni kwa maana ya wanunuzi, nendeni tu kwa mkulima mmoja mkanunue kahawa. Hakuna kupita hata kwa Wakurugenzi, ninavyosema hapa, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wangu anasikia, tulishakubaliana katika ngazi ya Mkoa kwamba jamani eeh, biashara hizi zinawanyonya wakulima.

Kwa hiyo, hakukuwa na sababu ya Waziri ambaye ulimtuma Mbeya Mheshimiwa Waziri Mkuu, akaja yeye mwenyewe na akaona wananchi wakamkatalia juu ya suala la Cheli, bado anakuja kusaini kanuni kuruhusu Cheli. Sasa mimi nadhani huu ni ujeuri tu, maana Waziri anajenga hoja kwamba Zambi naye anafanya biashara ya kahawa. Mimi sijawahi kufanya biashara ya kahawa, na wala sitegemei kufanya biashara, nawatetea Watanzania wale ambao wanavuja jasho ili waweze kupata haki ya mazao yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii viko vyombo vinafanya kazi. Kama mnataka kumtafuta Zambi kwamba anafanya biashara hiyo, ndiyo sababu anajitetea kama na ndugu yangu nimeweka pesa, nimefanya nini, nichunguzeni, siwezi kunya mazishwa kwa sababu eti na mimi nafanya biashara ndiyo kinakuwa kisingizio cha Waziri, hata kidogo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi naomba niseme sitaunga mkono bajeti yako, mpaka utoe tamko kwa mambo mawili, kuvunjwa kwa Bodi hii, lakini pia kanuni hizi ziangaliwe upya ili Watanzania tuweze kuwatendea haki. Sitaunga mkono, na naomba Wabunge wenzangu wenyе nia njema tusiunge mkono bajeti ya Waziri Mkuu mpaka atoe maelezo ambayo yanaeleweka katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, suala la Kiwira limekuwa linazungumzwa sana, wafanyakazi wa *Kiwira Coal Mine* wanaishi kama watoto yatima ambao hawana baba wala mama. Wanaishi kama hisani, leo wanapewa laki moja, leo laki mbili ndivyo wanavyoweza kuendesha maisha hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu tuone kwamba hii ni aibu ya nchi, watu wako pale wanakaa, Serikali haiwezi kuchukua maamuzi. Viko vyombo katika hii Serikali ambayo ziko tayari kuwekeza pale, lakini kwa sababu ambazo hazieleweki, Serikali bado inasuasua katika kuchukua maamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunataka utoe tamko rasmi juu ya mambo ya Kiwira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo kamili juu ya mambo hayo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndio Weston Zambi, Mbunge kutoka Mbozi na ndio amehitimisha mchango wetu wa siku hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, labda tu niseme mchangiaji wetu kesho atakuwa ni Mbunge kutoka Visiwani na yeye sio mwingine, ni Mheshimiwa Maryam Msabaha ndio atatufungulia mchango wa majadiliano kesho na Waheshimiwa Wabunge wengine watakaofuata, basi atakayekuwa ameketi katika Kiti hiki atatoa mwongozo wa Wabunge wengine watakaofuta kuendelea kuzingatia hayo hayo; uwakilishi wa Kambi ya Upinzani, Chama tawala, *gender* kwa maana ya wanawake, wanaume na kadha wa kadha. Naomba tu niseme hayo.

Maombi ya kuchangia hotuba hii mpaka sasa wachangiaji wameshafika 118 na sina uhakika sana kama tunaweza kuwafikia wote, lakini tutaendelea kuangalia tunakwendaje. Hawa ni wale ambao hawajachangia hata mara moja. Wale waliokwisha kuchangia angalau mara moja hao nao katika orodha yangu wameshafika 44. Kwa hiyo, tutaendelea kwanza kuwapa kipaumbele wale ambao hawajawahi kuchangia hata mara moja kwenye kipindi hiki cha Bunge hili la Bajeti, kwa maana ya kwamba hawa waliokwisha ni wale waliokwisha kuchangia hotuba ya bajeti iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kushauriana katika Kiti na kuangalia utaratibu mzuri wa uendeshaji wa shughuli ndani ya Bunge, na baada ya hayo, naomba niwashukuru wote kwa michango yenu.

Sasa naahirisha shughuli hizi za Bunge, tutakutana hapa ndani ya Ukumbi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.44 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 26 Juni, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*